
GOLDLITE ONLINE EDUCATIONAL SERVICES

KCSE SMARTFOCUS QUICK REVISION SERIES




# KARATASI YA TATU
# MSURURU 1 -40
















**2025 EDITION**

**FOR MARKING SCHEMES INBOX 0724351706 or visit our website**

**www.goldlitekcserevision.co.ke**

MTIHANI 1

**SEHEMU A: RIWAYA**

**Clara Momanyi:** *Nguu za Jadi*

1. **Lazima**

   i. "Kuna waliomwita mnyakuzi huku wengine wakimwita dudumizi kwani alinyemelea viota vya wengine. Hajengi bali hubomoa."

   a) Jadili sifa **nne** za anayerejelewa katika dondoo. (alama 4)

   ii. **"Karibu mwenzangu. Subiri nikuletee kikombe cha chai''**

   "Hata usilete,sin a hamu ya chai mwenzangu. Nina machungu moyoni. Ndiposa nimekuja unisaidie kuyapanguza … kuyamaliza hutaweza."

   a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

   b) Fafanua umuhimu wa msemaji wa **maneno yaliyokolezwa** katika kuendeleza ploti kwenye riwaya *Nguu za Jadi*. (alama 4)

   c) Eleza machungu ambayo msemaji wa maneno yaliyokolezwa anayo moyoni, ambayo angependa asaidiwe kuyapunguza katika riwaya Nguu za Jadi. (alama 4)

   d) Jadili mbinu ambazo Mtemi Lesulia alizitumia kubakia uongozini ukirejelea riwaya *Nguu za Jadi*. (alama 4)

**SEHEMU B: TAMTHILIA**

**Timothy Arege:** *Bembea ya Maisha*

*Jibu swali la 2 au la 3.*

2. "Haikuwa mara moja mnavyofikiria. Ilianza pale chuoni. Wenzangu walinipa mvinyo kunirai kuonja ulevi."

   a) Eleza muktadha wa maneno haya. (alama 4)

   b) Kwa hoja **nne**, onyesha athari ya ulevi katika maisha ya mzungumzaji. (alama 4)

   c) Onyesha umuhimu **sita** wa mandhari ya dondoo hili. (alama 6)

   d) Mzungumzaji ameendeleza maudhui ya mabadiliko. Thibitisha ukirejelea tamthilia *Bembea ya Maisha*. (alama 6)

3. "Mtu ana ubaguzi kama nini! Ana moyo mgumu kama jiwe! Amejaliwa lakini bahili kama mchanga wa dhahabu. Hajui mali ya bahili huliwa na wadudu."

   a) Bainisha mbinu **nne** za kimtindo zilizotumiwa katika dondoo. (alama 4)

   b) Mzungumzaji anaashiria kwamba anayerejelewa alikuwa mchoyo. Onyesha kina cha kauli hii ukirejelea tamthilia *Bembea ya Maisha*. (alama 6)

   c) Jadili jinsi maudhui yafuatayo yalivyoshughulikiwa katika tamthilia *Bembea ya Maisha*. (alama 10)

      i. Usasa

      ii. Taasubi ya kiume

**SEHEMU C: HADITHI FUPI**

**D.W. Lutomia na Phibbian Muthama (wah.)**: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 4 au 5*

**Yussuf Shoka Hamad:** *Mzimu wa Kipwerere*

4. "Katika kijiji hiki kuvuta kileo chochote aina ya tumbaku kulikuwa marufuku na kungeweza kugharimu hata maisha ya mtu. Vilevile, kubwia unga na hata kunywa pombe yalikuwa makosa ya jinai ingawa pamoja na juhudi zote hizi kuzuia dawa kama hizi, mji wa watawa uliongoza kwa uingizaji, usambazaji na hata utumiaji wa vileo na dawa za kulevya, ukizingatia kuwa mambo yote haya yalikuwa yamepigwa marufuku na mzimu na yalimlazimu kila mtu kuyazingatia. … hayakuwa maswali rahisi kujibika si kwa sisi tu wahenga, bali hata mzimu wetu bila shaka haukuwa na jibu!"

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Dondoo hili limetawaliwa na mbinu **moja kuu** ya kimtindo. Itaje na uithibitishe. (alama 2)
c) Kwa hoja mwafaka, eleza jinsi suala la unafiki linavyojitokeza kwenye dondoo hili na katika hadithi nzima ya *Mzimu wa Kipwerere*. (alama 9)
d) Bainisha toni inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
e) Fafanua vigezo **vitatu** unavyoweza kuzingatia katika kutambua sifa za wahusika kwenye hadithi *Mzimu wa Kipwerere*. (alama 3)

**Mzamane Nhlapo:** *Nipe Nafasi*

**5.** "Jamii na serikali zinatunyima sisi wanawake uhuru.…Kabla sijafa, nataka kwanza niwe nimepata nafasi ya kuyaboresha maisha yangu na yale ya wanangu."

a) i. Taja asasi **mbili** za jamii zinazotumiwa kuwakandamiza wanawake. (alama 2)
ii. Huku ukirejelea hadithi ya *Nipe Nafasi*, fafanua jinsi jamii na serikali zimewanyima wanawake uhuru. ( alama 7)
iii. Jadili juhudi **tano** za mzungumzaji katika kuyaboresha maisha yake na maisha ya wanawe ukirejelea hadithi *Nipe Nafasi*. (alama 5)

**Paul Ngángá Mutua:** *Harubu ya Maisha*

b) "Mwenyewe wajua mimi sipendi mambo ya kukopa. Isitoshe mimi nimekuja hapa likizo. Sasa zimekatika wiki mbili nawe huyo na kazi tu."
Fafanua umuhimu **sita** wa mzungumzaji wa maneno haya katika kuijenga hadithi *Harubu ya Maisha*. (alama 6)

**SEHEMU D: USHAIRI**

*Jibu swali la 6 au 7*

**6.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali*.

Pana haja ya kupima, neno tuzowele –angu
Tusizowee kusema, hili ni teuo langu
Huenda huji mapema, -angu huja kuwa tungu
Ikaja kukusakama, na kukuposha kwa Mungu
Pana haja ya kupima.

Neno huwa ni la kwako, likiwa ndani moyoni
Lakini katu si lako, likishavuka menoni
Kwa hivyo likutokako, liweke kwenye mizani
Linaweza kuwa cheko, ama tusi kwa wendani
Pana haja ya kupima.

Vivyo hivyo kwa lebasi, huwa yako kisutuni
Hivyo nina wasiwasi, wambe yako sebuleni
Itavutiya matusi, ya wenzio insane
Wakakuchoma nafusi, kwa mishale ya lisani
Pana haja ya kupima.
Mwana ujuwe ni wako, punje ukiimezele
Lakini katu si wako, nde ukimuletele
Akiwa yu ndani yako, ni wa duniya vivile
Ukishishilia ni wako, muavye takakuole
Pana haja ya kupima.

Maisha nayo si wako, utabaradi milele
Ungayaishi ja yako, ni tunu ya maumbile
Mgawa si kufu yako, mshindane hili lile

Akupapo akupoko, utaishi palepale
Pana haja ya kupima.

Ni chetu chako si chako, ulimwengu huwa vile
Juhudi zingawa zako, wa kufaidi ni wale
Ikifika siku yako, nyono zikukae mbele
Ulichosema ni chako, huwabakiya wawale
Pana haja ya kupima.

Kaseme na moyo wako, Ubaini haya yale
Ukiambacho ni chako, kisikupe mageule
Kitu utajacho chako, huenda kiwe cha wale
Na usemacho si chako, kiwe chako ndicho kile
Pana haja ya kupima.

***Maswali***

a) Fafanua dhamira ya mwandishi wa shairi hili. (alama 2)
b) Pambanua bahari zozote **tatu** za shairi hili. (alama 3)
c) Dhihirisha kwa kutoa mifano matumizi ya uhuru wa mshairi. (alama 6)
d) Tambua toni inayojitokeza kwenye shairi hili. (alama 2)
e) Andika ubeti wa **nne** kwa lugha tutumbi. (alama 4)
f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika shairi . (alama 2)
   i. Lebasi
   ii. Punje ukiimezele

**7.** *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali*
Daima alfajiri na mapema
Hunipita na jembe na kotama
Katika njia iendayo kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na kubwa hamu
Kushika mpini na kutokwa na jasho
Ili kujikimu kupata malisho.
Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbwiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia;
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimletea
Nao umande kumbusu miguu
Na miti yote hujipinda migongo;
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akicheka ha ha ha ha ha ha…

Na mimi hubaki nikijiuliza
Kuna siri gani inamliwaza?
Au ni kujua au kutokujua?
Furaha ya mtu ni furaha gani?
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao.

Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Anayalimia matumbo ya waroho
Kuna jao gani linamridhisha?
Laiti angalijua, laiti angalijua!

**Maswali**

a) Fafanua hali ya mzungumzaji katika shairi hili. (alama 5)
b) Tambua aina **tatu** za taswira zinazojitokeza katika ubeti wa pili wa shairi hili. (alama 3)
c) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. (alama 1)
d) Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)
e) Bainisha vipengele **vinne** vya kimtindo katika shairi hili. (alama 4)
f) Pambanua muundo wa shairi hili. (alama 4)
g) Tathmini umuhimu wa maswali balagha katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

***8.*** *Soma utumgo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata*

Walikuja mahasidi, ah,
walikuja
Nyayo zao zikirindima, ah,
rindima
Kwa ghamidha ya uadui, oh
uadui
Wali wakibeba sime
Wali wakibeba mata
Wali wakibeba mienge
Ya moto kutangazia
Kwao kuwasili

Walikuja kwa ndimi
zilizohimili cheche
matusi kutumwaiya
hawakujua ya kwamba
Mbele ya mhimili huno
wetu
Wao wali vipora
Kwenye mlima wa sugu,
walituvamia
Aliwakabili mbwene
Mwana wa ngwamba, ee
mbwene
Aliwakabili mbwene kwa
kitali kikali
Wali wametuteka ja samaki
kwenye dema
Wali wamewapukutisha
Wetu mabarobaro
Aliwakabili mbwene
Ee mbene, mwana wa
ngwamba
Aliwakabili

Kwa hamasa za ujana
Kwa uchungu wa
kuumbuliwa
Wa wetu wana.

Aliwakabili mbene
Nao wakalipiza shambulizi
Kwa kujidai majagina
Walijibwaga uwanjani
Laiti wangalijua
wanajikabidhi
Viganjani mwa mbwene
Aliwakabili mbwene , ee
Mwana wa ngwamba, shujaa asoshindwa
Alipigana kitali
Cha kufa na kupona
Kuiopoa jamii yetu kuirejesha hadhi yetu
Kuirejesha mifugo yetu
Kuwarejeshea wakulima vikataa vyao
Kuwaokoa vipusa wetu
Nyara waliotekwa, ati walipiza kisasi
Aliwakabili mwana wa ngwamba
Aliwakabili upepo wa kusi
Hata kikomo cha mapambano kilipofika
Wagundi walijua kwamba
Walikuwa na mwana, ee mwana
Mbwene, ee mwana wa ngwamba
Hakuwa na kifani, ee kifani
Alipigana nao, ee mwana wa ngwamba
Kwa siku kumi bila tonge wala tone la maji
Kwetu kukenda kicheko cha wokovu
Kwao kukenda kilio

**Maswali**

a) Huu ni wimbo wa sifa. Thibitisha kwa kutolea mifano **mitatu** kifunguni. (alama 3)
b) Bainisha sifa **tatu** za jamii ya nafsineni katika utungo huu. (alama 3)
c) Huku ukitolea mifano, bainisha vipengele **vinne** vya kimtindo ambavyo nafsineni ametumiakufanikisha uwasilishaji wa utungo huu. (alama 4)
d) Tungo za aina hii zinaendelea kufifia katika jamii yako. Fafanua hatua **nne** utakazochukua ili kuishawishi dhidi ya hali hii. (alama 4)
e) Jadili mbinu zinazoweza kutumiwa kukusanya na kuhifadhi data kuhusu vitanzandimi. (alama 4)
f) Fafanua njia **mbili** ambazo kwazo msikilizaji anaweza kuchangia katika uwasilishaji wa kipera hiki. (alama 2)

MTIHANI 2

## SEHEMU A: USHAIRI

1. **Lazima**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Piiiiiip piiip pooop poooop piiip piiip!
Ni mlio wa gari letu
Tayari kwa safari yetu
Safari ya maisha yetu; ya kutukwamua
Kutoka kwenye mikatale ya nyangumi
Nduli! Shetani! Ibilisi! Baradhuli! Punda Mgonjwa.
Yote hayatoshi
Ya kina maelezo kutoa kumhusu.

Ninakumbuka bayana
Kaski nemsi mafungulia bakari huonekana

Ila

Kaski hiyo, nemsi haikuwa
Kaski hiyo, hali mbadala
Kaski hiyo, jinamizi; tanzia
Kaski hiyo, simanzi litanda
Kaski hiyo, ubahaimu lipandwa ardhini, ikamea na kuzaa.

Ukweli ni kwamba,
Wakufunzi, wenye jukumu la kunoa wanagenzi
Mstari wa mbele walijipanga, ubahaimu kutenda.
Maswali, kwa bidii walifungasha
Tafiti wakazamia; kinga na kinga moto ukawaka.
Moto ambao ungekuja kuteketeza kizazi cha usoni.
Majibu, na tochi yalisakwa na kumiminwa akilini mwa watafutiwa
Uadilifu, teke ukapigwa, na kaburi la sahau kuzikwa.
Wakati hupo lakini; hayo kubainika mwiko yalikuwa.

Mwongo mmoja sasa umepita
Hali tenge tahani,
Vyuo vikuu na vya kiufundi
Mahafali wamimina taifani.

Akaaa!

Wahandisi, majumba yawaporomokea
Mawakili, kesi zawaponyoka; kubwa kwa dogo, jepesi kwa gumu
Majaji; haki wanajisi kisa na maana, ughushi
Matabibu na wauguzi; wateja wao jongomeo wapiga foleni
Marubani; ndege zashindana ardhini kutapakaa

Wakufunzi kuelewa wanachofanya, nadra kama wali wa daku
Mahasibu, uadilifu dirishani metokea; hesabu chenga yawapiga.
Maaskofu matumbo mbele wameweka, sadaka wafakamia.
Wanasiasa kusazwa hawajaachwa
Mstari wa mbele katika ufisadi; huku wakiendeleza ukosefu wa ajira.
Maafa, vifusi, mabaki ya ndege na garimoshi,
Utamaushi, msongo wa mawazo, tama na ubinafsi mejaa kila kukicha.

Waama! Waama! Waama!
Hakika! Hakika! Hakika!
Hali tulimo kwa kweli
Ni msiba wa kujitakia
Usokuwa na kilio?
Mwiba wa kujidunga
Usoambiwa pole?
Ni ngumi tulopiga ukutani
Na kuumiza mikonetu?

Gari letu sasa hivi, nanga imeshangóa
Uadilifu kwa hakika, mizizi inataka kukita
Ili jamii kwa kweli, najisi tufagie
Na kufutilia mbali, doa iloshamiri.
Kama si sisi, ni nani atakayemaliza ubahaimu huu?

**Odindo Adinda**: *Diwani ya Mchonyoto na Mashairi Mengine*

a) "Ubahaimu unaoyerejelewa una ila nyingi." Fafanua kwa mujibu wa shairi hili. (alama 6)
b) Pambanua umbo la shairi hili. (alama 3)
c) Tambua toni inayojitokeza kwenye ubeti wa **saba** wa shairi hili. (alama 2)
d) Onyesha namna mshairi alivyofanikisha mbinu zifuatazo za kimtindo:
   i. Kejeli katika ubeti wa **tano** (alama 2)
   ii. Aina za takriri (alama 2)
   iii. Aina mbili za taswira (alama 2)
e) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. (alama 3)

## SEHEMU B: TAMTHILIA

**Timothy Arege**: *Bembea ya Maisha*

***Jibu swali la 2 au 3***

2. "Gongo liliyamega maadili yake kimyakimya na taratibu uwajibikaji ukawa umemponyoka na kuteleza kama sabuni ya povu jingi na kumwacha na kisomo chake tu."

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Changanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)
c) Jadili umuhimu wa msemaji wa kauli hii katika kujenga tamthilia *Bembea ya Maisha* *(alama 5)*

d) Tathmini madhara ya gongo linalorejelewa kwa jamii ukirejelea tamthilia *Bembea ya Maisha*. (alama 7)

3. "Tamaduni, mila na desturi zetu zinazidi kuyakubali mabadiliko. Thamani ya mtoto wa kike imepanda na nafasi yake kupanuka."

   a) Thibitisha kwa hoja **kumi na mbili** maneno yaliyopigiwa mstari ukirejelea tamthilia *Bembea ya Maisha*. (alama 12)

   **b)** Eleza tamaduni, mila na desturi **nane** za jamii inayorelewa katika tamthilia *Bembea ya Maisha*. (alama 8)

## SEHEMU C: RIWAYA

**Clara Momanyi**: *Nguu za Jadi*

***Jibu swali la 4 au 5***

4. i) "Alisikia jina lake likitajwa kuwa miongoni mwa wanawake walioleta mabadiliko makubwa ya vijana nchini, hasa wa kiume."

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

   b) Kwa hoja **kumi**, fafanua mchango wa mrejelewa, na wengine wa jinsia yake katika ujenzi wa jamii mpya kwenye riwaya *Nguu za Jadi*. (alama 10)

   ii) Jadili umuhimu wa mandhari ya *Ponda Mali* katika kufanikisha **ploti** kwenye riwaya *Nguu za Jadi.* (alama 6)

5. "… hawakujali kuwa haki ndiyo inayoinua taifa. Kwamba johari hii ikiadimika, basi taifa liko hatarini. **Matuo ilikuwa ikididimizwa taratibu na wanaoabudu ukunguni**. Laiti wangalichagua jina jema kuliko mali nyingi!"

   a) Tambua toni inayojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

   b) Thibitisha ukweli wa kauli iliyokolezwa, kwa hoja **kumi**, ukirejelea riwaya *Nguu za Jadi.* (alama 10)

   c) Onyesha mbinu ya kimtindo inayojitokeza katika kauli iliyopigiwa mstari inavyotumika katika riwaya *Nguu za Jadi.* (alama 8)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

**D.W. Lutomia na Phibbian Muthama (wah.)**: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

*Jibu swali la 6 au 7*

**Winnie Nyaruri Ogenche:** *Sabina*

6) i) **Mizizi ya elimu ni michungu ila matunda yake ni matamu**. Ikiwa mnataka kuyaonja matunda ya elimu, lazima mtie bidii kwani mtaka cha mvunguni sharti ainame."

   a) Pambanua aina **nne** za taswira zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

   b) Thibitisha ukweli wa kauli iliyokolezwa kwa mujibu wa hadithi *Sabina*. (alama 8)

**Dominic Maina Oigo:** *Kifo cha Suluhu*

ii) Jadili umuhimu wa barua ya Bi. Suluhu kwa Bwana Suluhu katika kufanikisha hadithi *Kifo cha Suluhu*. (alama 8)

**Douglas Ogutu:** *Toba ya Kalia*

7) i) "Kila mzazi humtakia mwanawe mema ila wakati mwingine hutumia mbinu mbovu."

Fafanua madhara ya mbinu kuu iliyotumiwa na warejelewa kumfikisha msemaji katika kilele cha ufanisi ukirejelea hadithi *Toba ya Kalia.* (alama 7)

**Mzamane Nhlapo:** *Nipe Nafasi*

ii) "Kabla sijafa, nataka kwanza niwe nimepata nafasi ya kuyaboresha maisha yangu na yale ya wanangu."

Onyesha vikwazo **saba** vinavyolemaza juhudi za msemaji na wenzake za kutekeleza kauli hii ukirejelea hadithi *Nipe Nafasi*. (alama 7)

**Phibbian Muthama:** *Nilitamani*

iii) "Nilikuwa na tumaini, naamini japo kwa kiasi fulani nilitamani na kutaka. Nilipanda ngazi kutoka kutamani na kuanza kutaka."

**"Tamaa mbele mauti nyuma."** Thibitisha kauli hii kwa hoja **sita** kwa mujibu wa hadithi *Nilitamani*. (alama 6)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8) ***Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali yanayofuata.***

"Kama kesho itapambauka
Jua la kinjano kuchomoza
Kuangazia siku mpya
Siku iso tumaini
Siku bila mimi na mama mtu
Kumbuka ewe kipenzi
Usiache chozi kufurika
Kiyeyusha makini yako inuka, mwanangu inuka
Silie daima, yote tatengenea."

Mpenzi mama ulolala usingizi usio na mzindushi
Nalikumbuka vyema hili ni beti uloniandikia
Kitandani ukiwa, ukiuguza donda
Donda walokusababishia walimwengu mahasidi
Ela nataka ujue, kamwe yote si shwari kwa mlezi kikembe
Hayawezi tengenea kwa yatima alozungukwa
Na waja wenye tamaa kila kitu kurithi
Hayawezi kuwa shwari kumtaza mwenzio,
        Ulotwambia tumwite baba na kumstahi
        Ati ni amri ya Muumba.
Akitoka na muhebi, pumbao apate yeye
Wafurahia ulochuma wewe.
Najitahidi mpenzi mama
Ukakamavu kujipa
Machozi kuyafuta
Ela hino kumbuka
Kuondoka kwako huko

Hatukukutarajia, japo hukuisha kunikumbusha
Ziraili liliingia ja mwewe
Na kukwiba mithili ya kifaranga
Mama yake akitazama.

***Maswali:***

a) i. Ainisha utungo huu kwa kuzingatia kipengele cha maudhui. (alama 1)
   ii. Fafanua sababu **tano** zinazothibitisha jibu lako katika swali la a (i). (alama 5)

b) Bainisha sifa **mbili** za jamii inayosawiriwa katika utungo huu. (alama 2)

c) Tambua toni utakayotumia katika uwasilishaji wa kipera hiki. (alama 2)

d) Unanuia kutumia mbinu ya kushiriki katika utafiti wa kipera hiki. Pambanua manufaa ya kutumia mbinu hii. (alama 5)

e) Jadili jinsi viziada lugha vinatumiwa katika kukuza vipera mbalimbali vya fasihi simulizi shuleni mwako. (alama 5)

MTIHANI 3

**SWALI LA LAZIMA**
**1. SEHEMU YA A: USHAIRI**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Amka amsha mwili,ukanyage ardhini
Amka pia akili,usingie mashakani
Amka kiwiliwili,usingizi ulaani
Amka fanya shughuli,nchi ipo hatarini

Amka wewe jasiri,hivi unalala nini?
Amka sio kuzuri,umetegemea nini?
Amka kuna dosari ,mchanga kitumbuani
Amka fanya shughuli,nchi ipo hatarini

Amka wewe jen Zi,amsha pia jirani
Amka kipya kizazi ,usikubali uhuni
Amka ufanye kazi,mkono wende kinywani
Amka fanya shughuli, nchi iko hatarini.
**(Chotara Mswahili)**

**Maswali**
**a)**Liweke shairi hili katika bahari tatu huku ukidhibitisha. (alama 3)
b)Eleza dhamira ya mshairi. (alama 3)
c)Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
d)Eleza mbinu ambazo mshairi ametumia kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
e)Tambua mbinu tatu za lugha alizotumia mshairi. (alama 3)
f)andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama4)

**SEHEMU YA B: Tamhilia –Timothy M Arege:Bembea ya Maisha**
**Jibu swali la 2au la 3**
**2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata:**
...lakini ndio tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama... kama... kama... kama vile tambara bovu.
a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza umuhimu wa msemaji katika kukuza ploti. (alama 4)
c)Tambua mbinu nne za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)
d)Kwa kutoa hoja nane kutoka kwa Tamthilia eleza ni vipi utamaduni ulivyothaminiwa katika jamii hii ya Bembea ya Maisha. (alama 8)

**AU**

3.Jadili nafasi ya mwanamke katika jamii ya Bembea ya Maisha. (alama 20)

**SEHEMU YA C:Riwaya ya Nguu za Jadi-Prof Clara Momanyi**
**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuta ;**
*Watategemewa na nani maishani? Hiki ndicho kizazi cha kesho au kizazi kilichopotea tayari?*

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b)Tambua toni katika mazungumzo haya. (alama 2)
c)Onyesha ni vipi kizazi cha leo na cha kesho kilivyopotea. (alama 12)

**AU**

**5.**Fafanua ufaafu wa anwani ya ,'Nguu za Jadi'. (alama 20)

**SEHEMU YA D: Diwani ya Mapambazuko ya Machweo na Hadithi zingine.**
**Jibu swali la 6 au la 7**
**6.Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuata.**
*Akainama chini kwenye tendeguu moja la kitanda cha besera.Akachukua kibatari cha kiberiti ili awashe taa.Mimi,nikiwa mle mvunguni.sasa kwa hakika nilishamjua shetani wa mzimu ule ni nani.Kumbe hakuwa shetani wala Kipwerere*!
a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
b)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)
c)Onyesha umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (alama 4)
d)Wanakijiji waliuogopa mzimu wa Kipwerere kiasi cha kuuabudu na kutoufanyia mzaha. Thibitisha kauli hii. (alama 8)

**AU**

**7.** Kimyakimya analikariri;
*Mteule nimechoka ,kila siku kusikiya,*
*Vyereje nchi hakika,visanga kupindukiya,*
*Tunazidi filisika ,**walaji kujijaziya***
*Msiba kujitakia, kweli hauna kiliyo.*

a)Huu ni ubeti wa shairi katika hadithi"Msiba wa Kujitakia'.Eleza sababu ya mwandishi kutumia mbinu hii katika usimulizi.
(alama 6)
b)Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari katika dondoo. (alama 8)
c)Bainisha maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika kifungu hiki. (alama 6)

**SEHEMU YA E :FASIHI SIMULIZI**
**8)**. (a) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya vitanza ndimi. (alama 2)

(b) Fafanua majukumu sita ya vitanza ndimi katika jamii. (alama 6)

(c) Eleza mbinu sita utakazotumia katika kukusanya na kuhifadhi habari kuhusu vitanza ndimi. (alama 12)

**MTIHANI 4**

**SEHEMU YA A: NGUU ZA JADI** **(ALAMA 20)**

**1. SWALI LA LAZIMA**

"Ndugu zangu, ukabila ni sumu ya nyoka. Ukabila huangamiza maendeleo ya nchi hata kama imestawi kiasi gani."

a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)
b) Eleza umuhimu nne wa msemaji wa kauli hii. (alama 4)
c) Onyesha mbili za uandishi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
d) Kwa kutumia hoja zisizopungua kumi, jadili maudhui ya ukabila yanavyojitokeza katika riwaya hii. (alama 10)

**SEHEMU YA B: BEMBEA YA MAISHA**

**JIBU SWALI LA 2 AU LA 3**

**2**. Wanasema kuwa Mungu hamtupi mja wake. Kweli iliyoje!

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Fafanua sifa za msemaji. (alama 4)
(c) (i) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 6)
(ii) "Lakini inakujuzu uelewe kuwa dunia ni nyumba ya mtihani." Onyesha ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya *Bembea ya Maisha*. (alama 6)

**AU**

**3**. (a) ***Changanua mbinu za kimtindo katika dondoo lifuatalo***. (alama 8)

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (Kimya). Siku hazigandi wala jana haitarudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (Kimya). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (Kimya). **Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya**. Maisha mapya. Pombe! (kama anayesemea pombe). Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu.

(b) Kauli iliyokolezwa wino katika dondoo inadokeza nia ya kubadilika kwa mzungumzaji. Kwa kurejelea tamthilia nzima, onyesha jinsi mwandishi alivyoshughulikia suala la mabadiliko. (alama 12)

**SEHEMU YA C: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO**
**JIBU SWALI LA 4 AU LA**
**4. MSIBA WA KUJITAKIA** **(ALAMA 20)**

"Tayari alikuwa amefanya kosa. Kosa ambalo alifahamu lilikuwa la kujitakia."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Bainisha toni inayodokezwa na dondoo hili. (alama 2)
c) Hadithi ya *Msiba wa Kujitakia* ina matukio mengi yanayoonyesha kinaya. Thibitisha. (alama 6)
d)"Tamaa mbele mauti nyuma." Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi: Nilitamani. (alama 8)

**AU**

**5.** Jadili jinsi maudhui ya **usaliti** yanavyojitokeza katika hadithi zifuatazo: (alama 20)

i. Toba ya Kalia
ii. Kifo cha Suluhu
iii. Fadhila za Punda
iv. Mapambazuko ya Machweo

**SEHEMU YA D: USHAIRI**
**6. SHAIRI HURU** **(ALAMA 20)**

***Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali***

Nimeyaandika maneno haya
Kwa niaba ya:
Mamilioni wasio malazi
Wabebao vifurushi vilivyo wazi
Wazungukao barabarani bila mavazi
... milki yao ya Maisha.
Kwa niaba ya:
Maelfu wanouawa bila haki
Wiki baada ya wiki
leo sumu au spaki
leo kamba au bunduki
na kwa wale wanosubiri kunyongwa.

Kwa niaba ya:
Vijana walio mitaani
wale mayatima wa maskini
wazungukao mapipani
kila pembe mjini
kuokota sumu kutia tumboni
kujiua bila kujua
ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza

walao chakula kilichooza
wachukuao choo wakijipakaza
polepole wakijiangamiza
katika vyumba vyao
baridi na giza
kwa sababu hawana watazama
wala wauguza.

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
Kwa sababu ya madawa tifutifu
yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
bila ya mtu kuona
    kama kwamba sote tu vipofu,

Na kwa niaba yete sote;
Tuliofungwa vifungoni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani
Tuliopokonywa maoni, machoni
Tuliotiliwa sumu, malishoni
Tuliodidimizwa kinyesini
    ili ‘maendeleo’
    yaendelee kwenda njiani
    huku yakitema machicha ya roho zetu.

**<u>Maswali</u>**

a) Hili ni shairi la aina gani? Tetea jibu lako. (alama 2)
b) Bainisha toni ya shairi hili . (alama 2)
c) Tambua aina tatu za urudiaji zinazojitokeza katika shairi. (alama 3)
d) Huku ukitoa mifano eleza namna mtunzi alivyotimiza arudhi za kishairi. (alama 3)
e) Eleza matumizi ya.
   i) Mistari mishata (alama 1)
   ii) Mistari kifu (alama 1)
f) Bainisha nafsi neni katika shairi hili. (alama 2)
g) Tambua aina za taswira katika shairi hili. (alama 2)
h) Mshairi anazungumza kwa niaba ya watu mbalimbali. Jadili.: (alama 4)

**AU**

**7. *Soma shairi hili kisha ujibu maswali.***

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyahutubu
Wayasome ndugu zangu, wa mbali na karibu
Cha wenye raha na taabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, chenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kuta na kucha twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa *balaa*, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha wenye raha na tabu ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina, Saidi Ali Rajabu
Wengune kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja wenye dini, watiio Wahabu
Mashekhe misikitini, humo hufanya muhibu
Mapadri kanisani, huvihubiri vitabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa, na moyo *kisebusebu*
Tunakaribia kufa, kwa kushindwa kujimudu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
Na mengine sitotaja, msinambe nina gubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

**Maswali**

1. Eleza mambo yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)
2. Ainisha bahari katika shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 3)
   (i) Mpango wa maneno
   (ii) Vipande
   (iii) Vina
3. Onyesha jinsi mbinu alizotumia mshairi kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
4. Onyesha umbo la ubeti wa 3. (alama 3)
5. Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi (alama 4)
6. Mshairi huyu ni bingwa kwa kutumia lugha. Thibitisha. (alama 2)
7. Fafanua toni katika shairi hili. (alama 1)
8. Eleza maana ya neno ***kisebusebu*** kama lilivyotumiwa katika shairi (alama 1)

**8. SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI** **(ALAMA 20)**

Mtoto wetu lala
Mtoto wetu lala
Mama ameenda sokoni
Kununua ndizi, atakuja na ndizi nyingi
Ndizi kubwa itakuwa yako
Utakula yote mtoto wetu
Kwa sababu mama anakupenda
Mama anakupenda
Mtoto wetu lala
Baba ameenda shambani kuvuna
Mimi mlezi wako nitakutunza kwa upendo
Nitakuandalia samaki kama jana
Mtoto wetu lala
Mama anakupenda sana.

**Maswali**

a) Huu ni wimbo wa aina gani. Thibitisha. (alama 2)
b) Taja na uthibitishe shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii asili ya wimbo huu. (alama 2)
c) Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anaimbia nani? (alama 2)
d) Eleza mbinu ambazo mwasilishaji wa utanzu huu anaweza kutumia ili kufanikisha uwasilishaji wake. (alama 2)
e) Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii. (alama 5)
f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii (alama 2)
g) Umepewa wajibu wa kutafiti mbolezi katika jamii yako. Pendekeza mbinu ambazo ungetumia kutafiti kipera hiki. (alama 5)

**MTIHANI 5**
**SEHEMU A: RIWAYA**

**Clara Momanyi: Nguu za Jadi**

1. **Lazima**

   "Pole kaka, huu ndio ulimwengu wetu… ulimwengu unaoendeshwa na sarafu, ndugu. Tumekuwa kama wanyama wa mwitu. N'ambie tofauti i wapi yakhe? Kama wanyama, hatuna tena mipaka ya umri, nasaba au vyeo."

   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Fafanua maana ya kitamathali kwenye kauli iliyopigiwa mstari. (alama 2)
   c) Onyesha jinsi unyama wa msemaji kwenye dondoo ulivyoathiri wengine kwenye jamii. (alama 6)
   d) Kando na msemaji wa dondoo hili, kuna wahusika wengine walioendeleza utovu wa maadili katika jamii. Thibitisha. (alama 8)

**SEHEMU B: TAMTHILIA**

**T. AREGE: *Bembea ya Maisha***

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. Si neno mama! (Kimya.) Hakuna kizuri kijacho kwa urahisi. Mazuri hutoka mbali na wakati mwingine yana hadithi za kutisha.

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)

(c) Fafanua sifa za msemaji. (alama 6)

(d) Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili. (alama 6)

3(a) "Ndiyo ni mgonjwa lakini mume ambaye ni mwanamume kweli hangoji kuelezwa kinafanyika nini."

(i) Bainisha maudhui yanayojitokeza katika dondoo. (alama 1)

(ii) Onyesha jinsi maudhui uliyotaja katika (i) yalivyoshughulikiwa katika tamthilia ya *Bembea ya Maisha*. (alama 9

3(b) Ndoa ni bembea. Jadili kwa kurejelea tamthilia ya ***Bembea ya Maisha***. (alama 10)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI**

**D.M. Lutomia na P. Muthama (Wah.): *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine***

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. **Yussuf Shoka Hamad**: "***Mzimu wa Kipwerere!"***

"Vipi kuhusu usambazaji wa mizigo? Tunahitaji akina mama zaidi maana mzigo ndio kama unavyouona na umejaa humu na hauuzwi kwa wingi! Umelifikiriaje hili?

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Bainisha mbinu **tatu** za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 3)

c) Eleza sifa **sita** za msemaji katika dondoo hili. (alama 6)

d) Suala la dawa za kulevya limejitokeza katika hadithi, "***Mzimu wa Kipwerere***." Thibitisha. (alama 7)

5. (a) "Kwa muda wote tuliokaa pamoja, sikufichua siri yoyote ambayo nilijua". Onyesha siri ambazo msemaji hakufichua katika hadithi, "***Kifo cha Suluhu***". (alama 7)

(b) "Ni wajibu wetu wanawake kutetea maisha yetu na yale ya Watoto wetu." Thibitisha kauli hii kwa kurejelea hadithi, "***Nipe Nafasi."*** (alama 13)

**SEHEMU D: USHAIRI**

**Jibu swali la 6 au 7**

***6. Soma mashairi yafuatayo kisha uyajibu maswali yanayofuata***

**Shairi 1**

**MIMBA ZA MAPEMA**

Zanikosesha amani, hizi mimba za mapema
Hunizushia huzuni, nikakosa kuungama
Ela leo nabaini, munisikilize vyema
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Ni ubaya wa malezi, wakwa baba au mama
Kwa kushindwa uongozi, kuongoza palo pema
Wakawaacha ja mbuzi,ndio haya huja nyuma
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Mwana avaa vibaya, nguo zisizo heshima
Nanyi mwamuangaliya, munashindwa kumsema
Tena munamteteya, haki sawa mwalalama

Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Wazazi haki wandani, wengi wao sio wema
Wajivalia vimini, banati wakitizama
Ndugu hili liacheni, mimba ndio zitakoma
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Au yuwataka pipi, kama ilo na Halima
Nae ajihisi hapi, yuwaonewa huruma
Wamgomea humpi, aenda pewa na Rama
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Mara aja na rafiki, wakiume wakisoma
Kuulizia hutaki, wawacha wakinguruma
Wallahi halikomeki, mimba zitazidi vuma
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Yuwakuaga mtoto, enda kesha kwenye ngoma
Nawe huoni uzito, wampa na darahima
Ela mwisho ni majuto, eleweni wanadama
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Jengine lililo sumu, silifichi nalisema
Na ndio lashika zamu, linaloharibu uma
Mwana kumwachia simu, na shule hajakhitima
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Hata shida za nyumbani, kukosekanapo sima
Mlo ukawa jioni, wali usio na nyama
Hapo tupo hatarini, tujitumeni kwa hima
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

Hizi ni beti a'shari, ndio mwisho kaditama
Nalighaliki shairi, sisemi tena kalima
Ela niloyadhukuri, yatwalieni muhima
Mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi

**Shairi 2**

Hata nijaze dhahabu, lifurike kontena,kisha ifanye kilima
Eti nataka karibu, ya kuwa italingana,alonitendea mama
Takuwa najiadhibu, najisumbua naona,dharau zaniandama
Sitolipa masahibu, na madhila mengi sana,yalompita mama

Hata nijenge benki, kubwa kuzishinda zote,zilojengwa duniani
Pesa nijaze lukuki, kila aina apate,za ndani na za kigeni
Riyale kwake si dhiki, dirham zisikate, na Dola za Marekani
Hazitalipa mikiki, mama yangu aipate, sekunde nimo tumboni
Hata nijenge nyumba, ya ghorofa hamsini, karibu kugusa mbingu
Yenye idadi ya nyumba, alfu u thamanini, milki ya Mama yangu
Awe mwenyewe atamba, nyumbani na sebuleni, kwa sofa ziso mbingu
Na masifa ya kujipamba, si kitu chenye thamani, ja bega la mama yangu

Hata ndege ninunuwe, Miele angani iko, na mama aishi humo
Katu chini isituwe, kugusa chini mwiko, kila kitu kimo
Anapotaka mwenyewe, aone kule aliko, darubini ndani imo
Mwenyewe nikusumbuwe, si sawa na ubeleko, wa mama mwenye makamo

Hata nijenge mabwawa, makubwa ya kwogelea, kwa mama nimeyaweka
Maji moto yanatiwa, na baridi kila saa, aoga anayotaka
Taulo amepangiwa, sabuni za kunukia, kila chini zinatoka
Kote ni kujisumbuwa, sudusi sijafikia, kinyesi changu kunyika

Hata nitunge shairi, niwe mimi nalighani, mama atakapolala
Sauti ile nzuri, kutoa nyoka pangoni, si ya debe yenye ila
Nikawa nalikariri, mama yuko kitandani, chombezo limetawala
Haijawa ni kadiri, na yako yasi mizani, kutaka mimi kulala

Hata nipewe na vyeo, vishindavyo vyeo vyote, maarufu duniani
Na watu wanionao, heshima kwa nipate, nalindwa sionekani
Ulinzi nilionao, saa na dakika zote, vifaru komando ndani
Si sawa na chake cheo,cha mama kwa hali zote,kwake ni kuruti duni

**Maswali**

a) Linganisha na ulinganue muundo wa shairi 1 na shairi 2. ( alama 4)

b) Linganua bahari za shairi 1 na shairi 2. ( alama 2)

c) Kwa kutolea mifano mwafaka,eleza sababu za mshairi kutumia uhuru wake katika shairi 1. ( alama 4)

d) Tambua nafsinenewa katika shairi 1 ( alama 2)

e) Kwa mujibu wa shairi 1, mimba nyingi za mapema,ni ubaya wa malezi. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja tatu. ( alama 3)

f) Andika ubeti wa tatu katika shairi 1 kwa lugha nathari. ( alama 4)

g) Eleza maana ya neno "**banati**" kama lilivyotumika katika shairi 1. ( alama 1)

**AU**

***7. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yanayofuata***

Baada ya mtihani yetu ya mwisho
Tulijikusanya gwarideni kuskia neno la mwisho.

Nyuso zetu zilijawa na furaha
isiyo na kifani,
Hatukujua ni ufunuo wa dunia gizani

Ni miaka tatu sasa bado sijajiunga chuo kikuu
Kisa ni matokeo yangu na wazazi kukosa ka kituu
Ni uchungu sana ila napambania kuipata nafuu

Zile ndoto zangu za kuwa rubani
Niliziwacha mkononi mwa rabani
Wale wanafunzi nilokuwa nao shuleni
Cha ajabu atusemezani kama zamani

Natamani kurudi shuleni
Ila ni tamu izi mapeni
Kwaheri mwalimu
Wewe ni mtu muhimu

**<u>Maswali</u>**

a) Thibitisha kuwa hili ni shairi huru. ( alama 3)

b) Kwa nini nafsineni hajajiunga na chuo kikuu? ( alama 2)

c) Tetea ukweli kuwa kifungu hiki ni shairi. ( alama 4)

d) Tambua kinaya kinachojitokeza katika ubeti wa pili. ( alama 1)

e) Tambua mstari mshata na mstari toshelezi inayojitokeza katika shairi hili. ( alama 2)

g) Eleza maudhui yanayotawala shairi hili. ( alama 2)

h) Eleza aina zozote mbili za urudiaji katika shairi hili. ( alama 2)

i) Tambua idhini moja ya kishairi katika shairi hili. ( alama 2)

j) Eleza vipengele vifuatavyo vya kimtindo kama vilivyotumika katika shairi hili. ( alama 2)

i) taswira

ii) sitiari

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI (Alama 20)**

8. ***Tazama picha ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.***



a) Tambulisha kipera kinachodhihirika hapa juu kwenye picha. (Alama 1)

b) Kipera hiki hupatikana kwenye utanzu gani. (Alama 1)

c) Kwa nini jamii inadhamini kipera hiki? (Alama 5)

d) Utanzu uliotaja kwenye b) unahitaji fanani mwenye wasifu upi kuuwasilisha? (Alama 5)

e) Umepanga kwenda nyanjani kukusanya data ya kipera hiki. Kwa nini njia ya kurekodi kwa video itakuwa bora? (Alama 5)

f) Kupitia kipera kilichotajwa katika a) hapa juu, ni shughuli zipi za kijamii zinaweza kudhihirika kipera kinapowasiliswa? (Alama 3)

**MTIHANI 7**
**SEHEMU YA A: USHAIRI**
**SWALI LA LAZIMA**

**MBELE YA SAFARI**

1. Ilipoanza safari , ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti

2. Njaa ikawa dhabiti ,na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti ,dhila na mingi mikiki
Tukajizatiti

3. Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari,utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari , juhudi iliyobaki
Tukajizatiti

4. Ile ilikuwa ndoto , mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto,sahala ‘mekuwa dhiki
Wagombanio kipato,utashi haukatiki
Nakutabakari

5. Msafara ukasita , kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita , mlima haupandiki
Basi sote ‘kijipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina

6. Tukiwa migongo wazi ,tukainama kwa shaki
Tukawa’chia ukwezi , kialeni wadiriki
Wakapanda bila kazi ,Kuteremsha miliki
Wakaitapia

7. Wakafikia makazi,ya pumbao na ashiki
Huko wakajibirizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

8. Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema , kwa umati halaiki
Imezima nia yote ,kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

a) Eleza safari inayolejelewa katika shairi hili. (al 2)

b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. (al 6)

c) Taja na ueleze bahari mbili za shairi ukizingatia : (al 4)

i. Mizani

ii. Vina

d) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (al 4)

e) Eleza umuhimu wa aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita (al 4)

f) Eleza umbo/ muundo wa shairi hili. (ala 2)

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**
**Timothy Arege**
**BEMBEA YA MAISHA**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. (a.) Soma dondoo lifuatalo kasha ujibu maswali.

**Sara :** Mimi ninashukuru kwa hawa alionipa mungu. Nikitaka zaidi nitakuwa mchache wa shukrani.(kimya) Dina nimesemwa sanana kutukanwa kwa sababu ya hawa wasichana wangu. Wewe unajua yote yaliyosemwa, hadharani na faraghani. Si makanisani, si magengeni. Leo nikiviona vitoto hivi vilivyochekwa na kusimangwa jana, vikijiendeshea mambo yao, ninaridhika moyoni. Hata nikiitwa nitaondoka nikiwa nimeridhika. (Anatokwa na machozi)

Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha.

i.) Changanua maudhui katika dondoo hili (ala 3)

ii.) Bainisha toni katika dondoo hili (ala 2)

iii.) Tambua mbinu tatu za lugha ambazo zimetumiwa katika dondoo hili. (ala 3)

(b.) Jadili jinsi suala la utu linavyoshughulikiwa katika tamthilia ya Bembea Ya Maisha(ala 12).

AU.

3. Kila binadamu hukabiliana na mabadiliko katika maisha yake. Jadili kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. (ala 20)

**SEHEMU YA C: RIWAYA**
C. MOMANYI: **NGUU ZA JADI**
**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** "Lazima amejiunga na kundi la marafiki wenye pesa wanaojaribu kumpotosha."

(a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**

(b) Anayesema maneno haya ni jasiri. Thibitisha kwa hoja tano. **(alama 5)**

(c) Tathmini kwa hoja kumi na moja nafasi ya wenye pesa katika kuendeleza tamaa na ubinafsi katika nchi ya Matuo. **(alama 11)**

AU

**5.** "Mangwasha siku zote hizi ulikuwa unachezeshwa kayamba tu. Ati walisema Osama alikuwa hatari kwa usalama duniani; kuna Osama kuliko huyu?" alijiskia kusema. Alishusha pumzi kwa nguvu akajiuliza kimoyomoyo kwa nini Mungu aliruhusu moto kumtia kwenye shimo la maangamizi na wanawe. Hata hivyo, aliamini kuwa wakati mwingine Mungu huruhusu mabaya

kutokea ili kuwafunza waja. Waaidha, alijua kuwa mashaka yanapomkumba mja, huwa ni funzo pia. Humtayarisha kuyahimili machungu zaidi ulimwenguni ama kumuasa dhidi ya kuabudu maovu. Maovu yanapotendwa na wachache, hata wale wasio na hatia pia hujikuta wamo humo uovuni. Ni mtego wa waliomo na wasiokuwemo.

(a) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 5)**

(b) Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisani aliko Mangwasha katika kukuza Riwaya ya Nguu za Jadi **(alama 5)**

(c) Nchi ya matuo imeshinikizwa na Nguu Za Jadi zinazorudisha nyuma usawa katika jamii. Tathmini kauli hii kwa hoja kumi. **(alama 10)**

## SEHEMU YA D :HADITHI FUPI

## *MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE*

*Jibu swali la 6 au 7*

### WINNIE NYARURI OGENCHE: ‘’SABINA’’

**6.** ‘’Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.’’

a) Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika**. (alama 6)

b) Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. (alama 4)

c) Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii.

(alama 10)

### YUSSUF SHOKA HAMAD: ‘’*Mzimu wa Kipwerere*’’

7.“…Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama.”

(a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (Alama 4)

(b)Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (Alama 4)

(c)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (Alama 2)

(d)Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. (alama 10)

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

***Swali la nane***

8. a) Ulumbi ni nini? (alama 2)

ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii?. ( alama 6)

iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. (alama 6)

b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. ( alama 6)

**MTIHANI 8**

**SEHEMU E: RIWAYA -** Nguu za Jadi – Clara Momany

1.'`Lakini mwishowe niliamua kulivurumisha behewa hilo la upotovu juu ya mwamba.Behewa la maasi na maangamizi ya nafsi iliyoshiba kiburi."

a) Eleza mkutadha wa nukuu. (al 4)
b) Fafanua toni katika dondoo hili. (al 2)
c) Fafanua umuhimu wa mandhari katika nukuu . (al 6)
d) Ukiukaji wa haki za kibinadamu uliendelezwa na uongozi katika nchi ya Matuo. Fafanua (al 8)

**SEHEMU B** : **TAMTHILIA –** Bembea ya Maisha – Timothy Arege

*Fanya swali la 2 au la 3*

2.'Nyota niliyoikamia sana katika ndoto yangu ya utotoni imepita na hiyo jana.Leo ndiyo iliyo mikononi mwetu"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al 4)
b) Fafanua tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondoo. (al 2)
c) Fafanua udhaifu wa msemaji wa maneno haya. (al 4)
d) Eleza jinsi mbinu rejeshi imetumika katika kukuza (i)Maudhui (al 5)
(ii)Wahusika (al 5)

3… wakati mwingine mwindaji huwa mwindwa. Hata kijijini wanaishi watu. Watu hao hawakumbwi na dhiki kiasi hiki. Ya nini kung'ang'ania maisha kana kwamba hayapiti ?Maisha ni mshumaa uso mkesha ! Ukijiachia sana peupe hata upepo unaweza kuuzima kabla ya kulika hadi nchani.

a) Eleza mkutadha wa dondoo (al 4)

b) Fafanua matumizi ya lugha (al 6)

c) Semi hizi zina maana gani ?

i)'Ukijiachia sana peupe hata upepo unaweza kuuzima kabla ya kulika hadi nchani.' (al.2)

ii) Maisha ni mshumaa uso mkesha ! (al 2)

d) Watu hao hawakumbwi na dhiki kiasi hiki.Onyesha dhiki ambazo zimemkumba msemewa (al 6)

**SEHEMU C** : USHAIRI

*Fanya swali la 4 au la 5*

4. .Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali

Upasi ukija, usipokukoma,hukupa tepo
Hupata faraja, utakapochuma, chuma lijapo
Hufunga kharija, kutokuandama, 'kawa hazipo
Watu hukutaja, kusifiwa wema, hujatendapo

Kukifika haja, ukawa u wima, kwa yaliyopo

Upasi ukija, ukiwa u mwema, kwa upatapo
Maovu huchuja, yakabaki tama, mema malipo
Pasingie hoja, zisije lawama, popote ziwapo
Ukapata tija, zilizoegema, kwa kisichopo
Usiwe kufuja, japo ukatuma, na utowapo

Upasi ukija, hujia salama, tata zisipo
Ukipata moja, nyingine zi nyuma, pale ulipo
Hutokea waja, kukupa hishima, waso'kujapo
Sione vioja, ndizoze alama, pato lilipo
Subiri kungoja, na nyingi rehema, zisoshukapo

Upasi ukija, mpaka khatima, ukiwa upo
Hukuvika koja, lililosakama, lisovukapo
Pasiwe pamoja, utakaposema, lisitimupo
Ukawa mmoja, katika azima, usikosepo
Ukafuzu hija, kishapo kiyama, wapata pepo

Upasi ukija, sizivute chama, wala viapo
Zache tafrija, zipazo lawama, zisofanywapo
Usiwe washaja, usiku mzima, kutolalapo
Kufanya miuja, iwapo athama, na majitapo
Mwisho utakuja, uwe kulalama, usitakapo

Hili 'melitaja, hikwambia thuma, usoshikapo
Majuto hupiga, kondo'ye kinyuma, pale wishapo
Wenda kuleleja, mangi ukasema, yasoshikwapo
Hwondoka daraja, zilizosimama, kula kuchapo
Zikabaki huja, macho yakanama, likesha

**MASWALI**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka (al. 1)
b) Bainisha tamathali <u>tatu</u> za usemi zilizotumiwa katika shairi hili (al. 3)
c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo (al 4)
   i) Idadi ya vipande katika mishororo.
   ii) Idadi ya mishororo katika ubeti
   iii) Mpangilio wa vina katika beti.
   iv) Mpangilio wa mizani katika mishororo
d) Huku ukitoa mifano bainisha <u>aina tatu</u> za uhuru wa kishairi aliotumia mshairi (al.3)
e) Andika ubeti wa <u>tatu</u> kwa lugha nathari (al. 4)
f) Fafanua toni ya ushairi hili (al. 1)
g) Bainisha nafsineni katika shairi hili (al. 1)
h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (al. 3)
   i) Tepo

ii) Yakanama
iii) Upasi

## USHAIRI

1. Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyatubu
Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha wenye raha na tabu,ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina,Saidi Ali Rajabu
Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, Ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni  kiwanja wenye dini, wamtiio wahabu
Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu
Mapadiri kanisani, huvihubiri vitabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa na moyo kisebusebu
Tunakaribia kuja, kwa kushindwa kujimudu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu

Na wengine sitotaja, msinambe ninagubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

<u>Maswali</u>

(a)Lipe shairi hili anwani ifaayo. (al. 1)

(b) kwa kutoa mfano, eleza mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika shairi. (al. 2)

(c)Eleza mbinu alizotumia mshairi kutimiza mahitaji ya kiarudhi (al. 2)

(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (al. 4)

(e)Taja na ueleze bahari zozote mbili zilizotumika katika shairi hili. (al. 2)

(f)Eleza umbo la shairi hili. (al. 4)

(g)Eleza toni ya shairi. (al.1)

(h)Fafanua dhamira ya mshairi. (al. 2)

(i)Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (al. 2)

(i) Malofa:

(ii) Udubu:

**<u>SEHEMU D : HADITHI FUPI -</u>** Mapambazuko ya machweo

*Fanya swali la 6 au la 7*

***Kifo cha Suluhu– Dominic Maina***

6.(a)"Kwa muda wote nilioishi nawe,sikukuendea kinyume wala hayakunijia kichwani mawazo yenyewe."

(i)Eleza muktadha wa dondoo hii. (al. 4)

(ii)Tambua sifa ya msemaji inayodhihirika katika dondoo (al. 2)

(iii)Mrejelewa wa kauli hii anafaa kuomba msamaha.Thibitisha (al. 6)

b)Eleza changamoto zinazowakumba mayatima ukirejelea hadithi ya ***Sabina.***(al.8)

***.7.Msiba wa kujitakia – D.W lutomia***

Jioni. Machoka ameketi kitako kochini. Amerejea akiwa amechoka zaidi ya kuchoka. Pilkapilka zake za kutafuta kibarua mchana kutwa zimegonga mwamba. Hajui la kufanya. Matumbo yake yanateta kwa kushindwa kuhimili makali ya njaa. Hajatia chochote kinywani tangu asubuhi. Taswira ya chumba chake ingeweza kumliza kipofu! Anawaza juu ya maisha yake. Maisha ya wasakatonge. Maisha ya wanaojiita 'pangu pakavu'. Maisha ya wapiga kura. Maisha ambayo ni tofauti sana na maisha ya waliopigiwa kura. <u>Maisha kati ya makundi haya mawili yaani mpiga kura na mpigiwa kura, yametengana kama mbingu na ardhi.</u> Machoka anabaki kukodoa macho huku maonevu yakiihukumu nafsi yake. Anasimama pale kama kigingi. Hasongi wala kufurukuta.

a) Changanua mtindo katika fungu hili. (al.7)

b)Thibitisha ukweli wa kauli ambayo imepigigwa mstari. (al. 5)

c) Matatizo ya Wanamatopeni ni mwiba wa kujidunga.Thibitisha (al.8)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

8,Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

*Ndimi Mwambu, dume la ukoo mtukufu wa Mbaitu*

*Ulojipambanua kwa mabingwa*
*Wachezaji hodari wa ngoma na kinanda*
*Ndimi dume liloingia nyanjani*
*Makoo yakatetemeka ya kuduwaa*
*Yakang'ang'ania gozi kusakata nami*
*Ni mimi ! Ni mimi ! Hakuna mwingine wa kupigiwa mfano !*

a) Tambulisha kipera kinachojitokeza katika kifungu hiki (al. 1)

b) Eleza sifa tano bainifu za kipera hiki katika fasihi simulizi. (al.5)

c) Kwa kutoa hoja tano, fafanua manufaa ya kurithisha kipera hiki kwa vizazi vijavyo. (al.5)

d) Umenuia kutumia mbinu ya mahojiano katika kukusanya data.Jadili manufaa manne ya mbinu hii. (al. 4)

e) Jadili matatizo yanayomkumba mtafiti nyanjani. (al. 5)

**MTIHANI 9**

**SEHEMU YA A: TAMTHILIA**

**Timothy M. Arege**.: ***Bembea ya Maisha***

**1. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

Eti hajakosa adabu? Mtu ana ubaguzi kama nini! Ana moyo mgumu kama jiwe. Amejaliwa lakini bahili kama mchanga wa dhahabu. Hajui mali ya bahili huliwa na wadudu?

**(a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

**(b)** Tathmini umuhimu wa maswali balagha katika dondoo hili **(alama2)**

**(c)** Toa mifano ya vipengele vingine viwili vya kimtindo katika dondoo hili **(alama4)**

**(d)** Fafanua nafasi ya anayeitwa bahili katika dondoo hili kwa kuijenga tamthilia ya Bembea ya Masha **(alama10)**

**SEHEMU YA B: RIWAYA: NGUU ZA JADI**

**Clara Momanyi:** ***Nguu za jadi***

**Jibu swali la 2 au la 3**

**2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Hakika shingo hubeba vyombo, lakini moyo hubeba mambo, tena makubwa. Mrima amemkumbatia chui. Hajui chui si rai wa kumbatiwa? Mwishowe atafukarishwa asalie kuguguna vifuu. Hajui dunia ni rangirangile? Acha aendelee kuwasumbua nyuki. Siku akiumwa sawasawa, atarejea hapa hapa akiramba majeraha."

**(a)** Chambua mtindo katika kifungu hiki **(alama4)**

**(b)** Eleza majeraha aliyoyalamba Mrima kabla ya kurejea nyumbani jinsi Mangwasha alivyotabiri **(alama16)**

3. **(a)** Onyesha jinsi nchi ya Matuo inavyojiangamiza yenyewe **(alama8)**

**(b)** Ushirikiano ni jambo muhimu katika kufaulu kwa jamii. Thibitisha ukirejelea wananchi wa Matango **(alama4)**

(**c**)Eleza umuhimu wa mandhari ya mahakamani katika kujenga riwaya Nguu za jadi **(alama8)**

**SEHEMU YA C: USHAIRI**

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Na ujenge nyumba yako, jingi jasho likuoshe,

Ufyeke, upime na uweke nguzo,

Kisha paa uweke na ukandike,

Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mpaka mende usiku,

Nje na ndani ya nyumba watazunguka,

Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,

Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,

Ukae nje nzima siku usubiri,

Wazima wamelala ukirudi usiku,

Vichwa vigumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu

Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,

Na kisha wengine usiku mchana uwasake.

Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

**Maswali**

**(a)** Hili ni shairi la aina gani? **(alama1)**
**(b)** Eleza **muundo** wa shairi hili **(alama3)**
**(c)** Eleza jinsi mshairi alivyoutumia **uhuru** wake katika utunzi wa shairi hili. **(alama4)**
**(d)** Taja mbinu **mbili za lugha** alizotumia mshairi na uzitolee mifano. **(alama4)**
**(e)** Andika **ubeti wa tatu** kwa lugha nathari. **(alama4)**
**(f)** Eleza **ujumbe** wa mshairi. **(alama2)**
**(g)** Toa mfano mmoja wa mshororo **mshata**. **(alama1)**
**(h)** Kichwa gani kinaliafiki shairi hili? **(alama1)**

**5. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Piiiiiip piiip pooop poooop piiip piiip!
Ni mlio wa gari letu
Tayari kwa safari yetu
Safari ya maisha yetu; ya kutukwamua
Kutoka kwenye mikatale ya nyangumi
Nduli! Shetani! Ibilisi! Baradhuli! Punda Mgonjwa.
Yote hayatoshi
Ya kina maelezo kutoa kumhusu.

Ninakumbuka bayana
Kaski nemsi mafungulia bakari huonekana

Ila

Kaski hiyo, nemsi haikuwa

Kaski hiyo, hali mbadala
Kaski hiyo, jinamizi; tanzia
Kaski hiyo, simanzi litanda
Kaski hiyo, ubahaimu lipandwa ardhini, ikamea na kuzaa.

Ukweli ni kwamba,
Wakufunzi, wenye jukumu la kunoa wanagenzi
Mstari wa mbele walijipanga, ubahaimu kutenda.
Maswali, kwa bidii walifungasha
Tafiti wakazamia; kinga na kinga moto ukawaka.
Moto ambao ungekuja kuteketeza kizazi cha usoni.
Majibu, na tochi yalisakwa na kumiminwa akilini mwa watafutiwa
Uadilifu, teke ukapigwa, na kaburi la sahau kuzikwa.
Wakati hupo lakini; hayo kubainika mwiko yalikuwa.

Mwongo mmoja sasa umepita
Hali tenge tahani,
Vyuo vikuu na vya kiufundi
Mahafali wamimina taifani.

Akaaa!

Wahandisi, majumba yawaporomokea
Mawakili, kesi zawaponyoka; kubwa kwa dogo, jepesi kwa gumu
Majaji; haki wanajisi kisa na maana, ughushi
Matabibu na wauguzi; wateja wao jongomeo wapiga foleni
Marubani; ndege zashindana ardhini kutapakaa
Wakufunzi kuelewa wanachofanya, nadra kama wali wa daku
Mahasibu, uadilifu dirishani metokea; hesabu chenga yawapiga.
Maaskofu matumbo mbele wameweka, sadaka wafakamia.
Wanasiasa kusazwa hawajaachwa
Mstari wa mbele katika ufisadi; huku wakiendeleza ukosefu wa ajira.
Maafa, vifusi, mabaki ya ndege na garimoshi,
Utamaushi, msongo wa mawazo, tama na ubinafsi mejaa kila kukicha.

Waama! Waama! Waama!
Hakika! Hakika! Hakika!
Hali tulimo kwa kweli
Ni msiba wa kujitakia
Usokuwa na kilio?
Mwiba wa kujidunga
Usoambiwa pole?
Ni ngumi tulopiga ukutani
Na kuumiza mikonetu?

Gari letu sasa hivi, nanga imeshangóa
Uadilifu kwa hakika, mizizi inataka kukita
Ili jamii kwa kweli, najisi tufagie
Na kufutilia mbali, doa iloshamiri.

Kama si sisi, ni nani atakayemaliza ubahaimu huu?
**Odindo Adinda**: Diwani ya Mchonyoto na Mashairi Mengine
**Maswali:**
**(a)** "Ubahaimu unaorejelewa una ila nyingi." Fafanua kwa mujibu wa shairi hili. **(alama7)**
**(b)** Pambanua umbo la shairi hili. **(alama3)**
**(c)** Tambua toni inayojitokeza kwenye ubeti wa **tano** wa shairi hili. **(alama2)**
**(d)** Onyesha namna mshairi alivyofanikisha mbinu zifuatazo za kimtindo:
**(i)** Aina za usambamba **(alama2)**
**(ii)** Tasfida **(alama2)**
**(e)** Andika ubeti wa mwisho kwa lugha nathari. **(alama4)**

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

### D.W Lutomia na Phibbian Muthama: Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine

**Jibu swali la 6 au la 7**

### MZIMU WA KIPWERERE ~ YUSSUF SHOKA HAMAD

**6. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**
Yaani kile kitendo cha kichaka kile kuitwa mzimu kilikuwa homa ya jiji na shetani tosha
**(a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**
**(b)** Eleza umuhimu wa nyimbo katika kujenga hadithi ya Mzimu wa Kipwrere **(alama4)**
**(c)** Fafanua sababu za kichaka kurejelewa kama shetani **(alama6)**
**(d)** Eleza umuhimu wa mandhari ya Mzimu wa Kipwerere katika kuijenga hadithi hii **(alama6)**

### NIPEE NAFASI ~MZAMANE NHALAPO

**7. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**
"ina maana kwamba hukuomba ruhusa ya kuja huku kutoka kwa mumeo au wakwe zako?
**(a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**
**(b)** Fafanua sifa nne za msemaji wa kauli hii **(alama4)**
**(c)** Fafanua mambo mawili ambayo msemewa alifanya bila kuomba ruhusa **(alama2)**
**(d)** Fafanua umuhimu wa mandhari ya kraal katika kuijenga hadithi hii **(alama4)**
**(e)** Fafanua jinsi msemewa amekabiliana na changamoto zinazomkumba **(alama6)**

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8. Tazama picha ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

**MTIHANI 10**

**SEHEMU YA A: RIWAYA: NGUU ZA JADI**

**Clara Momanyi:** ***Nguu za jadi***

1. **Lazima**

**Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

Chuki iliwavaa Wakule, ikawavisha mashauo na wingi wa tadi. Yote haya yakaelekezwa kwa Waketwa. Majivuno na magigimo hayo yakasambaa hadi kwa viongozi, wakasheheni kiburi. Wakazua uzushi na kuusambaza kwa wenyeji. Kila lililo baya lilielekezwa kwa Waketwa. Hata ukame na njaa viliposhamiri, Waketwa waliandamwa na kumiminiwa lawama. Mvua ya mafuriko iliponyesha na kusomba watu, Waketwa walinyooshewa vidole vya lawama. Hata maradhi sugu ambayo yaliwashinda madaktari, yalidhaniwa kuletwa na Waketwa. Takriban kila lililowashinda watu, lilisemekana chanzo chake ni Waketwa. Ama hakika, chakani mwa simba halali nguruwe.

**Maswali**

**(a)** Chambua mtindo katika kifungu hiki **(alama4)**

**(b)** Eleza sifa za Wakule zinazojitokeza kwenye kifungu hiki **(alama6)**

**(c)** Huku ukirejelea riwaya nzima ya Nguu za jadi, eleza sifa kumi za Waketwa **(alama10)**

**SEHEMU YA B: TAMTHILIA**

**Timothy M. Arege.:** ***Bembea ya Maisha***

**Jibu swali la 2 au la 3**

2. **Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Basi nawe usiyafanye marefu kuliko inavyostahili! Nimesikia.

**(a)** Eleza muktadha wa dondoo **(alama4)**

**(b)** Tambua vipengele vya kimtindo katika dondoo hili **(alama2)**

**(c)** Tambua toni inayojitokeza katika dondoo hili **(alama2)**

**(d)** Tambua sifa za msemaji wa maneno haya inayojitokeza katika dondoo hili **(alama2)**

**(e)** Jadili vyanzo vya mgogoro kwenye ndoa ukirejelea msemaji na msemewa **(alama10)**

**Au**

3. **(a)** Sara amemfaa Asna kwa ushauri si haba kuhusu maisha. Thibitisha dai hili ukirejelea tamthilia ya Bembea ya maisha **(alama10)**

   **(b)** Huku ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha, eleza tofauti ya hali ya maendeleo kati ya hospitali za mjini na hospitali za kijijini **(alama10)**

**SEHEMU YA C: USHAIRI**

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Daima alafajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo Kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani
Nimuonapo huwa anatabasamu

Kama mtu aliye na hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho

Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza
Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimtetea
Nao umande kumbusu miguuni
Na miti yote hujipinda migogo
Kumpapasa, kumtoa matongo
Na yeye kuendelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akichekelea hahahahaha
……. Na mimi kubaki kujiuliza

Kuna siri gani inayomliza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani?
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;
Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbu ya waroho.
Kuna jambo gani linamridhisha?
Kama si kujua ni kutojua
Laity angalijua, laity angalijua

**Maswali:**

**(a)** Eleza hali ya mzungumziwa katika shairi hili **(alama2)**

**(b)** Huku ukitoa mifano, onyesha aina mbili za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili **(alama4)**

**(c)** Fafanua aina tatu za taswira ukirejelea ubeti wa pili **(alama3)**

**(d)** Maswali ya balagha katika shairi hili yanasisitiza maudhui yapi **(alama2)**

**(e)** Kwa kutoa mifano, bainisha vipengele vitatu vya kimtindo katika shairi hili **(alama3)**

**(f)** Eleza toni ya shairi hili **(alama2)**

**(g)** Bainisha nafsineni katika shairi hili **(alama1)**

**(h)** Eleza sura ya shairi hili **(alama3)**

**Au**

**5. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Najitoma ukumbini, niseme yanikerayo,

Yamenichoma rohoni, na kukera wangu moyo
Mizozo ni ya nini, viongozi mlo nayo
Wadau tuunganeni, tuandike katiba mpya

Wakereketwa ungana, mwahitaji muungano,
Mwahitaji kupatana, hili swala nyeti mno,
Washike dau patana, tunangoja lenu neno,
Wadau tuunganeni, tuandike katiba mpya

Wabinafsi na mkome, mizozo tuepusheni,
Uchu wenu uwahame, uongozi kutamani
Pamoja tujenge ngome, haufai ushindani,
Wadau tuunganeni, tuandike katiba mpya

Katiba ilete afu, hiyo kesho kwa vijana
Yaandikwe kwa usanifu, iwafae watu wana,
Njama wazosarifu, wakome yao hiana,
Wadau tuunganeni, tuandike katiba mpya.

Katiba ilinde wote, na iwe kwetu ngao,
Wadogo wakubwa wote, watendewe haki yao,
Iwajali watu wote, pamoja na mali yao,
Wadau tuunganeni, tuandike katiba mpya.

Katiba ilete tiba, kwa mizozo ilo hai
Itwondolee mwiba, tuliojidunga mui
Ikakosekana huba, miongoni mwa jamii
Wadau tuunganeni, tuandike katiba mpya.
Katiba ni tangamano, utengano tupuuze,
Tena ni uelewano, mizozo tusikuze,
Pia ni mshikamano, uhasama tukatize,
Wadau tuunganeni, tuandike katiba mpya

**Maswali:**

**(a)** Kwa maoni yako, kwa nini mtunzi anaonekana kukereza ? **(alama2)**

**(b)** Mtunzi ana maana gani anposema ''katiba ilinde wote, na iwe kwetu ngao'' **(alama2)**

**(c)** Neno ngao limetumikaje hapa? **(alama2)**

**(d)** Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari **(alama3)**

**(e)** Eleza muundo wa shairi hili **(alama4)**

**(f)** Eleza mbinu alizotumia mtunzi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi **(alama4)**

**(g)** Eleza maana ya **(alama3)**

**(i)** Wakereketwa

**(ii)** Mui

**(iii)** Afu

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

**D.W Lutomia na Phibbian Muthama: Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine**

**Jibu swali la 6 au la 7**

**HARUBU YA MAISHA ~ PAUL MUTUA**

**6. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Saa ngapi? Si wajua mtoto angali anakusubiri? Mtoto atalala!"

**(a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

**(b)** Bainisha mbinu mbili za kimtindo katika dondoo **(alama2)**

**(c)** Mwanamke amemdhulumu mwanaume katika jamii. Huku ukurejelea hadithi ya Harubu ya maisha thibitisha hali hii huku ukitoa mifano **(alama6)**

**(d)** Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi ya Harubu ya maisha **(alama8)**

**Au**

**MZIMU WA KIPWERERE! ~ YUSSUF SHOKA HAMAD**

**7. (a) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

Siku iliyofuata, majira ya magharibi pevu, nilifika pale mzimuni. Kama ilivyo ada yangu, nilivaa guo jeupe lililonifunika gubigubi kama maiti. Nikaangalia huku na huko, sikuona mtu. Hapo nikasogea karibu zaidi na ule mzimu. Nilipofika nikauimba ule wimbo wote. Nilipomaliza tu nikajitoma kichakani mle bila hofu wala kimeme…nilichokiona humo, sikuamini macho yangu! Mle ndani ya mzimu mlikuwa na makanda na makasha ya tumbaku, unga wa kilevi na bangi kwenye marobota. Kulikuwa na mapipa ya chang'aa na tembo ya mnazi. Humo pia, mlikuwa na kitanda cha besera kilichotandikwa vizuri. Juu ya kitanda hicho, palitupiwatupiwa asumini na maua ya mlangilangi…

**Maswali**

**(i)** Eleza aina ya taswira katika kifungu hiki. **(alama4)**

**(ii)** Ukirejelea hadithi hii, fafanua jinsi imani katika mambo ya kichawi yamejikita katika jamii **(alama6)**

**AHADI NI DENI ~ RAYYA TIMAMMY**

**(b) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Asalaam aleikhum, wajisikiaje?"

"Waaleikhum salaam. Nyumbani mwaambaje?"

**(i)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

**(ii)** Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo katika kujenga hadithi hii **(alama4)**

**(iii)** Fafanua toni ya mazungumzo katika muktadha huu **(alama2)**

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata**

**Yona:** Leo nitakuwa baba na wewe mama. Mimi sipendi mwajificho.

**Sara:** Sawa basi. (*Anaimba huku akishika masikio yake*) Maskini punda, alinyimwa pembe, akapewa masikio hiyo ndiyo pembe. Pembee pembe, akapewa masikio hiyo ndiyo pembe.

**Yona:** Mamake Neema, nahisi njaa. Napeza kula samaki.

**Sara:** Ala! Umejuaje kuwa ninapika samaki? Baba Neema samaki kutoka Soko Mjinga ni tamu kama asali. Chakula ki tayari. *(Anampa kitawi chenye vipande vya vijiti).* Ndio hii samaki.

**Yona:** *(Akiimba)* Nimeshiba sana. Asante. Nataka kwenda katika shamba la mahindi kukaza seng'enge. *(Anachukua kipande cha mti)* Nimechukua nyundo yangu kwenda kujenga ua. *(Anatumia kijiti hicho kupigia vijiti vingine ardhini huku akisema kuwa anajenga ua).*

**Sara:** Nimechoka sasa. Tuimbe kidogo.

**Wote:** *(Wanaimba huku wakirukaruka)*

Watoto wangu ee
Ee
Mimi mama yenu
Ee
Sina nguvu tena
Ee…

**Maswali**

**(a)** Bainisha utanzu ambapo utungo wa aina hii unapatikana. **(alama1)**

**(b)** Wewe ni mmoja wa wawasilishaji wa utanzu huu wa fasihi simulizi. Eleza sifa unazofaa kuwa nazo. **(alama5)**

**(c)** Eleza sifa zozote nne za kipera hiki. **(alama4)**

**(d)** Eleza shughuli mbili za kiuchumi zinazodhihirika katika utungo huu. **(alama2)**

**(e)** Unanuia kufanya utafiti kuhusu kipera hiki. Eleza changamoto zinazoweza kukukabili unapotekeleza shughuli hiyo. **(alama6)**

**(f)** Eleza udhaifu wa maandishi kama kifaa cha kuhifadhi data. **(alama2)**

**MTIHANI 11**

**SEHEMU A:**

**FASIHI SIMULIZI**

**LAZIMA**

1. **Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Mimi ni Olichilamgwara
Olichilamgwara mwana mbee wa Ojilong
Ojilong wa Marukatipe
Wazee waliposhindwa
Nilivuka misitu milima na mito
Ni mimi jabali
Kipande cha jifya la mama
Nilipokuwa nalisha mifugo
Nilisikia baragumu inalia
Baragumu ya wito
Mifugo wa mtemi wamechukuliwa
Nikachukua mkuki wangu
Wenye kigumba cha mti
Nikachukua upanga wangu
Wenye makali kama mmweso wa radi
Upanga uliopasua pembe za nyati kwa dhoruba moja
Ndipo nilipofyatuka kasi kama umeme
Kufumba kufumbua nikawakaribia nduli
Kusikia vishindi vyangu wakaanza kubabaika
Kuona kifua changu cha manyoya ya kanga wakatetemeka
Macho yangu makali kama kaa la moto yalipowatazama wakakimbia
Mkuki wangu ulipaa kama umeme
Wote wakalala
Mifugo wakanifuata…
Mko wapi vijana
Mmekuwa kama majivu baada ya moto kuzimika?

**Maswali**

a) Tambua kipera ulichokisoma na udhibitishe jibu lako (al. 2)

b) Tambua sifa za jamii zinazosawiriwa katika utungo huu (al. 2)

c) Kwa kutoa mifano bainisha vipengele vine vya kimtindo vilivyotumiwa na nafsinenial. 4)

d) Fafanua sifa nne za kipera hiki (al. 4)

e) Eleza mambo manne ambayo mtendaji wa kipera hiki anaweza kufanya ili kufanikisha utendaji wake. (al. 4)

f) Fafanua mikakati ambayo jamii inaweza kutumia ili kuzuia tungo kama hizi kufifia(al. 4)

**SEHEMU YA B: USHAIRI**

**Jibu swali la 2 au 3**

2. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:**

Binadamu hatosheki, ni kiumbe chenye zani, kweli mja hapendeki,
Kwa kweli haaminiki, hila ameficha ndani, la wazi ni unafiki
Ukweliwe haafiki, njama zake zi moyoni, usimwone ni rafiki
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

Wengine watakuua, wakiona una pesa, hata zikiwa kidogo,

Hizo kwao ni maua, hupupiwa zikatesa, wakazifuata nyago,
Hadi kwenye wao ua, pasipo hata kupesa, wala kukupa kisogo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Pindi kinunua kitu, hafurai Shaitani, bali tajawa chukizo,
Mtu kiwa mtukutu, tanunua mtimani, kwalo lako tekelezo,
Tamko lake 'Subutu', kuondoa tumaini, na kukuulia wazo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Aliye na taraghani, taabu kuishi naye, kazi yake kujidai,
Takusema faraghani, asosema kiwa naye, kupendeza maadui,
Hana faida nyumbani, ni mtu akuchimbaye, mradi usitumai,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka,

Kwa hakika ni balaa, kumkirimu mchawi, aliejaa uchoyo,
Bahati ina hadaa, kukupa alo sadawi, aibatili rohoyo
Mipangoyo kwake jaa, na nia ya ustawi, huwiza vunja kaniyo,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka

Ninacho change killo, ninalia sanasana, kinyesi nimetupiwa,
Ningetoa azimio, lakini uwezo sina, kwa matatizo kuambiwa,
Ama nitumie mbio, fuadi ninanena, akilini nazuiwa,
Mtu kuwa na tamaa, akitaka kiso chake, ni hatari kama nyoka.

**MASWALI:**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)
b) Fafanua mambo **matatu** ambayo nafsineni analalamikia. (alama 3)
c) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 3)
   (i) Idadi ya vipande katika kila mshororo
   (ii) Mpangilio wa vina katika kila ubeti
   (iii) Idadi ya mishororo katika kila ubeti
d) Andika ubeti **wa nne** katika lugha nathari. (alama 4)
e) Bainisha tamathali mbili za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
f) Huku ukitoa mifano, onyesha mbinu mbili alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 2)
g) Andika aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
h) Fafanua muundo wa ubeti **wa tano**. (alama 3)

**3. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Ee mpwa wangu,
Kwetu hakuna muoga,
Uoga ukikufikia, huenda ni wa akina mamayo,
Fahali tilichinja ili uwe mwanamume,
Eewe mpwa wangu, kisu kikali ajabu!
Iwapo utatingisa kichwa,
Uhamie kwa wasiotahiri.

Wanaume wa mbari yetu,
Si waoga wa kisu,
Wao hukatwa kuanzia macheo hadi machweo,

Wewe ndiye wa kwanza,
Iwapo utashindwa,
Wasichana wote,
Watakucheka,
Ubaki msununu,
Simama jiwe liwe juu
Ndege zote ziangamie.

Simu nimeipokea,
Ngariba alilala jikoni,
Visu ametia makali,
Wewe ndiye wangojewa,
Hadharani utasimama,
Macho yote yawe kwako,
Iwapo haustahimili kisu,
Jiuzulu sasa mpwa wangu,
Hakika sasa mpwa wangu,
Hakika tutakusamehe, mwaka kesho unakuja.

Asubuhi ndio hiii,
Mama mtoto aamushwe,
Upweke ni uvundo,
Iwapo utatikisa kichwa.
Iwapo wewe ni mme,
Kabiliana na kisu kikali,
Hakika ni kikali!

Kweli ni kikali!
Wengi wasema ni kikali!
Fika huko uone ukali!
Mbuzi utapata,
Na hata shamba la mahindi,
Simama imara,
Usiende kwa wasiotahiri.

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha (al. 2)
b) Tambua anayeimba na anayeimbiwa shairi hili (al. 2)
c) Toa ithibati kwenye shairi hili kuthibitisha kuwa msimulizi ana taasubi za kiume (al. 2)
d) Taja kwa kutolea mifano mbinu zozote nne za uandishi katika shairi hili (al. 4)
e) Taja shughuli zozote mbili za kiuchumi za jamii inayorejelewa katika shairi hili (al. 2)
f) Eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiuarudhi (al. 4)
g) Msamiati ufuatao umetumika kwa maana gani katika shairi hili? (al. 4)
    i) Mbari
    ii) Msununu
    iii) Ngariba
    iv) Uvundo

**SEHEMU C: TAMTHILIA; BEMBEA YA MAISHA – TIMOTHY M. AREGE**

**Jibu Swali la 4 au 5.**

4. **"Huku ndiko kuvumilia hasa. Tazama faraja ilivyoalika sasa"**

a) Weka dondoo hili katika muktadha. (alama 4)

b) Eleza sifa za msemaji katika dondoo. (alama 6)

c) Onyesha jinsi faraja ilivyoalika katika maisha ya msemewa kwa kurejelea tamthilia ya: Bembea ya Maisha. (alama 10)

**AU**

**5.**

**(a) Changanua mtindo katika kifungu kifuatacho. (alama 10)**

Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (*Kimya*). Siku hazigandiwala jana hairudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (*Kimya*). Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (*Kimya*). Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! *(kama anayeisemea pombe).* Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. *(anapunga mkono.)* Kwaheri pombe. Buriani.

b) Bainisha toni ya dondoo hili. (alama 2)

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kuijenga tamthilia nzima.(alama 8)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

**Jibu swali la 6 au 7**

**6. Harubu ya maisha *Paul Nganga Mutua***

"Naja. Nakamilisha shughuli ndogo hapa kisha nianze safari…"

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (al. 4)

(b) Eleza sifa sita za msemaji wa kauli hii (al. 6)

(c) Jadili changamoto wanazokumbana nazo waajiriwa kwa kurejelea hadithi hii (al. 10)

**7. D.W .LUTOMIA : *Msiba wa kujitakia***

**Wetu ni wetu ,hata akiwa mbaya …ni wetu.hatuna budi kuchagua yeye .lisilobudi hubidi.**

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (**alama 4)**

(b)Fafanua vipengele vya kimtindo katika dondoo hii. (**alama 4**)

(c)Hiari ya maamuzi ya wahusika mbalimbali yamewaletea madhila anuwai.jadili.(**alama 12**)

**SEHEMU YA E: RIWAYA- NGUU ZA JADI**

8. *Hivyo,alitaka kubadili hali hata kama ilimaanisha kukitia kichwa chake kinywani mwa samba. Alitaka kuliokoa jahazi lililokuwa likielekea mwambani kwa kasi. Lakini angeliweza vipi kupambana na utandu wa mahasisi hao?.*

(a) Eleza mbinu nne za mimtindozinazojitokeza katika dondoo (al 4)

(b) Eleza sababu za msemaji kutaka kufaulisha kauli iloyopigiwa mstari (al 10)

(c) Eleza umuhimu wa msemaji katika kujenga ploti ya riwaya hii (al 6)

# MTIHANI 12

## SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI

**1. LAZIMA**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu.Wanyama hawa waliishi baharini. Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba. Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko, matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza. Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka.

Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

**Maswali**

a) Tambua kipera hiki. (alama1)

b) Eleza **sifa tatu za** kipera hiki. (alama3)

c) Eleza **umuhimu wa fomula ya kuanzisha** katika aina hii ya ngano. (alama 3

d) Wewe ni fanani anayewasilisha kipera hiki kwa hadhira.Taja mambo **matatu** ambayo utafanya kuhakikisha **umefanikiwa katika uwasilishaji** wako. (alama 3)

e) Taja **manufaa mawili** ya ngano katika jamii. (alama 2)

f) Kipera hiki **kinaendelea kudidimia** katika jamii yako.Eleza **mbinu tatu utakazozitumia kukidumisha** katika jamii ya leo. (alama3)

g) Eleza maana ya lakabu (al.1)

h) Fafanua sifa za lakabu (al.4)

## SEHEMU B: HADITHI FUPI

**D.M Lutomia na PMuthama(Wah): Mapambazuko ya Machweo na Hadithi nyingine**

**Jibu swali la 2 au 3**

2. "**Fadhila za Punda**"

*"Yu wapi kirukanjia wako? Wajua yuko wapi? Uliacha mbachao kwa msala upitao. Atakutunza nani, maana kwako fadhila za punda ni mashuzi!"*

a) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (alama 4)

b) Tambua **tamathali mbili za usemi** zilizotumika katika dondoo hili. (alama 2)

c) Fafanua **sifa zozote nne za anayeambiwa** maneno haya. (alama 4)

d) Kwa kurejelea hadithi 'Fadhila za Punda' onyesha **jinsi wanawake wanadhulumiwa** na jinsia ya kiume kwa kutoa **mifano kumi** mwafaka kutoka hadithini. (alama10)

**AU**

**3**. a)Suala la umaskini limejitokeza katika hadithi ,"**pupa**." Thibitisha (al.10)

b)Eleza jinsi wahusika mbalimbali wamewajibika katika hadithi "**Harubu ya maisha**" (al.10)

## SEHEMU C: Riwaya

**Clara Momanyi :Nguu za jadi**

**Jibu swali 4 au 5**

**4.** *"Tangu lini mke amuulize mumewe kule aendako au atokako?.....Ama kweli, wanawake wa kisasa wanavunja kila mwiko uliowekwa na wazee."*

a) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (alama4)

b) Bainisha maudhui matatu katika dondoo hili . (alama3)

**c)** Eleza **umuhimu wa msemaji** (alama4)

d) **Changanua mtindo**: (alama10

Mangwasha moyo ulirindima kifuani. Alijua akishikwa pale, kitumbua chake kitakuwa kimeingia mchanga. Hata hivyo , alikamia kujua kilichomo ndani hata hatua hii ingemfikisha pabaya. Barua iliyoletwa na mwanamke Yule lazima ina mambo.

Pengine hata ya kuwahusu wao wenyewe. Bahasha ilikubali, ikamfungulia Mangwasha kile alichotaka kujua. Aliposoma yaliyomo, wahaka ulimvamia ghafla. Mangwasha alihisi kisunzi. Alitoka mbio akaharakisha kwenda kuirudufu ile barua. Aliamini kwamba habari zilizokuwa mle ni muhimu. Zilikuwa ushahidi wa kutosha ambao ungekata ile kesi kwa mpigo. Haikuhitaji mashahidi wale watetezi. Yaliyomo yalimfunulia mikono mbele yake. Yakamkatia hukumu ya kesi iliyokuwa mahakamani .

**AU**

**5.** Jadili nafasi ya mwanamke katika jamii ukirejelea riwaya ‘Nguu za Jadi (al.20)

## SEHEMU D: TAMTHILIA
## T.M Arege:Bembea ya Maisha

**6.** a)Changanua mtindo (al.6)

Yona :(Kwa huzuni)Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua , jana ningeiishi tootofafautitttttofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. (Kimya ) tofauti .Silesi zetu za maisha tungezila zillivyokuja kwa furaha. (kimya) siku hazigandi wala jana haitarudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. (Kimya) Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachilia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. (Kimya ). Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe ! (Kama anayeisemea pombe ). Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuielewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu (Anapunga mkono.)Kwaheri pombe . Buriani.

b)Bainisha aina mbili za taswira katika kifungu hiki (al.4)

c)Tambua toni mbili katika dondoo hili (al.4)

d)Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya

e)Eleza umuhimu wa mandhari ya hospitalini (al.6)

**AU**

**7.** a)Eleza umuhimu wa mhusika Sara katika kujenga vipengele vifuatavyo :

i) Maudhui (al.6)

ii)Ploti (al.4)

b)Fafanua madhara ya ulevi katika tamthilia ya Bembea ya maisha (al.10)

## SEHEMU E: Ushairi

**8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali .**

Jiulize ni kwa nini, uanzapo kuongea
Sana sana makundini, watu hukuondokea
Ndugu ujitathmini, hakika umepotea
Sisi takuombea, mwenye damu ya kunguni!

Mwenye damu ya kunguni , nayo lugha ya ajuza
Wengi hawamtamani, maneno yake yaliza

Yeye ana walakini, dosari kuliko pweza
Kama wewe umefunza, sote hutuona duni!

Sote hutuona duni, na hilo tumezowea
Kazi zetu zote guni, yeye tu amebobea
Umewachokoza mbuni , mateke anapokea
Sisi twakuombea, upae hadi hewani!

Upae hadi hewani, ujione kama bingwa
Mewashinda  gazetini, wandishi kwako wapingwa
Yeye kwetu mpinzani, metia mipaka tingwa
Twakuombea mtafiti,hesabu hadi mizani!

Hesabu adi mizani, utunge kwa kukosoa
U hodari hesabuni, nasi tushakuzoea
We nduli kwa majirani, na waja mekutegea
Kurekebisha hujui, ywatanika peupeni!

Ywatanika peupeni, ywajisifu mjuaji
Amezidi zetu mboni, na amevijunjia mji
Twamwachia waamuzi, kesi wasome majaji
Sisi twakuombea ,sirekebike kidogo!

a) Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi  hili (al.6)
b) Tambua muundo wa shairi hili (al.4)
c) Tambua bahari ya shairi hili kwa kuzingatia mpangilio  wa maneno (al.2)
d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari (al.4)
e) Tambua aina tatu za takriri zinazojitokeza (al.3)
f) Onyesha toni ya shairi hili (al.1)

**MTIHANI 13**
**SEHEMU YA A: USHAIRI**

**1. Lazima**

**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Jiulize ni kwa nini, uanzapo kuongea
Sana sana makundini, watu hukuondokea
Ndugu ujitathmini, hakika umepotea
Sisi twakuombea, mwenye damu ya kunguni!

Mwenye damu ya kunguni, nayo lugha ya ajuza
Wengi hawamtamani, maneno yake yaliza
Yeye ana walakini, dosari kuliko pweza
Kama wewe umefunza, sote hutuona duni!

Sote hutuona duni, na hilo tumezowea
Kazi zetu zote guni, yeye tu amebobea
Umewachokoza mbuni, mateke anapokea
Sisi twakuombea, upae hadi hewani!

Upae hadi hewani, ujione kama bingwa
Mewashinda gazetini, wandishi kwako wapingwa
Yeye kwetu mpinzani, metia mipaka tingwa
Twakuombea mtafiti, hesabu hadi mizani!

Hesabu hadi mizani, utunge kwa kukosoa
U hodari hesabuni, nasi tushakuzoea
We nduli kwa majirani, na waja mekutegea
Kurekebisha hujui, ywatanika peupeni!

Ywatanika peupeni, ywajisifu mjuaji
Amezidi zetu mboni, na amevijunjia mji
Twamwachia waamuzi, kesi wasome majaji
Sisi twakuombea, sirekebike kidogo!

**Maswali**

**(a)** Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili **(alama6)**
**(b)** Tambua miundo wa shairi hili **(alama4)**
**(c)** Tambua bahari ya shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa maneno **(alama2)**
**(d)** Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathani **(alama4)**
**(e)** Tambua aina tatu za takriri zinazojitokeza **(alama3)**
**(f)** Onyesha toni ya shairi hili **(alama1)**

**SEHEMU YA B: RIWAYA: NGUU ZA JADI**
**Clara Momanyi: Nguu za jadi**
**Jibu swali la 2 au la 3**

**2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Kisisi kilimvaa. Sasa alikuwa akihema pumzi za mjusi. Jasho lilimtiririka usoni kama aliyemwagiwa maji. Alijikwaa miguu ovyo. Kiwiliwili chake kikaanza kuyumba kwa hofu na hawafu."

**(a)** Tambua aina za taswira katika dondoo hili **(alama4)**
**(b)** Eleza aina mbili za urudiaji katika dondoo **(alama2)**
**(c)** Eleza na uthibitishe mandhari ambamo dondoo hili limetolewa **(alama2)**
**(d)** Eleza toni ya dondoo hili **(alama2)**
**(e)** Eleza umuhimu wa mandhari ya dondoo hili ukirejelea vipengele vifuatavyo **(alama10)**

**3.** 'Hakuna siri duniani" Thibitisha dai hili ukirejelea riwaya yote ya Nguu za jadi **(alama20)**

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**

**Timothy M. Arege.: Bembea ya Maisha**
**Jibu swali la 4 au la 4**

**4. (a)Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**
Ukilazwa tayari unakuwa umeonja seli. Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema. Amri na vitisho kama askari. Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa. Katika wodi hewa iliyojaa harufu ya dawa imezagaa, vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura. Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.
Changanua mtindo **(alama6)**
**(b)**Asna na Sara ni wahusika wawili wenye mitazamo tofauti kuhusu maisha. Thibitisha **(alama6)**
**(c)**Jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa kwa mujibu wa tamthilia ya Bembea ya maisha **(alama8)**

**5.** Jadili mambo yanayofanikisha ndoa katika tamthilia ya Bembea ya maisha**(alama20)**

**SEHEMU C: HADITHI FUPI**
**D.W Lutomia na Phibbian Muthama: Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine**
**Jibu swali la 6 au la 7**
**AHADI NI DENI ~RAYYA TIMAMMY**

**6. (a) Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**
Maneno hayo yalikuwa kama hirizi aliyoamua kuivaa ili yamwongoze na aliamua hilo akijiambia kimoyomoyo kuwa ingawa babake hayupo tena, atahakikisha ametekeleza wasia wake. Hata huo mwaka haukufika nusu alipata tena habari mbaya. Maskini sasa alikuwa kiate. Mwalimu mkuu alimwita afisini siku hiyo kutoka darasani. Alipokuja yule mesenja kumwita alibabaika sana akijiuliza kuna nini.
Alipofika afisi mwa mwalimu mkuu, mwalimu mkuu aliweza kuusoma wahaka usoni mwake. Akanena naye kwa upole. Mwalimu mkuu siku zote alikuwa moyoni akiomba wasichana wote wangalikuwa kama … kwa bidii na utiifu. Aliona kuwa shule yake ingefanya vyema sana wasichana wote wangekuwa …. Kwa vitendo!
**(i) Changanua mtindo** **(alama6)**
**(ii)** Bainisha mbinu mbili zinazoweza kutumiwa kutambua sifa za mrejelewa katika dondoo **(alama4)**

**NIPE NAFASI ~MZAMANE NHALAPO**
**(b)Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**
"Alijua pia kuwa walijali utamaduni na heshima ya ukoo wa Belo zaidi kuliko hali iliyosababisha uamuzi wa kuja kwao."
**(i)** Thibitisha kuwa ukoo wa Belo ulijali utamaduni wao **(alama8)**
**(ii)** Fafanua namna anayerejelewa alivyoenda kinyume na utamaduni wa ukoo wa Belo ili kujikomboa **(alama2)**

**7. MZIMWI WA KIPWERERE**
**(a)** Eleza ni kwa nini hadithi fupi ***"Mzimwi wa Kipwerere"*** ikaitwa Mzimwi wa Kipwerere **(alama5)**
**(b)** Kwa nini mzimu huu unatisha **(alama5)**
**(c)**Mzimwi wa Kipwerere ulikuwa na siri yake. Thibitisha **(alama10)**

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

**8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata**
Katiechi Analia, Katiechi Analia
Chozi lausaliti undani wake
Undani ambao ameuficha kwa miaka na mikaka
Undani ambao japo anachelea kutangaza asije akaonekana apendaye chongo…
Itabidi kuutoa, kuumwaga mtama

Na kiini cha chozi hili ni kwamba imewadia
Imewadia siku ya siku kanisani kwenda,
Kujitia pingu
Kujitia pingu, pingu za aushi
Je, hakuyataka haya?
Hakupania yapakata kama mwanagenzi,

Apatakavyo malaika mikononi pake?
Kwani basi analovya, kidari kwa maji chumvi?
Shavu lake laini,kuwa kijivu kwa shaka?
Ama ni yano mapenzi yalomlemea?
Mapenzi alopalia kwa miaka na dahari?

Kipi kinokwinamisha,
Kwa tewengu kukubwaga?
Ama ni majukumu kuhofia mwenzetu?
Ni adha za ulezi?
Ni hofu ya kutelekezwa?
Jikoni kuachwa jukumu la kawaida?
Ama ni ugeni kwa nasaba uso asili unokuuguza?
Je, ni mazoea unochelea kuacha?
Ama ni uzito wa nanga ua huba?
Kipi, sema ewe mwenzangu, sema.

Nikahi ni sitara
Usumbufu kuepuka vipanga na mwewe
Ndoa huneemesha na jina kukupa utatukukuka kimwana
Shujaa ukapata wa kukulinda
Miliki ni hakikisho kutoka kwa dume hata katika mauko,
Penzi halali kupata, na warithi kuambulia,
Wa kiume kukufaa
Silie mwana silie,
Watutia simanzi
Waitia ndoa doa, nuksani kukuandamia.

Wavyele mpeni Baraka
Mashangazi mtemeeni mate
Viganjani kumiminia pumzi zenu za neema
Ndoa yake kutengenea
Maumbu acheni
Kulengwa na machozi
Mwamliza zaidi, unyonge kumtia
Baba mtu mshike kondooyo,
Mwongoze kidesturi, madhabahu karibia,
Mkabidhi mkweo, mwenzi wake wa maisha.

Ndiye takayekuwa fahali, simba atakuwa kikaida
Amri tatoa yeye, malkia kufuata,
Utashi wake tatimizwa, ndivyo sheria inenavyo
Bila yeye kutamka mtamba aandamwi na sahibu
Tampenda ewe kinda, tanyenyekea bila kulalama
Penzi talinda wewe, wengine sije paramia
Kukupoka mwamba wako!

**Maswali**

**(a)** Ainisha utungo huu kimaudhui. **(alama1)**
**(b)** Eleza sifa tatu za utungo huu **(alama3)**
**(c)** Chambua mitindo katika utungo huu. **(alama4)**
**(d)** Unanuia kuwasilisha utungo huu jukwani, tathmini vipengele sita ambavyo utavizingatia ili kufanikisha mawasilisho yako. **(alama6)**
**(e)** Eleza manufaa manne ya ndoa kutokana na wimbo huu. **(alama4)**
**(f)** Jamii ina matarajio yepi kuhusu wanandoa? (**alama2)**

**MTIHANI 14**

## SEHEMU YA A: TAMTHILIA

**Timothy M. Arege.: *Bembea ya Maisha***

**1. Lazima**

**Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Zangu. Hizo ni akili za kwetu. Zinatia na kutoa utadhani mashine."

*(a)* Eleza muktadha wa dondoo hili *(alama4)*
*(b)* "Hizo ni akili za kwetu" Thibitisha ukweli wa kauli hii *(alama6)*
*(c)* Ulevi ni tatizo sugu katika jamii. Thibitisha dai hili kwa hoja zozote kumi *(alama10)*

## SEHEMU YA B: RIWAYA: NGUU ZA JADII

**Assumpta K. Matei: *Nguu za jadii***

**Jibu swali la 2 au la 3**

**2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

Waketwa ni watu waliokuwa na bidii ya mchwa kwa jambo walilofanya. Baadhi yao hata walifanikiwa kujenga maduka makubwa makubwa ya jumla, wakanunua magari mengi sana ya usafiri. Katika mitaa mingine ya kifahari kama vile Majuu, waliishi Wakule wengi. Wao ndio waliokuwa wengi serikalini. Lesulia ambaye alikuwa mtemi wa nchi alitoka katika jamii hii. Wakule waliwaonea kijicho sana Waketwa kwa sababu ya umaarufu wao katika shughuli walizofanya. Waketwa ni watu waliokuwa na maarifa ya ujasirimali tangu zamani. Hawakuchagua kazi kama Wakule. Takriban kazi zote zilizodhaniwa duni walizifanya wao bila manung'uniko. Walifanya kazi yoyote ilimradi wapate riziki. Waliokuwa matarishi, waliifanya kazi hiyo kwa bidii na heshima kubwa. Waliokuwa wafagiaji walifagia kwa ustadi mkubwa, mji ukawa safi kabisa. Matopasi walisafisha vyoo kwa uwezo wao wote. Vyoo vya mji wa Taria vikasafika hadi kusifika kote. Waliokuwa maseremala waliranda kwa ufundi wa ajabu. Wakatengeneza samani na vifaa mbalimbali vilivyowavutia hata watalii. Waliofua vyuma, walifua kwa nguvu zao zote wakazalisha vifaa mzomzo.

Katika bidii hii ya Waketwa, hakukukosekana malalamiko kuhusu utawala wa Mtemi Lesulia. Kwa mara ya pili sasa baada ya kushinda kiti cha mtemi wa Matuo, raia wengi walidhani mambo yangebadilika. Ukosefu wa ajira hasa kwa vijana waliohitimu katika taaluma mbalimbali ulikuwa sasa ni mazoea. Baadhi yao hata wakashikilia kwamba elimu haikuwa na thamani kwao. Nchi haikuweza kupanua uchumi ili kuwaajiri wala kuanzisha miradi ya kuwawezesha kujiinua kiuchumi. Aghalabu, ajira chache zilizopatikana zilipewa watu wasiokuwa na juzi wala maarifa. Kazi zilitolewa kwa kujuana, haidhuru hata kama mtu hakuhitimu ipasavyo. Kutokana na mapendeleo katika uajiri, wengi waliishia kufanya kazi ambazo hawajazisomea. Halikuwa jambo la kushangaza kumwona karani akiajiriwa kuwa daktari wa meno na muuguzi akifanya upasuaji hospitalini. Wagonjwa hospitalini wakawa wanafariki kiholela

*(a)* Chambua maudhui katika kifungu hiki *(alama10)*
*(b)* "Lesulia ni kielelezo cha viongozi wabaya wasiofaa katika jamii" Fafanua *(alama10)*

**3. Jadili namna mwandishi alivyoshughulikia suala la ukiukaji wa haki katika kazi yake** *(alama20)*

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibbian Muthama: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine***

**Jibu swali la 4 au la 5**

**Kifo cha suluhu**

**4. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Aliyaacha machozi yamtoke shibe yake kwani asingeweza kujizuia. **<u>Barua ile imfichulia siri si haba</u>**"

Dhibitisha kauli iliyopigiwa mstari *(alama20)*

**5.** Jadili umuhimu wa mandhari ya shule msingi ya Nyamenu katika kuikuza hadithi ya Sabina *(alama20)*

## SEHEMU YA D: USHAIRI

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yanayofuata**

Maendeleo ya umma
Sio vitu maghalani
Kama tele vimesaki
Lakini havishikiki
Ama havikamatiki
Bei juu

Maendeleo ya umma
Sio vitu gulioni
Kuviona madukani
Kuvishika mikononi
Na huku wavitamani
Kama tama ya fisi
Kuvipata ng'o

Maendeleo ya umma
Sio vitu shubakani
Dhiki ni kwa mafakiri
Nafuu kwa mafakiri
Ni wao tu washitiri
Huo ni uistimari
Lo! Warudia

Maendeleo ya umma
Ni vitu kumilikiwa
Na wanyonge kupatiwa
Kwa bei kuzingatiwa
Bila ya kudhulumiwa
Na hata kuhadaiwa
Hiyo ni haki.

Maendeleo ya umma
Dola kudhibiti vitu
Vijapo nchini mwetu
Na kuwauzia watu
Toka nguo na sapatu
Pasibakishiwe na kitu
Huo usawa.

Maendeleo ya umma
Watu kuwa na kauli
Katika zao shughuli
Vikaoni kujadili
Na mwisho kuyakubali
Maamuzi halali
Udikteta la.

Maendeleo ya umma
Watu kuwa waungwana
Vijakazi na watwana
Nchini kuwa hakuna
Wote kuheshimiana
Wazee hata vijana.

**Maswali**

***(a)*** Eleza dhamira ya shairi hili. ***(alama2)***
***(b)*** Baininsha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. ***(alama2)***
***(c)***Eleza umuhimu tatu wa usambamba katika shairi hili. ***(alama2)***
***(d)*** Onyesha jinsi maendeleo ya umma ulivyo kinaya. ***(alama2)***
***(e)***Eleza mambo ambayo mshairi nachukulia kuwa maendelo halisi ya umma. ***(alama4)***
***(f)*** Tambua matumizi ya mstari mishata kwa kutolea mifano. ***(alama2)***
***(g)*** Bainisha nafsi neni katika shairi hili. ***(alama1)***
***(h)*** Fafanua toni ya shairi hili. ***(alama1)***
***(i)*** Andika ubeti wanne kwa lugha nathari. ***(alama4)***

**7. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yanayofuata**

Nakutubu maandiko, yafike hadi mliko,
Musome kwa muwamko, ujumbe uwe zinduko,
Shereheni pa miviko, ama kokote mwendako,
Kuna watu vitokoko,

Huku kwetu tuliko, hatuishi unguliko,
Tuna watu wa vituko, watutiao sumbuko,
Wanao utundu foko, na ufakiri wa mbeko,
Kuna watu vitokoko,

Yaletayo sikitiko, kwao ni mitimbwiriko,
Hata kuvuta tumbako, wakukalia kitako,
Wape nasaha zako, watasema ‘nenda zako’,
Kuna watu vitokoko, hawendi ela kwa mboko.

Ungawambia waliko, kuna moto wa muwako,
Wataangua kicheko, ‘kisema ‘shauri lako’,
Hadi yajiri mauko, nadama na fadhaiko,
Kuna watu vitokoko,

Wananena micharuko, maneno yaso mashiko,
Wakizua gawanyiko, kwayo mawi matamko,
Hawajali sokomoko, zilitazo hangaiko,
Kuna watu vitokoko,

Kumanga huku na huko, kama majibwa koko,
Na kuibua kwenye soko, ndiko wakuhitariko,
Wachapwechapwe viboko, wapate misawijiko,
Kuna watu vitokoko,

Msingoje ongezeko, huno ndo’ wangu mfiko,

Sijanena miropoko, nimenadi badiliko,
Tuwe waso tukutiko, tusipende machafuko,
Kuna watu vitokoko,
(Malenga wa Ghuba, Fred obondo)

**Maswali**

***(a)*** Shairi hili ni la aina gani? ***(alama2)***

***(b)*** Taja sifa tano za kiuarudhi katika shairi hili ***(alama5)***

***(c)*** Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari ***(alama3)***

***(d)*** Eleza maana ya mshororo ufuatao: Hadi yajiri mauko, nadama na fadhaiko, ***(alama2)***

***(e)*** Shairi hili ni la bahari gani? ***(alama3)***

***(f)*** Huku ukitoa mifano mitatu eleza mbinu alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiuarudhi ***(alama3)***

***(g)*** Eleza maana ya maneno yafauatayo kama yalivyotumika katika shairi ***(alama2)***

***(i)*** Mawi

***(ii)*** Misawajiko

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata**.

**Elija maneen**

Inasemekana Elija alikuwa na miujiza sana. Aliweza kupiga kura mpira ukaenda na kupora mbingu siku za wakoloni. Aidha alifungiwa ndani ya sanduku, na walipofungua baadaye wakapata hayumo. Sifa nyingine aliyopewa ni kwamba, alicheza dhidi ya watu waliosifika sana kusakata kandanda, yeye peke yake na kuwasinda wapinzani wake.

Hata hivyo, hayo yanaposimuliwa, elija aliugua na kufa mtu wa kawaida tu, huku akisononeka kwa maumizi nyumbani kwake, maeni Kimilili.

***(a)*** Tambua tanzu na kipera cha fasihi kinachohusishwa na kifungu hiki ***(alama2)***

***(b)*** Huku ukirejelea kifungu hiki, eleza vitambuslishi vine vya kipera ulichotaja ***(alama4)***

***(c)*** Twajifunza nini kutokana na usimulizi huu ***(alama4)***

***(d)*** Nyimbo ni mashairi. Jadili ***(alama4)***

***(e)*** Fafanua hasara za nyimbo katika jamii. ***(alama6)***

**MTIHANI 15**

**SEHEMU YA A: TAMTHILIA**
**Timothy M. Arege.:** ***Bembea ya Maisha***
**1. Lazima**
**Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**
"Machozi yatakosaje kukutoka?"
"Kweli ni kawaida. Wakati mwingine ni huzuni…"
"Wakati mwingine ni ya furaha…"
**(a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**
**(b)** Bembea ya maisha huwa na furaha na huzuni. Tetea kauli hii kwa mujibu wa tamthilia Bembea ya maisha **(alama16)**

## SEHEMU YA B: RIWAYA: NGUU ZA JADII

**Clara Momanyi:** ***Nguu za jadii***
**Jibu swali la 2 au la 3**

**2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Cheiya! Ni Cheiya! Mashauri alitamka akaegesha gari kando ya barabara. Alichomoka kutoka pale mbio akimfuata Cheiya. Hakuamini Cheiya angeweza kutekeleza kitendo cha kikatili jinsi ile. Kumbe alikuwa akimposa nyoka! Mwenyezi Mungu alimnusuru alipoachana naye. Huku nyuma, alifuatwa na Mangwasha na wenzake. Sauna alipaaza sauti na kusema, "Mkamateni! Mkamateni muuaji! Mshikeni!" umayamaya ule ulighafilika. Msichana mrembo kama yule angewezaje kuwa muuaji? Mangwasha hakuamini macho yake. Alisimama kumtazama aliyetaka kumtoa Lonare roho. Watu wakaingia mbioni kumfukuza chiya. Huyu alipomwona Mashauri, alimwonyesha visigino mara moja. Alitoka pale mbio kama mwehu kuelekea barabara kuu ya mji. Aliivuka bila kujali magari yaliyokuwa yakipita kwa kasi.

Umati mkubwa sasa ulimfukuza Cheiya. Mashauri akahisi kovu lililo moyoni lilikwaruza upya. ..

**(a)** Tambua aina nne za taswira kwenye kifungu hiki **(alama4)**
**(b)** Kando na taswira, tambua mbinu nyingine sita za kimtindo **(alama6)**
**(c)** Fafanua maudhui yoyote matano yanayojitokeza katika kifungu **(alama10)**

**3.** "Kijengacho mtu ni utu" ni vipi watu wa Matuo walikaidi msemo huu **(alama20)**

## SEHEMU YA D: USHAIRI

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yanayofuata**
**MWANAMKE**

**1.** Namwona yu shambani,
Na jembe mkononi,
Analima,
Mwanamama,
Mavuno si yake,
Ni ya mume wake.

**2.** Namwona viwandani,
Pia maofisini,

Yu kazini,
Hamkani,
Anabaguliwa,
Na anaonewa.

**3.** Namwona kitandani,
Yu uchi **maungoni.**
Ni mrembo
Kama chombo
Chenye ushawishi,
**Mzima utashi**

**4.** Namwona mkekani,
Yuwamo uzazini,
Apumua, augua,
Kilio cha kite,
Cha mpiga pute,

**5.** Kwani mwanamke,
Ni yeye peke yake,
Haki anakosa
**Kwa kweli ni kosa**
***(Mohammed Seif Khatib)***

**Maswali:**

**(a)** **"**Shairi hili ni la kukatisha tamaa" Fafanua dai hili kwa kutolea mifano minne **(alama4)**

**(b)** Eleza umbo la shairi hili **(alama5)**

**(c)** Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari **(alama4)**

**(d)** Bainisha tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi zima. **(alama3)**

**(e)** Onyesha mifano miwili ya ubabedume inayojitokeza katika shairi hili **(alama2)**

**(f)** Eleza maana ya maneno yafuatayo jinsi yalivyotumiwa katika shairi: **(alama2)**

***(i)*** Mzima utashi
***(ii)*** Maungoni

**5. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yanayofuata**

**SIWE?**

**1.** Siwe ulosema jana, ya kuwa u mashuhuri?
Ya kuwa wajuwa sana, aidha huna kiburi?
Nchini wajulikana, mwanasiasa mahiri,
Bungeni tukuajiri?

**2.** Siwe ulotushawishi, kwa chumvi na kwa sukari,
Na matamu matamshi, ukaziteka suduri,
Ukanena penya moshi, moto ndiyo yakwe siri,
Nawe ndiye hiyo nari?

**3.** Siwe uloji'ta moto, uwakao biribiri,
Kamba 'tatia fukuto, Litakalo leta kheri',

Utatufunua mato, Maisha yawe mazuri,
Tukupe kura waziri?

**4.** Siwe ulosema hayo, na mengi ukabashiri,
Ukamba wafata nyayo, nyayo ziso utiriri,
Tusiwe na wayowayo, wa kufikirifikiri,
Tukuachie ujari?

**5.** Siwe tulokuinua, Mabegani kama mwari,
Tungawa twalemelewa, waume tukajasiri,
Kamba tukikuchaguwa, mema kwetu yatajiri,
Tukakeyi kusubiri?

**6.** Siwe ulotugeuka, kwamba leo u waziri,
Wajiona melimuka, tena ukawa ayari,
Walaghai ukicheka, ukuu umekughuri,
Leo mekuwa hodari?

**7.** Siwe ulojawa raha, za hino yetu sayari,
Ukawa ja vile shaha, hatukupati shauri,
Kutuona ni karaha, wakatiwo twahasiri,
Ushakiya msitari?

**8.** Siwe uliyetughura, ukafunga na safari,
Ukaelekea bara, Kwa wenzio matajiri
Ukatuacha majura, na tama kukithiri,
Kanama Ushaghairi?

**9.** Siwe uliyetuasi, ukenda pasi kwaheri,
Mbona hutwambii nasi, tukajua yetu shari,
Leo una masidisi, husemi na aso gari,
Ndio mezidi jeuri?

**10.** Siwe'lotwaa mgwisho, ukawa wajifakhiri?
Chenye mwanzo kina mwisho, hilo wajuwa dhahiri,
Vyaja kutoka vitisho, kwani hayo sidahari,
Mambo mengimdawari?

**11.** Siwe utakayeiza, mwishowo ukidhihiri,
Siku itayoteleza, kuja kwetu ansari,
Kuja kutubembeleza, kwa nyunga nalo khamri,
Tauya nazo nadhiri.

**Maswali**

**(a)** Mtunzi wa shairi hili ana dhamira gani? **(alama2)**
**(b)** Taja na ueleze bahari tatu za shairi hili? **(alama3)**
**(c)** Onyesha jinsi mtunzi alivyotumia idhini ya kishairi. **(alama3)**
**(d)** Taja na ufafanue tamathali ya usemi iliyotawala katika shairi hili. **(alama2)**
**(e)** Anayerejelewa alibadilika vipi? Eleza. **(alama4)**

**(f)** Andika ubeti wa tisa kwa lugha ya nathari. **(alama4)**
**(g)** Mshairi ana maana gani kwa kusema. **(alama2)**
**(i)** Wakatiwo twahasiri.
**(ii)** Ukaziteka suduri

## SEHEMU C: HADITHI FUPI

**D.W Lutomia na Phibbian Muthama:** ***Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine***
**Jibu swali la 6 au la 7**

### WINNIE NYARURI OGENCHE: *Sabina*

**6. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Akili za masomo huna… zinachangamkia barua na mambo ya wanaume tu. Mamako alikuwa vivyo hivyo na unajua kilichomfika. Kweli mtoto wa nyoka ni nyoka!"

**(a)** Weka dondoo hili katika muktadha wake **(alama4)**
**(b)** Tambua mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili **(alama4)**
**(c)** Onyesha udhaifu wa msemaji katika dondoo hili **(alama6)**
**(d)** Eleza matatizo yanayokumba mtoto wa kike kwa mujibu wa hadithi **(alama6)**

**Au**

### RAYYA TIMAMMY: *Ahadi ni deni*

**7.** Uwajibikaji katika jamii unachangia kuboresha maisha. Fafanua kauli hii kwa kurejelea hadithi 'Ahadi ni Deni" **(alama20)**

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali yanayofuata**.

Hapo zamani za kale, Mungu alituma wajumbe wawili waende duniani. Wajumbe hawa ni Kinyonga na Mjusi. Kwanza alimtuma Kinyonga na kumwagiza akaseme "Wanadamu hamtakufa." Kinyonga alienda kwa mwendo wa kuduwaa, akasimama hapa na pale akila matunda ya miti. Kwa sababu ya hali hii alichelewa sana kufikisha ujumbe kwa binadamu.

Baada ya muda kupita, Mungu alimtuma Mjusi na ujumbe akasema, "Wanadamu sharti kufa." Mjusi alinyanyua mkia akafyatuka pu! Mbio akawahi duniani kabla ya Kinyonga kuwasili. Kwa haraka alitangaza agizo kuu, "Wanadamu sharti kufa! Akarejelea harakaka kwa Mungu. Baada ya muda Kinyonga naye akafika duniani na kutangaza "Wanadamu hamtakufa!" Wadamu wakapinga mara na kusema, "La!" Tayari tumepata ujumbe wa Mjusi, "Wanadamu sharti kufa! Hatuwezi kupokea tena neno lako! Basi kulingana na neno la Mjusi, wanadamu hufa.

Maswali:
**(a)** **(i)** Tambua kipera hiki **(alama1)**
**(ii)** Toa sababu zako **(alama1)**
**(b)** Eleza sifa tatu zinazohusishwa na ngano za fasihi simulizi katika hadithi hii **(alama3)**
**(c)** Andika sifa mbili za Kinyonga **(alama2)**
**(d)** Hadithi hii ina umuhimu gani? **(alama3)**
**(e)** Fafanua mambo yanayochangia kudidimia kwa utani wa kale/zamani kudidimia **(alama5)**

**MTIHANI 16**

**1. SEHEMU A: SWALI LA LAZIMA (ALAMA 20):**

**FASIHI SIMULIZI**

**Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali**

Hapo zamani za kale, Nyani na Mamba walikuwa marafiki wa kufa kuzikana. Watoto wao walipendana na kufaana kama ndugu wa toka nitoke. Familia ya Mamba aliishi mtoni nayo ya Nyani aliishi katika msitu uliokuwa maili thelathini kutoka mtoni. Kila mara marafiki hawa walitembeleana na kusaidiana kwa hali na mali. Kwa vile Mamba alikuwa mvuvi msahuhuri, aliweza kumwauni Nyani na aila yake kwa samaki wa aina mbalimbali. Nyani naye alimpelekea Mamba matunda na nafaka kutoka shambani mwake.

Urafiki wao ulikita mizizi na kunawiri Zaidi wakati Mamba alipokuja kwa Nyani kumposea mwanawe binti. Ukwe uliutilia viungo uhusiano wa Nyani na Mamba wakawa wanagandana kama kupe na mkia wa Ng'ombe. Wakatenda mengi pamoja. Wakazungumza ya kupwa na ya kujaa. Hakuna hata mmoja wao aliyeutilia shaka uaminifu wa mwenzake. Wake zao nao walifuata kaida ya maji kufuata mkondo. Walikuwa masahibu wa chanda na pete.

Msimu mmoja wa mapukutiko ulishuhudia mabadiliko ya kudumu katika maisha ya Nyani na Mamba. Wakati huo, bahari ilichafuka si haba. Kazi ya Mamba ya uvuvi ikaanza kukabiliwa na majabali ya kila aina. Kila mara Mamba alipokwenda uvuvini, alirudi akichekelewa na nyavu zake. Hakuambulia chochote. Njaa ilianza kubisha hodi katika familia ya Mamba. Hali hii ilitishia kuutia ufa urafiki kati ya Mamba na Nyani. Mamba alivamiwa na pepo ambaye hata yeye alishindwa kumfahamu. Kila mara alipomwona. Nyani au watoto wake alitamani kumdakia na kumla mzima mzima. Kadiri aalivyojaribu kujiasa dhidi ya fikira hii mbovu ndivyo moyo wake ulivyoendelea kumshauri, "Una njaa bwana, familia yako itaangamia. Je huoni rafiki yako na familia yake wanaweza kuwa kitoweo? Utaendelea kula wishwa hadi lini? Mbona huyo Nyani ambaye anajiita rafiki yako sasa amekata guu humu? Mbona haji tena kukutazama? Hata karafuu alizokuwa akikuletea ameacha kuleta. "Mamba akaanza kumshuku rafiki yake na akasadiki kuwa Nyani alikuwa mla naye tu.

Usiku mmoja baada ya kula mate na kujilaza kitandani mwake akihesabu nyota, wazo lilimjia. Alikata shauri kumlaghai rafiki yake wa miaka mingi ilia pate kujiokoa yeye na familia yake kutoka katika kinamasi cha njaa. Asubuhi yake alikwenda kwa Nyani akiwa amejinamia kwa jitimai. Alisema, "Rafiki yangu, jana tulipoagana nilipata tanzia. Mjumbe kutoka kijijini aliniarifu kuwa baba yangu ni mgonjwa mahututi. Alisema kwamba baba ananitaka nyumbani upesi," Habari hizi zilimtia Nyani majonzi makuu. Alimwahidi Mamba kwamba wangeandamana pamoja. Kwa vile Nyani hangeweza kutembea majini, ilibidi abebwe na Mamba. Alipatwa na kichefuchefu na manyezi kila alipotazama bahari iliyojitandaza mbele yao kwa mbwembwe. Hata hivyo, Mamba alimhakikishia kuwa wangefika salama. Naye kwa Imani iliyotokana na urafiki na mazoea ya miaka mingi, alitulia.

Safari ilikuwa ndefu na yenye machovu yaliyomfanya Nyani kulala mgongoni mwa Mamba. Walipofika kwenye vina vya maji, Mamba aliamua kumpasulia mbarika Nyani. "Rafiki yangu, nimekuwa nikidhani wewe ni rafiki wa dhati, kumbe uzuri wako wa mkakasi? Mimi na wanangu tumetafunwa na njaa kwa miezi kadha sasa huku maghala yako yakishiba na kutapika chakula. Hujadiriki hata siku moja kuja kujua kama nimepata hata senti moja ya kusagia mkunguni. Jana usiku nilipokuwa nikiwazia hali yangu, nilioteshwa katika ndoto kwamba kama ningepata moyo wako na kuula, basi hali ya uhitaji ingeniishia. Moyo wangu unaniuma sana kukufanyia tendo hili, hata hivyo lisilo budi hutendwa."

Nyani alipigwa na butwaa nusura moyo wenyewe ujikabidhi kwa Mamba. Hata hivyo, akili yake nyepesi ilifanya kazi. Alimwambia Mamba,"Ndugu yangu, pole sana ikiwa umekuwa unadhani sikujali. Kwa kweli, hata ungeniomba moyo wangu siku hizo ningekupa tu. Unajua tena sisi Nyani, Tumbili na Kima tuna mioyo mingi. Hata hivyo, nasikitika kuwa Mungu alituambia kuwa daima mioyo yetu itakaa mitini. Basi ndugu mpenzi, badala ya kuendelea na safari hii, turudi pale mtini nikupe moyo wangu pamoja na mitatu ya wanangu kusudi uwalishe wanao na mkeo."

Mamba akaingia mtegoni. Wakarudi hadi ufuoni. Kwa vile Mamba hakuweza kutoka majini, alibaki ufuoni akimngojea rafiki yake amletee mioyo.

*For marking schemes visit our web page www.goldlitekcserevision.co.ke or contact 0724351706 for more*

Mamba alitunga macho yake kwenye ujia alioufuata Nyani akiomba pasitokee lolote la kumchelewesha Nyani. Matumbo yalimnguruma kwa njaa. Roho ikampapa kwa tumaini. Alingoja, akongoja, akangoja... wiki, mwezi, mwaka... Nyani hakurudi. Mamba akajua amepwaguliwa na Nyani. Akaapa kumtafuta kwa udi na ambari. Huo ukawa mwisho wa urafiki kati ya Nyani na Mamba. ***Hadithi yangu inaishia hapo.***

**Maswali**

a) Tambua kipera cha utungo huu. Thibitisha. (alama 2)

b) Tambua mbinu **sita** kimtindo alizotumia mtambaji wa utungo huu. (alama 6)

c) Umepewa jukumu la kutamba ngano hii. Fafanua mambo **matano** muhimu utakayozingatia ili kufanikisha uwasilishaji wako. (alama 5)

d) Fafanua umuhimu wa ngano hii katika jamii. (alama 3)

e) Unapanga kufanyia utafiti nyanjani kipera hiki kwa njia mahojiano. Eleza changamoto zozote nne unazoweza kukumbana nazo katika utafiti wako. (alama 4)

## SEHEMU B. TAMTHILIA

### T. Arege: Bembea ya Maisha

**Jibu swali la 2 au la 3**

*2. __Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:__*

**"Unayafanya makubwa bure mwenzangu. Unafahamu vizuri kuwa hiyo si hulka yangu. Sasa mimi nina haja gani kuuvunja mji?"**

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b)Bainisha toni ya msemaji (alama2)

(c)Msemaji amepitia dhiki mbalimbali katika jamii yake, Tambua dhiki alizopitia (alama4**)**

(d)Onyesha namna maudhui ya mgogoro yanavyojitokeza katika tamthilia nzima (alama10)

**Au**

3. Utafanya nini mwenzangu? Dunia ikijua anakusaidia jikoni itasema unashusha hadhi yake na kwa mizani ya jamii utakuwa unajivulia nguo.

(a)Bainisha swala linalodokezwa katika kauli hii . (alama 2)

(b)Eleza jinsi msemewa alivyojenga tamthilia (alama4) (c) Kwa kurejelea mifano **saba** ,eleza jinsi swala hili limejitokeza katika tamthilia kwa hii husika (alama 14)

## SEHEMU YA C: RIWAYA

**Clara Momanyi.:** ***Nguu za Jadii***

**Jibu swali la 4 au la 5**

***4.Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:***

"Wapendwa, tunafahamu ya kwamba kiongozi si mwanasiasa pekee. **__Kila mmoja wetu ni kiongozi kwa namna yake ya kipekee.__** Msiiamini sana lugha ya kisiasa kwa sababu mara nyingi lugha hii hupindua usemi. Huwezi kupindua uongo ukawa ukweli na ukweli ukawa uongo. Kamwe uongo hauongoi"

**(a)** Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

**(b)** Tambua mbinu iliyotumika katika dondoo hili **(alama2)**

**(c)** Eleza umuhimu wa msemaji **(alama6)**

**(d)** Tathmini ukweli wa maneno yaliyopigiwa mstari **(alama8)**

5. Riwaya Nguu za jadii inahimiza ujenzi wa jamii mpya. Jadili **(alama20)**

## SEHEMU YA D

### Hadithi Fupi – Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine – Dw Lutomia

***Jibu swali la 6 au la 7***

### KIFO CHA SULUHU

6. Mume wangu, hebu zivute fikra zako miaka kumi na mitano iliyopita tulipoingia katika mkataba wa ndoa. Kwa nini unataka kujitia hamnazo kuhusu ahadi ulizozitoa? Umesahau namna tulivyohangaika, tukachekwa na watu, tukakosa hata marafiki na hatimaye tukabandikwa majina ya ajabu? Umesahau, mume wangu? Umesahau namna kazi yako ya kuuza makaa ilivyofika hatima ya ghafla baada ya serikali kupiga marufuku ukataji wa miti katika eneo la Dafrao? Naomba ukumbuke. Ninaamini huenda umesahau! Ama cheo chako cha ubunge ulichokipata kwa mbinu nizijuazo mimi kimekulevya na kukufanya uisahau familia yako?

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 5)

b) Fafanua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili. (alama 6)

c) Tambua toni iliyotumika katika dondoo hili. (alama 2)

d) Fafanua umuhimu wa ujumbe alitoa mnenaji wa maneno haya. Tumia hoja nane. (alama 8)

**A**

**7.“Wewe mke sampuli gani usiyetaka kumuunga mkono mmeo?”** Kwa kurejelea hadithi hii na nyingine zifuatazo, jadili **adha** anazopata mnenewa pamoja na wahusika wa jinsia yake. *Hadithi ya Nipe nafasi*, *Ahadi ni deni na* *<u>Fadhila za punda</u>*

**8.SEHEMU YA E;USHAIRI**

**<u>UTU NI NINI?</u>**
Utu na ubinadamu, ni kama yai na kuku
Utu ni ile nidhamu, *mola aliyokhuluku*,
Ubinadamu ni damu, ya utu wa kila siku,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Ye yote mwanaadamu, ana asili ya utu,
Ya’ni kwenye yake damu, hakikosi hiki kitu,
Utu sifa maalumu, ya mtu kuitwa mtu,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu ni kiumbe hai, tunacho chaonekana
Utu kamwe haudai, tabia ya kujivuna,
Utu ni ule uhai, ushikao uungwana,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu huweza pimika, kwa hisia ya akili,

Huweza kuhifadhika, kulingana na *fadhili*,
*Utu huweza pendeka, palipo na maadili*
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Utu unayo aibu, na *tabia ya muhali*,
Utu huenda na jibu, la Imani na ukweli,
Utu huiona tabu, tabia ya ujahili,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Filosofia ya utu, inapinga ubinafsi,
Utu hautaki kitu, cha upeke wa nafsi,
Utu hauna kiatu, cheupe au cheusi,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Utu wa kweli kwa *mja*, ni wenzake kuwajali,
Utu huiona haja, ya kujua watu hali,
Utu ni kuwa pamoja, kwenye shida mbalimbali,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake.

Utu ni ubinaadamu, udugu na wenzi wako,
Utu wote waheshimu, kwa nidhamu na kicheko,
Utu ona mwanadamu, sijitenge peke yako,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

Ingawaje tu dhaifu, katika ubinafsi,
Utu kweli nausifu, ubinadamu halisi,
Utu ni sifa tukufu, iletayo kila *nemsi*,
Utu wowote wa mtu, ni kuwajali wenzake

MASWALI

a) Tambua **aina** ya shairi hii kwa kutolea idhibati. (alama 2)

b) Kwa hoja nne fafanua ujumbe wa mshairi. Taja sifa tano za mtu mwenye utu kulingana na shairi.(alama 5)

c) Tambua mbinu mbili za kimtindo zilizotumiwa na mshairi. (alama 2)

d) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 3)

e)Tambua nafsi neni katika shairi. (alama 1)

***i)*** Tambua mbinu tatu alizotumia mshairi ili kukidhi mahitaji ya kishairi. (alama 3)

g) Andika ubeti wa saba kwa lugha nathari. (alama 4)

**MTIHANI 17**

## SEHEMU YA A : BEMBEA YA MAISHA

**LAZIMA**

1.``…gari likisha kwenda kwa gia Fulani kuhitaji ibadilishwe nyingine. Huwezi kurudia gia ile ile. Gari Hupiga resi tu.

a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
b) Tambua mbinu za lugha (alama 4)
c) Fafanua sifa nne za msemewa (alama 4)
d) Jadili mbinu ishi ambazo wahusika mbalimbali wametumia kukabiliana na changamoto walizokumbana nazo katika tamthili ya Bembea ya Maisha. (alama 8)

## SEHEMU YA B: RIWAYA( NGUU ZA JADI)

**Jibu swali la 2 au 3**

2 a) … "Je, akipuuza nitakalomwambia, hataniona mie ni mwongo tu?"
i) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
ii) Eleza umuhimu wa mrejelewa (alama 4)
iii) Bainisha mbinu zozote mbili za uandishi kwenye dondoo hili (alama 2)
b) Riwaya 'Nguu za Jadi ni kiakisi cha hali halisi katika jamii nyingi za kiafrika, Jadili (alama 10)

3 a) Eleza Umuhimu wa Mandhari ya afisini mwa chifu Mshabaha**. (alama 10)**
b) "Mume huyo ambaye ni mfano wa mume kamwachia madhila yasiyopimika." (alama 10)

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

Jibu swali la 4 au 5

**4** a) Jadili changamoto zinazoikumba asasi ya ndoa kwa kurejelea hadithi zifuatazo. (alama 10)
(i) Fadhila za punda.
(ii) Kila mchezea wembe.

b) Onyesha changamoto zinazowakumba watoto wa kike kwa kurejelea hadithi zifuatazo (alama 10)
i. Nilitamani.
ii. (Sabina.

**5.** "…Alinipigia simu kunijulia hali. Sikutaka kumpa shida zangu. Nikamhakikishia kuwa kila kitu shwari… niliona kama mungu amemtuma malaika wake."

a) fafanua umuhimu wa anayerejelewa katika dondoo hili (alama 6)
b) ni yapi yanayofanya msimulizi kumwona mrejelewa kama malaika.(alama 4)
c) "tama mbele mauti nyuma". Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi hii.(alama 10)

## SEHEMU YA D : USHAIRI

**Jibu swali la 6 au 7**

6. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali

Maisha yako yalivyo, hakuna ayajuaye,
Leo yatakuwa ovyo, kesho uyashangiliye,
Hivyo ndivyo yaendavyo, mjuzi Mola pekeye,
Maisha sawa na fumbe.

Subira kitu muhimu, kwa nguvu ishikiliye,
udumu nayo dawamu, wala usiiachiye,
Huku wamwomba karimu, mambo akufunguliye,
Maisha sawa na fumbo.

Leo ukiwa na shida, basi uivumiliye,
Huenda kesho labda, upate ufurahiye,
Kila kitu kina muda, kianze na kiishiye,
Maisha sawa na fumbo.

Katu usije kufuru, ,abaya ujikiriye,
Ukatoka kwenye nuru, gizani ukaingiye,
Utajinyima uhuru, wasiwasi ujitiye,
Maisha sawa na fumbo,

Yupo alokuwa duni, maisha uyachokiye,
Ukimtia machoni, utatamani uliye,
Leo apewa thamani, akipta huyu ndiye,
Maisha sawa na fumbo.

Nausitisha waadhi, naomba uzingatiye,
Niliyosema baadhi, ila isipuuziye,
Nikikosa kumradhi, basi nisamehe miye,
Maisha sawa na fumbo.

a) Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili (alama 1)
(b) Bainisha bahari za shairi hili kwa katumia vigezo vifuatavyo (alama 2)
(i) Vina
(ii) Kibwagizo
c) Jadili muundo wa shairi hili (alama 4)
d) Kwa kutolea mifano, onyesha aina mbili za urudiaji katika shairi hili (alama 2)
e) Eleza toni ya mtunzi wa shairi hili (alam 2)
f) Taja nafsi neni kwenye shairi (alama 1)
(g) Andika ubeti wa tatu katika lugha tutumbi (alama 4)
h) Onyesha namna ambavyo ametumia leseni ya kishairi (alama 2)
h) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa:- (alama 2)
(i) Kufuru
(ii) Waadhi.

**7 Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yanayofuata:**

**RISALA ZA AMANI**

Tungo peleka risala, sala kwa Mwenyezi Mungu
Na watu kila kabila, bila kujali mnengu
Waambie ukabila, kabila lao na langu
Si neno pamwe na mila, ila sote walimwengu

Sote ni taifa hili, hili watie fahamu
Mtu ni mwenye amali, mali bora ni nidhamu
Ndio inostahili, ila amani idumu
Yatupasa kuhimili, mili tusimwage damu

Wa bara na wa mvita, vita tusende tumika
Tutarudia kujuta, uta utapofyatuka
Kutujengea matata, tata zisipotatuka
Huja huku kuzorota, ota la kuthaminika

Mijini na mashinani, nani hufuzu kwa vita ?
Taifa lenye amani, mani hupata kuota
Pakawa kutamakani, kani pasipo kuteta
Pakiwa matumaini, ini huota mafuta

**SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI**

8. Ukiona neno usiseme neno, ukisema neno utapatwa na neno.
(a) Bainisha Utanzu na Kipera cha utungo huu. ( alama 2)
(ii) Toa idhibati ya jibu la (a)) (i) . (alama 1)
(b) Kwa kutolea mfano eleza sifa zozote nne za Kipera hiki (alama 5)
(c) Eleza dhima ya Kipera hiki katika jamii. (alama 5)
(d) Fanani wa kazi ya Sanaa huwa na nafasi kubwa sana katika jamii. Eleza. (alama 7)

**MTIHANI 18**

**A. BEMBEA YA MAISHA – Timothy Arege - LAZIMA**

**1. Ninavaa vizuri na kujivisha tabasamu ila ndani viraka na huzuni tele. Maana huwezi kushitakia hali yako kwa kila mja. Kama kitabu huyaficha yaliyomo seuze binadamu?**

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Bainisha mbinu mbili za kitamathali katika dondoo hili (alama 4)
(c) Fafanua hisia za kifungu hiki. (alama 2)
(d) Pana uhusiano mkubwa baina ya sifa za wahusika na maudhui katika kazi ya fasihi. Huku ukimrejelea mhusika Bunju, onyesha ukweli wa madai haya kwa mifano mwafaka. (alama 10)

**B. RIWAYA YA NGUU ZA JADI– Clara M**

2. **I say, wajua nimewaona wapi leo? Katika hoteli ya Saturn. Wameshikana mikono kwa njia ambayo imenifanya nikutafute.**

(a) Eleza sifa nne za mnenaji wa kauli hii. (alama 4)
(b) Jadili umuhimu wa msemewa wa kauli hii. (alama 4)
(c) Wanaosemekana kushikana mikono wanaendeleza uozo katika jamii. Thibitisha. (alama 10)
(d) Bainisha mtindo katika dondoo. (alama 2)

Au

3. **Mandhari ya afisi ya Chifu Mshabaha ni muhimu sana katika riwaya hii ya Nguu za Jadi. Onyesha namna mandhari hayo yanajenga;**
(a) Maudhui mbalimbali (alama 10)
(b) Migogoro ya aina mbalimbali. (alama 10)

**C. HADITHI FUPI D.W. Lutomia na P. Muthama(Wah):** *Mapambazuko ya Machweo na hadithi zingine.*

**4. Kimyakimya analikariri:**

**Mteule nimechoka, kila siku kusikiya**
**Vyereje nchi hakika, visanga kupindukiya,**
**Tunazidi filisika, walaji kijijaziya,**
**Msiba kujitakia, kweli hauna kilio.**

(a) Huu ni ubeti wa shairi katika hadithi ya 'Msiba wa kujitakia.' Eleza sababu ya mwandishi kutumia mbinu hii katika usimulizi wake. (alama 6)
(b) Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari katika dondoo. (alama 8)
(c) Bainisha maudhui mbalimbali ya nayojitokeza katika kifungu hiki. (alama 6)

Au



*Kwa majibu tembelea tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke ama piga nambari kwa 0724351706*

**5. <u>Dadii, nashikia</u> njaa …**

**Pole, mama. Nimefika…**

(a) Eleza umuhimu wa msemaji wa kauli iliyopigwa mstari. (alama 4)
(b) Fafanua sababu za mwandishi kutumia maneno yaliyopigwa mstari. (alama 4)
(c) Msemaji wa kauli ya pili ni mwenye matumaini. Thibitisha kwa hoja nne. (alama 4)
(d) Jadili njia au mbinu mbalimbali ambazo wahusika wanatumia katika hadithi ya Harubu ya Maisha kukabiliana na changamoto zinazowakumba. (alama 8)

**D. USHAIRI**

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.**

Naamba kazi ni kazi, vyovyote vile iwavyo
Madamu si <u>ubazazi</u>, kwa mwanaadamu ndivyo
Kushona na upagazi, pia vile vyenginevyo
Kazi ni kitu azizi, wala vyenginevyo sivyo
Mtu hachagui kazi.

Mtu hadharau kazi, ile ahisiyo duni
Ayazuie machozi, walilia jambo gani
Ukulima na ukwezi, na uvuvi baharini
Hizi nazo njema kazi, yafaa uzibaini
Mtu hachagui kazi

Si laiki kubughudhi, hakuna iliyo duni
Hayo makubwa maradhi, na tena uhayawani
Kazi zote zina hadhi, hivyo tusibagueni
Inafaa tuziridhi, tuzitende kwa yakini
Mtu hachagui kazi.

Ni wajibu kuipenda, na kuikiri moyoni
Na kwa dhati kuitenda, kwa juhudi na makini
Matatizo huyashinda, na uvivu kuuhuni
Hapo mtu atashinda, na magumu kumhuni
Mtu hachagui kazi

**<u>MASWALI</u>**

(a) Eleza ujumbe wa shairi hili. (alama 4)
(b) Kwa mifano mwafaka fafanua bahari katika shairi hili (alama 4)
(c) Mtunzi alikuwa na nia gani katika shairi hili? Taja mbili kuu. (alama 2)
(d) Andika ubeti wa pili wa shairi hili katika lugha nathari. (alama 4)
(e) Eleza muundo wa shairi. (alama 4)
(f) Bainisha uhuru wowote wa kishairi katika shairi hili. (alama 2)

**7. Soma shairi hili kisha ujibu maswali.**

Jicho, tavumiliaje, kwa hayo uyaonayo?
Kicho, utasubirije, maonevu yapitayo
Kwacho, lijalo na lije, nimechoka vumiliyo



*Kwa majibu tembelea tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke ama piga nambari kwa 0724351706*

Naandika!

Moyo, unao timbuko, maudhi tuyasikiayo
Nayo, visa na mauko, wanyonge wayakutayo
Kwayo, sina zuiliko, natoa niyahisiyo
Naandika!

Hawa, wanotulimiya, dhiki wavumiliayo
Hawa, mamiya mamiya, na mali wazalishayo
Hawa, ndo wanaoumiya, na maafa wakutayo
Naandika!

Hawa, sioni wengine, kwao liko angamiyo
Hawa, uwapa unene, watukufu wenye nayo
Hawa, bado ni wavune, kwa shida waikutayo
Naandika!

Bado, wawapo mabwana, wenye pupa na kamiyo
Bado, tafauti sana, kwa pato na mengineyo
Bado, tuling'owe shina, ulaji pia na choyo
Naandika!

**Maswali**

(a) Fafanua ujumbe wa shairi hili. (alama 5)
(b) Onyesha mifano miwili ya uhuru wa kishairi katika shairi. (alama 2)
(c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 4)
(d) Tambulisha kwa mifano mbinu zozote mbili za sanaa katika shairi. (alama 4)
(e) Eleza bahari za shairi hili kwa misingi ya mishororo na vipande. (alama 3)
(f) Fafanua toni inayojitokeza katika ubeti wa mwisho. (alama 2)

## E. FASIHI SIMULIZI

**8. Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali**

Mjomba ananiambia,
Umewadia wakati ,
Wakuondoka utotoni
Kwa sababu msitu na kisu
vinaitana

kando ya zizi lake,
'yule ng'ombe ni wako,
' ni mahari ya baadaye …
Kando ya ghala asema
'ile gunia; ya mahindi na mtama,
Ni chakula
cha wageni wako,



*Kwa majibu tembelea tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke ama piga nambari kwa 0724351706*

Lakini

Mjomba anaenndelea,
'Ukilia,
utakuwa kilizi..
utakuwa aibu…
utakosa chochote,

mahari , gharama yako,
wageni, gharama yako,
mimi si mjombako
kwaheri'

(a) Eleza aina ya wimbo huu kwa kutoa sababu. (alama 2)
(b) Kwa kurejelea kifungu hiki, bainisha sifa za kipera ulichokitambua. (alama 4)
(c) Bainisha sababu tatu za kutumia mbinu ya kushiriki wakati wa kutafiti kipera hiki. (alama 3)
(d) Eleza sababu sita kwa nini wanajamii wanafaa kuhifadhi kipera hiki. (alama 6)
(e) Fafanua tamathali zozote tatu za lugha katika kifungu hiki. (alama 3)
(f) Bainisha mbinu ya usambamba katika utungo huu. (alama 2)



*Kwa majibu tembelea tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke ama piga nambari kwa 0724351706*

**MTIHANI 19**
**SEHEMU YA A ;**
**SWALI LA LAZIMA-FASIHI SIMULIZI**

1.
    a) Fafanua maana ya lakabu (alama 2)
    b) Sifa za lakabu ni zipi (alama 5)
    c) Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii? (alama 3)
    d) Jadili manufaa ya utafiti katika fasihi simulizi. (alama 10)

**<u>Hadithi fupi</u>**

**Mapambazuko ya machweo na Hadithi nyingine**

2. Eleza nafasi ya vijana na wazee katika hadithi ya Mapambazuko ya machweo. (alama 20)
   Nafasi ya vijana

AU

3. 'Sasa ni saa ngapi? Si wajua mtoto angali anakusubiri? Mtoto analala!'
    a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
    b) Bainisha mtindo katika dondoo hili (alama 3)
    c) Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza maudhui katika hadithi ya Harubu ya maisha. (alama 10)
    d) Kwa hoja tatu, eleza umuhimu wa msimulizi katika kuendeleza hadithi ya mzimu wa kipwerere (alama 3)

**TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA NA TIMOTHY AREGE**

4. "…haikuwa mara moja mnavyofikiria. Ilianza pale chuoni. Wenzangu walinipa mvinyo kunirai kuonja ulevi."
    a) Eleza maudhui manne yanayojidokeza katika dondoo hili. (alama 4)
    b) Eleza athari za mhusika anayerejelewa kujitosa katika suala linalooredheshwa kwenye dondoo. (alama 6)
    c) Kwa kurejelewa mifano tano katika tamthilia ya Bembea ya maisha, eleza tofauti iliopo katika maisha ya ndoa ya zamani na sasa (alama 10)

AU

5. Jadili sababu kumi zilizompeleka mwandishi T. Arege kuandika Tamthilia hii. (alama 20)

**RIWAYA YA NGUU ZA JADI NA PROFESA CLARA MOMANYI**

6. "Samahani… Nina shida kidogo. Ninaomba usaidizi. Sikuwa nikilipa ushuru katika biashara zangu. Sasa wanataka kuzifunga na kunipeleka kotini."
    a) Eleza muktadha wa dondoo (alama 4)
    b) Bainisha toni katika dondoo hili (alama 2)
    c) Msemaji wa maneno haya na wengine ni adui ya wananchi wa Matuo. Eleza ukweli wa kauli hili. (alama 14)

AU

7. Matumizi mabaya ya mamlaka ni tatizo sugu sana katika mataifa mengi ya Afrika yanayoendelea kiuchumi. Kwa kutolea hoja mwafaka, tetea ukweli wa kauli kwa mujibu wa riwaya ya nguu za jadi. (alama 20)

8. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**.

Jiulize ni kwa nini, uanzapo kuongea
Sana sana makundini, watu hukuondokea
Ndugu ujitathmini, hakika umepotea
Sisi twakuombea, mwenye damu ya kunguni!

Mwenye damu ya kunguni, nayo lugha ya ajuza
Wengi hawamtamani, maneno yake yaliza
Yeye ana walakini, dosari kuliko pweza
Kama wewe umefunza, sote hutuona duni!

Sote hutuona duni, na hilo tumezowea
Kazi zetu zote guni, yeye tu amebobea
Umewachokoza mbuni, mateke anapokea
Sisi twakuombea, upae hadi hewani!

Upae hadi hewani, ujione kama bingwa
Mewashinda gazetini, wandishi kwako wapingwa
Yeye kwetu mpinzani, metia mipaka tingwa
Twakuombea mtafiti, hesabu hadi mizani!

Hesabu hadi mizani, utunge kwa kukosoa
U hodari hesabuni, nasi tushakuzoea
We nduli kwa majirani, na waja mekutegea
Kurekebisha hujui, ywatanika peupeni!

Ywatanika peupeni, ywajisifu mjuaji
Amezidi zetu mboni, na amevijunjia mji
Twamwachia waamuzi, kesi wasome majaji
Sisi twakuombea, sirekebike kidogo!

a) Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili (alama 6)
b) Tambua miundo wa shairi hili (alama 4)
c) Tambua bahari ya shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa maneno. (alama 2)
d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathani (alama 4)
e) Tambua aina tatu za takriri zinazojitokeza (alama 3)
f) Onyesha toni ya shairi hili (alama 1)

**MTIHANI 20**
**LAZIMA**

**1. FASIHI SIMULIZI**

**Aisei mmesikia hii kweli? Jamaa mmoja siku moja alilala fo fo fo baada ya kupiga mtindi hadi akachoka tiki! Alipofika kwake alipata mke amefura kama hamri. Kwa vile hakutaka mambo mengi, alienda moja kwa moja hadi kulala na akaanza kung'orota. Usiku wa manane uliposhika kani, msela huyu akaanza kuota kuwa yeye ni kuku na akaanza kutaga mayai kubwa kuuuubwa! Akataga yai la kwanza; akatua. Akataga la pili; akatua, alipokuwa anataga la tatu kwa nguvu zake zote, akapokea kofi moja kali na teke la ubavuni kutoka kwa mkewe. Akaamka huku akishangaa… mkewe akimlaani kwa matusi makali, " Mbona unaninyea kama mtoto? Huwezi amka kwenda chooni? Mjinga wewe! Unalewa ovyovyo kisha kuja kujiendea haja kubwa matandikoni?"**

(a) Bainisha kipera cha utungo huu kwa kutoa ithibati. (alama 2)
(b) Jadili sifa nne za kipera ulichokitambua. (alama 4)
(c) Umepewa nafasi ya kuigiza kipera hiki shuleni mwenu. Fafanua mambo manane ambayo utayaigiza kutoka kwenye kifungu hiki. (alama 8)
(d) Eleza changamoto zozote nne unazoweza kupatana nazo kama mtafiti katika kutafiti kazi za fasihi simulizi. (alama 6)

**B. RIWAYA YA NGUU ZA JADI- Clara M.**

**2. Naapa kwamba kutokea leo, mimi ni mfuasi wa Lonare. Nitampigania kwa hali na mali hadi awe mtemi wetu.**

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
(b) Eleza sababu kuu iliyomfanya mnenaji wa kauli hii kubadilisha msimamo wake. (alama 2)
(c) Kwa kurejelea dondoo hili bainisha sifa za mnenaji. (alama 4)
(d) Kwa kurejelea riwaya ya *Nguu za Jadi* onyesha jinsi jamii hii imekumbwa na usaliti.(alama 10)

**3. Mwandishi wa Nguu za Jadi ameshughulikia maudhui ya uwajibikaji kikamilifu. Onyesha jinsi alivyomhusisha mhusika Mangwasha katika kukuza uwajibikaji katika riwaya hii.** (alama 20)

**C. TAMTHILIA YA BEMBEA YA MAISHA- Timothy A.**

**4. Alama ndizo muhimu…**
**Afadhali angepunguza alama akapanda nafasi …**

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)
(b) Mbali na elimu, bainisha maudhui mengine mawili yaliyo katika dondoo hili. (alama 2)
(c) Bainisha mbinu ya lugha iliyojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)
(d) Jadili namna elimu katika *Bembea ya Maisha* imekumbwa na changamoto nyingi. (alama 12)

**5. Hayo ni ya kale…na ya kale hayanuki. Wengi hawafuati tena mila hizo. Walimwengu sasa wanavaa sare moja.**

(a) Bainisha mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)
(b) Onyesha namna sifa za mnenaji zinavyojenga maudhui mbalimbali katika tamthilia.(alama 6)
(c) Jadili athari ya mabadiliko katika jamii ya *Bembea ya Maisha.* (alama 10)

**D. HADITHI FUPI – MAPAMBAZUKO YA MACHWEO – Lutomia na Wengine**

***(Mzimu wa kipwerere)***

6. Woooooh! Woooh! Joojo! Nimewakamata! Nimewafumania, wanafiki wakubwa nyie!
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Elaza sifa za msemaji. (alama 4)
   (c) Bainisha unafiki unaojitokeza katika hadithi hii. (alama 12)

**E. USHAIRI**

7. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

DHAMIRI YANGU

Dhamiri imenifunga shingoni
Nami kama mbuzi nimefungwa
Kwenye mti wa utu. Kamba ni fupi
Na nimekwisha chora duara.
Majani niwezayo kufikia yote nimekula
Ninaona majani mengi mbele yangu
Lakini siwezi kuyafikia: kamba,kamba

Oh! Nimefungwa kama mbwa.
Nami kwa mbaya bahati, katika
Uhuru kupigania, sahani ya mbingu
Nimeipiga teke na niigusapo kwa mdomo
Mbali zaidi inakwenda na siwezi tena.
Kuifikia na nilipofungwa
Nimekwisha pachafua na kuhama siwezi

Kamba isiyoonekana haikatiki
Nami sasa sitaki ikatike, maana,
Mbuzi wa kamba alipofunguliwa, mashamba
Aliharibu na mbwa aliuma watu
Ninamshukuru aliyenifunga hapa
Lakini lazima nitamke kwa nguvu
''Hapa nilipo sina uhuru'' (***E. Kezilahabi)***

Maswali

a) Taja matatizo manne ambayo mshairi analalamikia. (alama 4)
b) Bainisha mifano ya aina mbili zifuatazo za urudiaji katika shairi hili. (alama 2)
   i. urudiaji neno
   ii. usambamba
c) Eleza maana ya ***''Kamba isiyoonekana haikatiki''*** katika shairi. (alama 2)
d) Taja na utoe mifano ya aina nne za taswira katika shairi hili. (alama 4)
e) Toa mifano miwili ya matumizi ya mistari mishata katika shairi hili. (alama 4)
f) Bainisha toni mbili kwa kutoa mifano kutoka katika shairi. (alama 4)

8. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Ilipoanza safari, ilianza kwa dhiki
Tulishikana kwa ari, kwenda safari ya haki
Tukawa ni majabari, nyoyo zisitaharuki
Tukajizatiti.

Njaa ikawa thabiti, na kiu kutamalaki
Nasi tulitia dhati, tusijali kuhiliki
Ingawa mbele mauti, dhila na mingi mikiki
Tulijizatiti.

Huu mwisho wa safari, tukaambiwa ni haki
Shangwe kwetu na fahari, utumwa hatuutaki
Kuwa mbele ya safari, juhudi iliyobaki
Tulijizatiti.

He ilikuwa ndoto, mwisho wake mafataki
Nguvu zimechomwa moto, sahala ‘mekuwa dhiki
Wagombania kipato, utashi haukatiki
Na kutabakari

Msafara ukasita, kwenye mlima wa haki
Kijasho kinatuita, mlima haupandiki
Basi sote ‘kajipeta, kukikwea kima hiki
Twataka hazina.

Tukiwa migongo wazi, tukainama kwa shaki
Tukawa’chia ukwenzi,kialeni wadiriki
Wakapanda bila ngazi, kuteremsha miliki
Wakaitapia

Wakafikia makazi, ya pumbao na ashiki
Huko wakajibarizi, kwenye raha lakilaki
Wakaisahau ngazi, ya umma ulomiliki
Mbele ya safari

Na hazina yetu sote, kuishusha hawataki
Wamo wanatema mate, kwa umati halaiki
Imezima nia yote, kiza hakitakasiki
Mbele ya safari

*[Said A. Mohammed: Mbele Ya Safari]*

<u>Maswali.</u>

a) Eleza safari inayorejelewa katika shairi hili (alama 2)
b) Onyesha kinaya cha safari inayozungumziwa. (alama 6)
c) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia: (alama 4)
   i. Mizani
   ii. Vina
d) Andika ubeti wa saba kwa lugha ya nathari. (alama 4)
e) Eleza aina mbili za uhuru wa kishairi zilizotumiwa katika ubeti wa sita na umuhimu wake katika shairi hili. (alama 4)

**MTIHANI 21**

**SEHEMU YA A: USHAIRI (ALAMA 20)**

**LAZIMA**

Na ujenge nyumba yako, jingi jasho likuoshe,
Ufyeke, upime na uweke nguzo,
Kisha paa uweke na ukandike,
Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mpaka mende usiku,
Nje na ndani ya nyumba watazunguka,
Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,
Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,
Ukae nje nzima siku usubiri,
Wazima wamelala ukirudi usiku,
Vichwa vigumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu
Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,
Na kisha wengine usiku mchana uwasake.
Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

**Maswali**

(i) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)
(ii) Eleza **muundo** wa shairi hili (alama 3)
iii) Eleza jinsi mshairi alivyoutumia **uhuru** wake katika utunzi wa shairi hili. (alama 4)
iv)Taja mbinu **mbili za lugha** alizotumia mshairi na uzitolee mifano. (alama 4)
v)Andika **ubeti wa tatu** kwa lugha nathari. (alama 4)
vi)Eleza **ujumbe** wa mshairi. (alama 2)
vii)Toa mfano mmoja wa mshororo **mshata**. (alama 1)
viii)Kichwa gani kinaliafiki shairi hili? (alama 1)

**SEHEMU YA B:TAMTHILIA**

**BEMBEA YA MAISHA (TIMOTHY M. AREGE)**

Jibu swali la 2 au 3

2.'' Lakini ndiyo tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama...kama…kama vile tambara bovu.''

a. i)Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (Alama 4 )
ii)Tambua mbinu **mbili** za kimtindo katika dondoo. (Alama 2)
b) Fafanua **umuhimu wa msemaji** katika kujenga ploti. (Alama 4)
c) **Utamanduni** huthaminiwa sana na jamii ya tamthilia ya Bembea ya Maisha. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutoa mifano **kumi** mwafaka tamthiliani. (alama 10)

3.Beni:Afadhali hao.Mjukuu wangu hatofautishi kondoo,mbuzi na mbwa.Wote hao kwake yeye ni mbwa!(*wanacheka wote)*

Yona: Inachekesha.

***Swali***

Mazungumzo haya kati ya Beni na Yona yanabainisha tofauti iliopo kati ya suala la *usasa na ukale*. Kwa kutoa mifano **kumi** inayoonyesha usasa na **kumi** inayoonyesha ukale,linganua masuala haya. (alama 20)

**SEHEMU YA C: RIWAYA**

**NGUU ZA JADI:*CLARA MOMANYI***

***Jibu swali la 4 au 5***

4.“Naweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake.”
(a)Weka dondoo hili katika **muktadha** wake. (alama 4)
(b)Tambua **maudhui** katika dondoo hili. (alama 4)
(c)Kwa kutoa mifano **kumi na miwili** mwafaka kutoka riwayani,onyesha jinsi maudhui uliyotambua hapo juu(4b) yalivyoshughulikiwa na mwandishi. (alama 12)

5. **Tamaa na ubinafsi** ni baadhi ya masuala makuu yaliyoshughulikiwa kwa mapana na marefu na *Clara Momanyi* katika riwaya yake ya *Nguu za Jadi*. Kwa kutoa mifano mwafaka riwayani thibitisha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

**SEHEMU YA D :HADITHI FUPI**

***MAPAMBAZUKO YA MACHWEONA HADITHI NYINGINE***

*Jibu swali la 6 au 7*

**WINNIE NYARURI OGENCHE:SABINA**

6.Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.
a)Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika**. (alama 6)
b)Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. (alama 4)
c)Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii. (alama 10)

**YUSSUF SHOKA HAMAD: *Mzimu wa Kipwerere***

7.“…Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama.”
(a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (Alama 4)
(b)Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (Alama 4)
(c)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (Alama 2)
(d)Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. (alama 10)

**SEHEMU YA E: FASI HI SIMULIZI**

8. a) Ulumbi ni nini? (alama 2)
ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii?. ( alama 6)
iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. (alama 6)
b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. ( alama 6)

For marking schemes and more papers contact us on 0724351706 or visit our website www.goldlitekcserevision.co.ke and download

**MTIHANI 22**

**SWALI LA LAZIMA**
**1. SEHEMU YA A: USHAIRI**
**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Amka amsha mwili,ukanyage ardhini
Amka pia akili,usingie mashakani
Amka kiwiliwili,usingizi ulaani
Amka fanya shughuli,nchi ipo hatarini

Amka wewe jasiri,hivi unalala nini?
Amka sio kuzuri,umetegemea nini?
Amka kuna dosari ,mchanga kitumbuani
Amka fanya shughuli,nchi ipo hatarini

Amka wewe jen Zi,amsha pia jirani
Amka kipya kizazi ,usikubali uhuni
Amka ufanye kazi,mkono wende kinywani
Amka fanya shughuli, nchi iko hatarini.
**(Chotara Mswahili)**

**Maswali**

**a)**Liweke shairi hili katika bahari tatu huku ukidhibitisha. (alama 3)
b)Eleza dhamira ya mshairi. (alama 3)
c)Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
d)Eleza mbinu ambazo mshairi ametumia kukidhi mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
e)Tambua mbinu tatu za lugha alizotumia mshairi. (alama 3)
f)andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari. (alama4)

**SEHEMU YA B: Tamhilia –Timothy M Arege:Bembea ya Maisha**
**Jibu swali la 2au la 3**
**2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata:**
...lakini ndio tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama... kama... kama... kama vile tambara bovu.
a)Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Eleza umuhimu wa msemaji katika kukuza ploti. (alama 4)
c)Tambua mbinu nne za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)
d)Kwa kutoa hoja nane kutoka kwa Tamthilia eleza ni vipi utamaduni ulivyothaminiwa katika jamii hii ya Bembea ya Maisha. (alama 8)

**AU**

3.Jadili nafasi ya mwanamke katika jamii ya Bembea ya Maisha. (alama 20)

**SHEMU YA C:Riwaya ya Nguu za Jadi-Prof Clara Momanyi**
**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuta ;**

*Watategemewa na nani maishani? Hiki ndicho kizazi cha kesho au kizazi kilichopotea tayari?*

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)

b)Tambua toni katika mazungumzo haya. (alama 2)

c)Onyesha ni vipi kizazi cha leo na cha kesho kilivyopotea. (alama 12)

**AU**

**5.**Fafanua ufaafu wa anwani ya ,'Nguu za Jadi'. (alama 20)

**SEHEMU YA D: Diwani ya Mapambazuko ya Machweo na Hadithi zingine.**

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6.Soma dondoo kisha ujibu maswali yanayofuata.**

*Akainama chini kwenye tendeguu moja la kitanda cha besera.Akachukua kibatari cha kiberiti ili awashe taa.Mimi,nikiwa mle mvunguni.sasa kwa hakika nilishamjua shetani wa mzimu ule ni nani.Kumbe hakuwa shetani wala Kipwerere*!

a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (alama 4)

b)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (alama 4)

c)Onyesha umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (alama 4)

d)Wanakijiji waliuogopa mzimu wa Kipwerere kiasi cha kuuabudu na kutoufanyia mzaha. Thibitisha kauli hii. (alama 8)

**AU**

**7.** Kimyakimya analikariri;

*Mteule nimechoka ,kila siku kusikiya,*
*Vyereje nchi hakika,visanga kupindukiya,*
*Tunazidi filisika ,**<u>walaji kujijaziya</u>***
*Msiba kujitakia, kweli hauna kiliyo.*

a)Huu ni ubeti wa shairi katika hadithi"Msiba wa Kujitakia'.Eleza sababu ya mwandishi kutumia mbinu hii katika usimulizi.
(alama 6)

b)Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari katika dondoo. (alama 8)

c)Bainisha maudhui mbalimbali yanayojitokeza katika kifungu hiki. (alama 6)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

**8)**. (a) Huku ukitoa mifano, eleza maana ya vitanza ndimi. (alama 2)

(b) Fafanua majukumu sita ya vitanza ndimi katika jamii. (alama 6)

(c) Eleza mbinu sita utakazotumia katika kukusanya na kuhifadhi habari kuhusu vitanza ndimi. (alama 12)

**MWISHO**



For marking schemes and more papers contact us on 0724351706 or visit our website www.goldlitekcserevision.co.ke and download

**MTIHANI 23**

## SEHEMU A: USHAIRI

**1.Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yanayofuata. (alama 20)**

**TENDA BILA UZIMBEZIMBE!**

Natakadamu kulonga , longa nawe pia longa,
Longalonga ukipinga , pinga ukunguni pinga,
Pingapinga ukipanga , panga ya kutenda panga,
Amali tenda bila uzimbezimbe.

Kazi ukipata tenda, tenda ndugu yangu tenda ,
Tendatenda kwa kupenda , penda kwa khatari penda,
Pendapenda na kupanda , panda nia njema panda,
Amali tenda bila uzimbezimbe.

Vinyago ‘ kiweza chonga, chonga kwa makini chonga,
Chongachonga ukifunga, funga midomoyo funga,
Fungafunga ukichunga , chunga gange yako chunga ,
Amali tenda bila uzimbezimbe.

Wimbo nimtamu imba , imba kwa naghama imba,
Imbaimba ukipamba, pamba kiufundi pamba
Pambapamba ukiamba, amba ya heshima amba,
Amali tenda bila uzimbezimbe.

Uwapo muwashi jenga , jenga nyumba nyingi jenga,
Jengajenga ukienga, enga muwanzoni enga ,
Engaenga ukilenga , lenga ufanisi lenga,
Amali tenda bila uzimbezimbe
Kuni upatapo chanja, chanja kwa furaha chanja,
Chanjachanja ukionja, onja pato lako onja ,
Onjaonja ukivunja, vunja wazo jiwi vunja,
Amali tenda bila uzimbezimbe

Tungo nakoma kutunga, tunga ukiweza tunga ,
Tungatunga ukilinga , linga vina vyake linga,
Lingalinga ukiwanga, wanga mizanize wanga,
Amali tenda bila uzimbezimbe.
(Malenga wa Ghuba, Fred Obondo)

**Maswali**

a) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili. (alama 2)
b) Eleza umbo la shairi hili (alama 4)
c) Kwa kutolea mifano, eleza aina mbili za uhuru wa kishairi katika shairi hili (alama 2)
d) Taja kwa kutolea mifano mbinu mbili za lugha katika shairi hili . (alama 2)
e) Eleza ujumbe wa shairi hili (alama 4)
f) Eleza toni ya shairi (alama 2)
g) Andika ubeti wa pili kwa lugha ya nathari (alama 4)
h) Eleza maana ya kibwagizo cha shairi hili (alama 2)

## SEHEMU B – RIWAYA – NGUU ZA JADI – CLARA MOMANYI

**2**. ‘’Anataka kubakia uongozini ili azidi kuwanyanyasa na kuwapoka haki zenu.’’
i) Eleza mkutadha wa dondoo hili (alama 4)

ii) Eleza sifa mbili za mhusika msemaji (alama 2)
iii) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kujenga ploti ya hadithi hii (alama 2)
iv) Kwa kurejelea hadithi hii , jadili mbinu alizotumia mrejelewa kuendelea kubaki mamlakani (alama 10)

au

**3**.Kwa kutoa idhibati, jadili ufaafu wa anwani Nguu za jadi (alama.20)

## SEHEMU YA C – TAMTHILIA - BEMBEA YA MAISHA - TIMOTHY AREGE

**4.**''Kumbe watoto hawa tuliowadharau walikuwa nyota ya jaha.Sasa kijiji kizima kina mwanga .''
**i)**Thibitisha namna watoto hawa wamekuwa mwanga kwa kijiji hiki (alama 10)
**ii**) Eleza umuhimu wa msemaji (alama 4)
**iii**) Jadili namna mwandishi ametumia mbinu ya taswira kujenga maudhui katika tamthilia ya bembea ya maisha . (alama 6)

## D . HADITHI FUPI – MAPAMBAZUKO YA MACHWEO

**5.a)**Sasa mbona wamkaribisha humu mwako nyumbani kila anapobisha ? anapokukebehi na kututafishi hapa mbona unamvumilia ? Hana shukrani yule ! Mwepuke na ujishughulishe na yako,……….. mbona hunielewi ? …………..
**i)**Eleza mkutadha wa dondoo hili . (al.4)
**ii**)Changanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili . (al.4)
**b)i**) Eleza toni inayojitokeza katika dondoo hili (al.2)
**iii**)Dondoo hili linaonyesha migogoro katika jamii . Toa mifano mitatu ya migogoro inayojitokeza . (al.6)
**iv**)Onyesha namna msemaji anachangia kujenga ploti katika hadithi hii. (al.4)

au

**c)**Kwa kurejelea hidithi zifuatazo , jadili jinsi waandishi wamemsawiri/ wamemchora mwanamke . (al.20)
**i)** Sabina
**ii**) Nipe nafasi .

## E. FASIHI SIMULIZI

**6.a)** Usiwe na pupa mwanangu , Pupa haifikishi mtu popote. Badala yake huharibu , sikiliza mwanangu . Wazazi wako walipoana, walikaa sana bila kupata mtoto . Hakuna daktari ambaye hakujaribu kutegua kitendawili cha wao kupata mtoto. Mwishowe babako akataka kumpa mamako talaka . Wazee nyumbani walimhimiza aoe tena . Lakini mimi nilimshauri asimtupe mkewe . Alinisikia maana tumekuwa marafiki wa jadi . Mamako akapatwa na mughma mkubwa . Hakujua aokote wapi mtoto.
**i**) Tambua kipera cha maelezo haya (al.2)
**ii)**Eleza sifa mbili za kipera hiki (al.4)
**iii)** Jadili majukumu manne ya kipera hiki (al.4)
**b)i**) Taja na ueleze sifa mbili kuu za mtambaji bora wa fasihi simulizi (al.4)
**ii)** Onyesha baadhi ya matatizo yanayokumba utafiti na uhifadhi wa fasihi simulizi (al.6

**MTIHANI 24**

## SEHEMU YA A: RIWAYA

***Clara Momanyi: NGUU ZA JADI***

**LAZIMA**

1. "Lakini mbona umeamua kunyamaza hivyo? Huoni watu wanakutegemea?" "…Wajua, kinywa kilichofumbwa hakiingii nzi."

a) i) Eleza **muktadha** wa dondoo hili. (alama 5)

ii) Tambua **toni** katika dondoo hili. (alama 2)

iii)Taja **mbinu moja** ya lugha katika dondoo kisha utoe mfano wa mbinu hii katika dondoo. (alama 2)

b)Mataifa mengi ya bara Afrika yanakumbwa na **matumizi mabaya ya mamlaka** ambayo ni kikwazo kikubwa katika maendeleo ya kiuchumi.Kwa kutolea mifano **kumi na moja** riwayani ya 'Nguu za Jadi',tetea ukweli wa kauli hii. (alama 11)

## SEHEMU YA B:TAMTHILIA

**Timothy Arege: Bembea ya Maisha**

*Jibu swali la 2 au 3*

2. Hata bembea ikiwa ya chuma hatimaye hulika.Wanasema papo kwa papo kamba hukata jiwe .Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo .Huungwa na mchezo kuanza tena.

a) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (alama 4)

b) Jadili **umuhimu** wa msemewa wa maneno haya. (alama 6)

c) Kwa kutoa mifano mwafaka, tambua **mbinu tatu** za lugha ambazo zimejitokeza katika dondoo hili. (alama 3)

d) Baadhi ya wahusika katika tamthlia ya 'Bembea ya Maisha',bembea yao ilipokatika **haikuunganishwa tena hivyo basi mchezo haukuendelea, ulifika kikomo**. Onyesha ukweli wa kauli iliyokolezwa wino kwa kutolea mifano **saba** tamthliani. (alama 7)

***au***

3."Wanasema mlango mmoja ukifunga ,macho huiona mingine mingi iliyokuwa wazi ambayo awali yalikuwa hayaoni."

a) i) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (alama 4)

ii) Eleza kwa kutolea hoja **nne** umuhimu wa mandhari katika tamthilia hii. (alama 4)

iii) Mnenewa ni mfano mzuri wa wahusika wasiokata tamaa maishani.Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa kutoa hoja **sita** kutoka tamthiliani. (alama 6)

b) Jadili changamoto zinazokumba asasi ya ndoa kwa mujibu wa tamthlia ya Bembea ya Maisha. (alama 6)

## SEHEMU YA C: HADITHI FUPI

D.M.Lutomia na P.Muthama:***Mapambazuko ya machweo na Hadithi nyingine***

Douglas Ogutu:**Toba ya Kalia**

4. "Asante sana kwa kitambulisho hicho.Natumai rafiki zako humu nchini wanafurahia popote walipo.Kwa niaba ya kituo hiki ninatoa shukrani kwako kwa kuitikia mwito wa kuwa nasi leo."

a) Eleza **nafasi ya vijana** kwa mujibu wa hadithi ya '**Toba ya Kalia**'. (alama 6)

b) "Hatutakukubalia kumdhalilisha mumeo,Moshe ndugu yetu kwa kuwatawanya watoto wake kwa kisingizio cha kutafuta kazi pasi na kibali kutoka kwa yeyote."

Kwa kurejelea hadithi ya '**Nipe nafasi'** jadili changamoto **sita** anazopitia mnenewa pamoja na wahusika wa jinsia yake. (alama 6)

Dominic Maina Oigo.**Kifo cha Suluhu**

c) Abigael alimaliza kusoma waraka ule huku machozi yakimbubujika kama maji kwenye maporomoko…<u>Barua ile ilimfichulia siri si haba.</u>

Thibitisha **kauli** iliyopigiwa mstari ukirejelea hadithi ya **Kifo cha Suluhu**. (alama 8)

***au***

5. D.W.Lutomia:**Msiba wa Kujitakia**

Jioni.Machoka ameketi kitako kochoni. Amerejea akiwa amechoka zaidi ya kuchoka. Pilkapilka zake za kutafuta kibarua mchana kutwa zimegonga mwamba.Hajui la kufanya. Matumbo yake yanateta kwa kushindwa kuhimili makali ya njaa. Hajatia chochote kinywani tangu asubuhi.Taswira ya chumba chake ingeweza kumliza kipofu! Anaweza juu ya maisha yake. Maisha ya wasakatonge.Maisha ya wanaojiita 'Pangu Pakavu'.Maisha ya wapiga kura. Maisha ambayo ni tofauti sana na maisha ya waliopigiwa kura.
Maisha kati ya makundi haya mawili yaani mpiga kura na mpigiwa kura, yametengana kama mbingu na ardhi. Machoka anabaki kukondoa macho huku maonevu yakiihukumu nafsi yake.Anasimama pale kama kigingi.Hasongi wala kufurukuta.

a)Kwa kutolea mifano,fafanua **mbinu sita** za kimtindo katika fungu hili. (alama 6)

b) Dokeza **suala** ambalo linajitokeza katika maneno yaliyopigwa mstari. (alama2)

c) Onyesha namna Wanamatopeni wanavyokumbwa na **madhila** kwa kurejelea hadithi ya '*Msiba wa Kujitakia.*' (alama 8)

d) Fafanua **mbinu** nne za kutambua hulka/sifa za mhusika. (alama 4)

## SEHEMU YA D:USHAIRI

*Jibu swali la 6 au 7*

6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

1. Ni sumu, sumu hatari
Unahatarisha watoto
Kwa ndoto zako leweshi
Za kupanda ngazi
Ndoto motomoto ambazo
Zimejenga ukuta
Baina ya watoto
Na maneno laini
Ya ulimi wa mzazi

2. Ni sumu, sumu hasiri
Unajeruhi watoto kwa pesa
Kwa pupa yako hangaishi
Ya kuwa tajiri mtajika
Pupa pumbazi ambayo
Imezaa jangwa bahili
Badala ya chemichemi
Ya mazungumzo na maadili
Baina ya watoto na mzazi

3. Ni sumu, sumu legezi
Unalegeza watoto
Kwa mazoea yako tenganishi
Ya daima kunywa 'moja band'
Mazoea mabaya ambayo
Ulevi
Yakufunga katika klabu
Hadi saa nane usiku baridi
Huku yakilenga kutofahamiana
Baina ya watoto na mzazi

4. Ni sumu, sumu jeruhi
Unahasiri watoto
Kwa mapenzi yako hatari
Ya kuwaliwaza watoto kwa pesa
Zinawafikisha kwenye sigara na
Na kisha kwenya madawa
Ya kulevya
Barabara inayofikisha kwenye
Giza
La kaburi la asubuhi.

**Maswali**

a) Shairi hili ni la **aina** gani? Eleza. (alama 2)

b) Masuala kadhaa yamejadiliwa katika shairi hili.Fafanua yoyote **manne**. (alama 4)

c) Kwa kutoa mifano mwafaka ,tambua mbinu **mbili** za uandishi zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 4)

d) Eleza **sura** ya shairi hili. (alama 4)

e) Andika ubeti wa **nne** kwa lugha tutumbi. (alama 4)

f) Eleza maana ya vifungu hivi vilivyotumika katika shairi. (alama 2)

i) Jenga ukuta.

ii) Kwa pupa yako hangaishi.

***au***

**7**. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata***.**

Ya wapi silika hino, ya kwenda kinyumenyume?
Nilijibu hata kwa wino, majibuyo niyasome,
Kuno 'geuza maneno, na kuyafanya maleme,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Insiya jilaani, ni bora wazi niseme,
Kukubalia idhini, mimba wakazikateme,
Hiyo nayo haki gani, wasiyoona mit ume,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.

Twajilaani laana, kijitakia ujume,
Nayo habari hatuna, twajiletea ukame,
Pia habari hatuna, ni wana sio vimeme,
Haramu kuwa halali, insani twajilaani.
Muswada siyo halali, wakuviavya vikembe,
Utawapea halali, mabinti wetu watambe,
Magulamu ja fahali, nao wakame pembe,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

Kuavya mimba ni dhambi, ya kumuudhi Rahimu,
Laana twajaza tumbi, ya moto wa jahanamu,
Tuache vino vitimbi,turudie utimamu,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

Jambo hili nawambia, litazidisha ukware,
Ni ya uvundo tabia, ni afueni tuisare,
Tuweze kuitubia, tuwache zino parare,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

Muida ndio sinao, nina mengi ya kusema,
Wapigania hakio, zingatia nayosema,
'sipashe mswada huo , ni madhambi ya kuchoma,
Haramu kuwa halali, insani twajilani.

**Maswali**

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (alama 1)
b) Changanua shairi hili **kiarudhi**. (alama 4)
c) Kwa kutolea maelezo mwafaka,tambua **bahari tatu** za shairi hili. (alama 3)
d) Bainisha mbinu zifuatazo za kimtindo katika shairi hili: (alama 3)
i) Tashbihi
ii)Tanakuzi
iii) Swali balagha
e) Dhihirisha mtunzi huyu alivyofanikiwa kutumia **uhuru** wake kwa kutoa mifano **miwili**, kisha ueleze **umuhimu** wa kila uhuru ulioutambua. (alama 4)
f) Bainisha **toni** la shairi hili. (alama 1)
g) Fafanua masuala **mawili** ambayo yanazungumziwa katika shairi hili. (alama 2)
h) Bainisha aina **mbili za urudiaji** katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU YA E:FASIHI SIMULIZI

***Jibu swali la nane***

8.a) Nyimbo zina majukumu chungu nzima katika jamii.Kwa kutoa mifano mwafaka ya nyimbo hizi,fafanua majukumu **matano** ya nyimbo. (alama 10)
b) "Kama nguo yangu moja inachukua saa nne juani kukauka, je,nguo ishirini zitachukua muda gani?"
"Jibu - ni saa moja tu kwani zinatumia jua lile lile moja kukauka."
i) Tambua kijipera hiki. . (alama 1)
ii)Taja sifa za kijipera hiki. (alama 4)
c) Umekusudia kutumia mbinu ya **kushiriki** kufanya utafiti kuhusu tungo za aina hii. Eleza **manufaa matano** ya mbinu hii. (alama 5)

**MTIHANI 26**
**SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI**

1. Lazima
   (a) Fafanua maana ya lakabu. (alama 2)
   (b) Sifa za lakabu ni zipi. (alama 5)
   (c) Kwa nini lakabu ni muhimu katika jamii? (alama 3)
   (d) Jadili manufaa ya utafiti katika fasihi simulizi. (alama 10)

**SEHEMU B: HADITHI FUPI**

**D.M. Lutomia na P. Muthama (Wah.): Mapambazuko ya machweo na Hadithi nyingine**

*Jibu swali la 2 au la 3*

2. Eleza nafasi ya vijana na wazee katika hadithi ya Mapambazuko ya machweo. (alama 20)
3. 'Sasa ni saa ngapi? Si wajua mtoto angali anakusubiri? Mtoto analala!'
   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   (b) Bainisha mtindo katika dondoo hili. (alama 3)
   (c) Eleza umuhimu wa msemaji katika kuendeleza maudhui katika hadithi ya Harubu ya maisha. (alama 10)
   (d) Kwa hoja tatu, eleza umuhimu wa msimulizi katika kuendeleza hadithi ya mzimu wa kipwerere. (alama 3)

## SEHEMU C: TAMTHILIA

**T.M Arege: Bembea ya Maisha.**

*Jibu swali la 4 au la 5.*

4. "…haikuwa mara moja mnavyofikiria. Ilianza pale chuoni. Wenzangu walinipa mvinyo kunirai kuonja ulevi."
   (a) Eleza maudhui manne yanayojidokeza katika dondoo hili. (alama 4)
   (b) Eleza athari za mhusika anayerejelewa kujitosa katika suala linalooredheshwa kwenye dondoo. (alama 6)
   (c) Kwa kurejelewa mifano tano katika tamthilia ya Bembea ya maisha, eleza tofauti iliopo katika maisha ya ndoa ya zamani na sasa. (alama 10)

5. Jadili sababu kumi zilizompeleka mwandishi T. Arege kuandika Tamthilia hii. (alama 20)

## SEHEMU D: RIWAYA

**Profesa Clara Momanyi: Nguu za Jadi**

*Jibu swali la 6 au 7.*

6. "Samahani… Nina shida kidogo. Ninaomba usaidizi. Sikuwa nikilipa ushuru katika biashara zangu. Sasa wanataka kuzifunga na kunipeleka kotini."
   (a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)
   (b) Bainisha toni katika dondoo hili. (alama 2)
   (c) Msemaji wa maneno haya na wengine ni adui ya wananchi wa Matuo. Eleza ukweli wa kauli hili. (alama 14)

7. Matumizi mabaya ya mamlaka ni tatizo sugu sana katika mataifa mengi ya Afrika yanayoendelea kiuchumi. Kwa kutolea hoja mwafaka, tetea ukweli wa kauli kwa mujibu wa riwaya ya nguu za jadi. (alama 20)

## SEHEMU E: USHAIRI

8. ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

Jiulize ni kwa nini, uanzapo kuongea
Sana sana makundini, watu hukuondokea
Ndugu ujitathmini, hakika umepotea
Sisi twakuombea, mwenye damu ya kunguni!

Mwenye damu ya kunguni, nayo lugha ya ajuza
Wengi hawamtamani, maneno yake yaliza Yeye ana
walakini, dosari kuliko pweza Kama wewe umefunza,
sote hutuona duni!

Sote hutuona duni, na hilo tumezowea
Kazi zetu zote guni, yeye tu amebobea
Umewachokoza mbuni, mateke anapokea Sisi
twakuombea, upae hadi hewani!

Upae hadi hewani, ujione kama bingwa
Mewashinda gazetini, wandishi kwako wapingwa Yeye kwetu
mpinzani, metia mipaka tingwa Twakuombea mtafiti, hesabu hadi
mizani!

Hesabu hadi mizani, utunge kwa kukosoa
U hodari hesabuni, nasi tushakuzoea
We nduli kwa majirani, na waja mekutegea Kurekebisha hujui,
ywatanika peupeni!

Ywatanika peupeni, ywajisifu mjuaji
Amezidi zetu mboni, na amevijunjia mji Twamwachia
waamuzi, kesi wasome majaji Sisi twakuombea,
sirekebike kidogo!

(a) Eleza ujumbe unaojitokeza katika shairi hili. (alama 6)
(b) Tambua miundo wa shairi hili. (alama 4)
(c) Tambua bahari ya shairi hili kwa kuzingatia mpangilio wa maneno. (alama 2)
(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathani. (alama 4)
(e) Tambua aina tatu za takriri zinazojitokeza. (alama 3)
(f) Onyesha toni ya shairi hili. (alama 1)

**MTIHANI 27**

**SEHEMU A: USHAIRI (ALAMA 20)**

**1. LAZIMA**

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo!Hutaki,
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli miania, kwako ona haitoki,
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Machungu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!
Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiliki,

Na tena ukajiona, kuwa wewe mstahiki,

Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,

Uliyataka mwenyewe!

**Maswali**

1.Shairi hili ni la **aina** gani? Eleza (alama 2)

2.Ukizingatia vigezo vifuatavyo,taja **aina za bahari** za shairi (alama 3)

i. Kibwagizo

ii. Vina

iii. Vipande

3.Tambua kwa kutoa mifano **mitatu** ya mbinu ambazo mshairi ametumia ili kutosheleza mahitaji ya kiarudhi**.** (alama 3)

4.Eleza **muundo** wa ubeti wa **tano.** (alama 4)

5.Taja na utoe mifano ya aina zozote **mbili za tamathali za usemi** zilizotumika katika shairi. (alama 2)

6.Bainisha **toni** ya shairi hili. (alama 2)

7.Andika ubeti wa **pili** kwa **lugha ya nathari**. (alama 4)

**SEHEMU B:TAMTHILIA**

**Timothy M.Arege :Bembea ya Maisha**

**Jibu swali swali la 2 au la 3**

2. "Maisha ya sasa hayana fundi.Yanamwendesha kila mtu kama tawi lililosukumwa hadi likang'oka kutoka taagani na kupeperushwa na upepo…Ulimwengu wa sasa haubagui. Wadogo kwa wakubwa".

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Huku ukitoa mifano, changanua **mbinu tano za uandishi** ambazo zimejitokeza katika nukuu. (alama 10)

c) Kukatika kwa bembea haiwi mwisho wa mchezo huunganishwa na mchezo kuendelea.

Kwa kutoa mifano **sita** onyesha jinsi wahusika mbalimbali **walivyounganisha** bembea yao ya maisha. (alama 6)



For marking schemes inox 0724351706

3. Mabadiliko katika maisha ya mwanadamu hayana budi kumfika.Wakati mwingine mabadiliko haya huleta heri au mahangaiko. Jadili kwa kutoa mifano **jinsi wahusika mbalimbali walivyokumbwa na mabadiliko haya** ukirejelea tamthilia ya ‘Bembea ya Maisha’. (alama 20)

## SEHEMU C: RIWAYA

### Clara Momanyi: Nguu za Jadi

**Jibu swali la 4 au 5**

4. “Tangu lini mke amuulize mumewe kule aendako au atokako?.....Ama kweli, wanawake wa kisasa wanavunja kila mwiko uliowekwa na wazee.”

i) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (alama4)

ii) Kwa kutoa mfano,**taja mbinu ya lugha** iliyotumika. (alama2)

iii) Eleza **umuhimu wa msemaji** (alama4)

(iv) Kwa kutoa mifano **kumi** kutoka riwayani, fafanua jinsi **mwanamke amesawiriwa** katika jamii ya Matuo. (alama 10)

5. Jamii ya Matuo katika riwaya ya ‘Nguu za Jadi’ imekumbwa na **usaliti** si haba. Kwa kutoa mifano mwafaka riwayani, onyesha ukweli wa kauli hii. (alama20)

## SEHEMU D: HADITHI FUPI

### MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE

**Jibu swali la 6 au 7**

**‘Mapambazuko ya Machweo’**

6. “Una pesa ya kulipa teksi?”

a) Eleza **muktadha** wa dondoo hili. (alama 4)

b) Taja **mbinu mbili za lugha** ambazo zimejitokeza katika dondoo hili kwa kutoa mifano. (alama2)

c) Kwa kutolea hoja **nne**, onyesha **umuhimu wa mnenewa** katika kukuza vitushi vya hadithi hii. (alama 4)

d) Eleza jinsi anwani ‘Mapambazuko ya Machweo’ **ilivyoafiki hadithi** hii kwa kutoa mifano **kumi** kutoka hadithini . (alama 10)

“**Fadhila za Punda**”



For marking schemes inox 0724351706

7. “Yu wapi kirukanjia wako? Wajua yuko wapi? Uliacha mbachao kwa msala upitao. Atakutunza nani, maana kwako fadhila za punda ni mashuzi!”

a) Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (alama 4)
b) Tambua **tamathali mbili za usemi** zilizotumika katika dondoo hili. (alama 2)
c) Fafanua **sifa zozote nne za anayeambiwa** maneno haya. (alama 4)
d) Kwa kurejelea hadithi ‘Fadhila za Punda’ onyesha **jinsi wanawake wanadhulumiwa** na jinsia ya kiume kwa kutoa **mifano kumi** mwafaka kutoka hadithini. (alama10)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

8. Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu.Wanyama hawa waliishi baharini. Mauluna alikuwa amewatunukia mapenzi si haba. Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko, matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi. Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza. Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka.

Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura. Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata. Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

**Maswali**

a)Tambua **utanzu** huu na **kipera** chake. (alama2)

b)Eleza **sifa tano za utanzu** wa kipera hiki. (alama3)

c)Eleza **umuhimu wa fomyula ya kuhitimisha** katika aina hii ya ngano. (alama 3)

d)Wewe ni fanani anayewasilisha kipera hiki kwa hadhira.Taja mambo **matatu** ambayo utafanya kuhakikisha **umefanikiwa katika uwasilishaji** wako. (alama 3)

e)Taja **manufaa mawili** ya ngano katika jamii. (alama 2)

f)Kipera hiki **kinaendelea kudidimia** katika jamii yako.Eleza **mbinu tano utakazozitumia kukidumisha** katika jamii ya leo. (alama5)



For marking schemes inox 0724351706

**MTIHANI 28**

**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI**

**SWALI LA LAZIMA.**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo;**

i) Kufa kupona.
  a) Tambua utanzu na kipera cha utungo ulichopewa. **(alama 2)**
  b) Tambua kipengele kimoja cha kimtindo katika utungo huo. **(alama 1)**
  c) Taja vigezo vyovyote vinne vya kuainisha utungo wa namna hii. **(alama 4)**
  d) Eleza dhima tatu za utungo huu katika jamii. **(alama 3)**

ii) Kakangu analilia mwituni. – Shoka
  a) Eleza muundo wa utungo huu. **(alama 2)**
  b) Eleza sifa nne za utungo huu. **(alama 4)**
  c) Unanuia kukusanya data nyanjani kuhusu kipera hiki. Eleza changamoto zitakazokukabili wakati wa shughuli hii. **(alama 4)**

**SEHEMU YA B: HADITHI FUPI**

Timothy M. Arege.: ***Bembea ya Maisha***

**Jibu swali la 2 au la 3 2.**

**2. Soma dondoo lifuatalo kisha ujibu maswali yafuatayo:**

"Unayafanya makubwa bure mwenzangu. Unafahamu vizuri kuwa hiyo si hulka yangu. Sasa mimi nina haja gani kuuvunja mji?"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

(b) Bainisha toni ya msemaji. **(alama2)**

(c) Msemaji amepitia dhiki mbalimbali katika jamii yake, Tambua dhiki alizopitia. ( **(alama4)**

(d) Onyesha namna maudhui ya mgogoro yanavyojitokeza katika tamthilia nzima**(ala10)**

**AU**

**3.** "Sasa kichwa hicho kisizunguke? Kikae pale pale ndiyo ujue ni kichwa? Kichwa kazi yake kuzunguka. Lipi lisilozungusha kichwa? Kutafuta lisilokizungusha kichwa ni kama kuwinda hewa kutaka kufumbata kwenye konzi."

(a) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 3)**

(b) Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kukuza tamthilia ya Bembea ya Maisha.. **(alama 5)**

(c) Asasi ya ndoa inakumbwa na changamoto nyingi katika maisha. Thibitisha kwa kurejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama 12)**

**SEHEMU YA C: HADITHI FUPI**

D.W Lutomia na Phibbian Muthama: *Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine*

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** "Enhee! Mpaka sasa hukupata nafasi ya kupiga simu, au angalau kutuma arafa?" "Samahani ... ulipopiga nilikuwa barabarani, singeweza kupokea simu."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama 5)**
(b) Tambua toni katika dondoo hili. **(alama 1)**
(c) Eleza vipengele viwili vya kimtindo katika dondoo hili. **(alama 2)** (d) Eleza sifa nne za aliyekuwa barabarani akapigiwa simu na kushindwa kuipokea.
( **(alama 4)**
(e) Harubu ni sehemu ya maisha ya binadamu. Hakiki kauli hii kwa hoja nane kwa kurejelea hadithi Harubu ya Maisha. **(alama 8)**

**AU**

**5.** …akikiomba radhi kile kitawi cha mti kilichonasa kwenye kazu yake ya rangi ya udongo iliyoficha kiwingu cha nongo kwa kukosa kuoshwa tangu ainunue! Nikauacha mpambano ule kati ya mzimu na mwenye dhamana ya mzimu ambao sina shaka ulidumu hadi asubuhi pale wanakijiji walipofika kushuhudia siri nzito iliyomezwa na mzimu ule waliokuwa wakiogopa na kuamini kiasi cha kuabudu kwa unyenyekevu na uchaji uliotukuka!

(a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**

(b) Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. **(alama 4)**

(c) Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo. **(alama 4)**

(d) Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha 'mwenye dhamana ya mizimu' na wenzake kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini Mzimu wa Kipwerere kiasi cha kuabudu kwa unyenyekevu na uchaji uliotukuka. **(alama 8)**

## <u>SEHEMU YA D: RIWAYA</u>

C. MOMANYI: **Nguu Za Jadi**

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6.** "Lazima amejiunga na kundi la marafiki wenye pesa wanaojaribu kumpotosha."

(a) Eleza muktadha wa dondoo. **(alama 4)**

(b) Anayesema maneno haya ni jasiri. Thibitisha kwa hoja tano. **(alama 5)**

(c) Tathmini kwa hoja kumi na moja nafasi ya wenye pesa katika kuendeleza tamaa na ubinafsi katika nchi ya Matuo. **(alama 11)**

AU

**7.** "Mangwasha siku zote hizi ulikuwa unachezeshwa kayamba tu. Ati walisema Osama alikuwa hatari kwa usalama duniani; kuna Osama kuliko huyu?" alijiskia kusema. Alishusha pumzi kwa nguvu akajiuliza kimoyomoyo kwa nini Mungu aliruhusu moto kumtia kwenye shimo la maangamizi na wanawe. Hata hivyo, aliamini kuwa wakati mwingine Mungu huruhusu mabaya kutokea ili kuwafunza waja. Waaidha, alijua kuwa mashaka yanapomkumba mja, huwa ni funzo pia. Humtayarisha kuyahimili machungu zaidi ulimwenguni ama kumuasa dhidi ya kuabudu maovu. Maovu yanapotendwa na wachache, hata wale wasio na hatia pia hujikuta wamo humo uovuni. Ni mtego wa waliomo na wasiokuwemo.

(a) Changanua mtindo katika dondoo hili. **(alama 5)**

(b) Eleza umuhimu wa mandhari ya kanisani aliko Mangwasha katika kukuza Riwaya ya Nguu za Jadi **(alama 5)**

(c) Nchi ya matuo imeshinikizwa na Nguu Za Jadi zinazorudisha nyuma usawa katika jamii. Tathmini kauli hii kwa hoja kumi. **(alama 10)**

## SEHEMU YA E: USHAIRI

**8. Soma shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali**

Mungu naomba subira, subira nayo imani
Imani iliyo bora, bora hapa duniani
Duniani mwa kombora, kombora nayo hiani Hiani
pamwe ukora wenye kuhini.

Kuhini kwenye kiburi, kiburi na ufidhuli
Ufidhuli wa kudhuri, kudhuri wangu muwili Muwili
hata kidari, kidari kuwa thakili Thakili kisinawiri,
kisinawiri misuli.

Misuli kuwa hafifu, hafifu kama muwele
Muwele wa hitilafu, hitilafi ya nduwele Nduwele
kutakilifu, kutakilifu milele Milele kutoniafu,
kutoniafu na vishale.

Vishale vinitomele, vinitomele vikwato
Vikwato pia maole, maole kufanya mito
Mito ya matozi tele, tele mithili kitoto Kitoto kilo
vipele, vipele vyenye fukuto.

Fukuto lanipa neno, neno hili kutamka
Kutamka wazi vino, vino subira kutaka Kutaka imani
mno, mno n'sipate wahaka
Wahaka wa matukano, matukano na mashaka.
Mashaka haya ya leo, leo yawe yamepita
Yamepita na vilio, vilio vipishe nyota
Nyota njema ing'arao, ing'arao kunikita Kunikita
salamani, salamani nikadata.

**Maswali:**

**(a)** Kwa nini nafsi neni inaomba subira na imani? **(alama2)**

**(b)** Shairi hili ni la aina gani kwa kuzingatia **(alama4)**
**(i)** Mpangilio wa maneno **(ii)**
Mpangilio wa vina.

**(c)** Kwa kutolea mifano eleza mbinu mbili za lugha zilizotumika katika shairi. **(alama4)**

**(d)** Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. **(alama4)**

**(e)** Kwa kutolea mifano, eleza jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa kutekeleza arudhi. **(alama6)**

**MTIHANI 29**

**SEHEMU A: FASIHI SIMULIZI**

1. a) Kwa kutumia vipengele vitano, onyesha maingiliano yaliyopo baina ya fasihi simulizi. (alama 5)
   b) Ni mambo gani huchangia kubadilika kwa kazi za fasihi simulizi?(alama 10
   c) Zitaje changamoto zozote tano za miviga katika jamii yoyote ile. (alama 5)

**SEHEMU YA B: RIWAYA NGUU ZA JADI:**

**JIBU SWALI LA 3 AU 4**

2. „„Mrima, dunia yote inajua aliyemsaliti Yesu Kristo. Unajua mtu huyo aliishia wapi?

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Tambua mbinu mbili za kimtindo zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 4)

c) Fafanua namna wahusika walivyowaendea kinyume wenzao katika riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 12)

3. Bainisha nguu mbalimbali zilizotinga maendeleo ya nchi ya Matuo kulingana na riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 20

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

**BEMBEA YA MAISHA (Timothy M.Arege)**

4. „„Walishasema baada ya dhiki ni faraja, Faraja ni zao la dhiki. Leo hii kikapu cha mama kimejaa ndago."
   a) Eleza **muktadha** wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Eleza vipengele **viwili** vya kimtindo kwenye dondoo. (alama 4)
   c) Eleza maudhui **mawili** yanayodokezwa kwenye dondoo. (alama 2)
   d) Eleza **sifa** za msemaji. (alama 5)
   e) Kwa kutolea mifano mwafaka eleza dhiki alizopitia mama ambaye sasa kikapu chake
   kimejaa ndago. (alama 5)

5. Ukilazwa tayari unakuwa umeonja seli.Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema .amri na vitisho kama askari.Unashindwa kama uuguze moyo ama ugonjwa.Katika wodi hewa iliyojaaa harufu ya dawa imezagaa,vitanda vimesalimu amri mpaka shiti zikagura.Yaani hali nzima haikupi matumaini ya kutoka ukiwa bora.matumaini yanadidimia .Tumaini lako unaliweka katika sala.

   (a) Tambua toni mbili katika kifungu hiki (alama 2)

   (b) Tambua aina moja ya taswira katika dondoo hili (alama 2)

   (c) Kando na taswira chambua vipengele vingine vya kimtindo (alama 6)

   (d) Fafanua namna mandhari ya dondoo hili yalivyochangia kujenga tamthilia ya bembea ya maisha (alama 10)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

6. **Winnie Nyaruri Ogenche; Sabina**

"Ninaomba wazazi wenzangu muwape watoto wa kike elimu badala ya kuwaoza mapema. Hongera, mwanangu kwa kupata alama mia nne arubaini na saba"

a) Eleza umuhimu wa mrejelewa katika kukuza hadithi husika (alama5)
b) Tambua mbinu ya kimtindo iliyotumika katika dondoo hili (alama1)
c) Fafanua jinsi mbinu yenyewe ilivyotumika ili kufanikisha utunzi wa hadithi (alama6)
d) Fafanua changamoto zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi (alama8)

7. a) Jadili umuhimu wa barua ya mkewe suluhu katika kuijenga hadithi ya Kifo N cha Suluhu. (alama 10)
b) Fafanua swala la ajira kama linavyojitokeza katika hadithi, Harubu ya maisha. (alama 10)

**8. SEHEMU YA E : USHAIRI**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali.***

**ADA YA MJA**

Ada ya mja, ikimnyea mvua, hulalama ,kuzilaani mbingu
Ada ya mja, ikimchoma jua, hunung"una, kutukana majira.

Ada ya mja, apatapo mali, hazimtoshi, atafyonza zaidi Ada ya mja, apatapo
cheo, hakimtoshi atapiggania ukubwa.

Ada ya mja, apatapo mke, ataongeza, hajalishwi na urembo. Ada ya mja, apatapo
mume, atamshuku, udini haumshtui

Ada ya mja, zimpandapo hamaki, hutenda, nakujutia nadae Ada ya mja zimpatapo
furaha, huhidi, na kushindwa kulipa.

Ada ya mja, kucheka kovu asiyekuwa, asiyekuwa nanajeraha Ada ya mja, kucheka
kilema, ashindwapo, hali kwao kipo.

Ada ya mja, aonapo neno, husema neno, na kupatwa na neno. Ada ya mja, kula
kutamu, kulima mavune, kwamshinda.

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? Eleza. (alama 2)
b) Bainisha nafsi neni katika shairi hili (alama 2)
c) Fafanua hulka zozote nne za mja (alama 4)
d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4
e) Tambua aina mbili za urudiaji zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)
f) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari (alama 2)

g) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)
h) Tambua mifano miwili ya methali zilizodokezwa kwenye shairi hili (alama 2)

**MTIHANI 30**

**SEHEMU YA A: USHAIRI (ALAMA 20)**

**LAZIMA**

Na ujenge nyumba yako, jingi jasho likuoshe,
Ufyeke, upime na uweke nguzo,
Kisha paa uweke na ukandike,
Siku nyingi bila kuingiliwa na mgeni hutakaa.

Wataanza kutalii mpaka mende usiku,
Nje na ndani ya nyumba watazunguka,
Bila woga, bila ruhusa ulichonacho watakula,
Masalia yatakuwa yako, ijara ya kaziyo.

Na nyingi dawa uweke, nyumba nzima uihame,
Ukae nje nzima siku usubiri,
Wazima wamelala ukirudi usiku,
Vichwa vigumu hawafi mende rahisi.

Kifo cha mende sharti miguu juu
Kichwa ukikanyage kipasuke usikie,
Na kisha wengine usiku mchana uwasake.
Mpaka watakapokwisha. Usiseme nao.

**Maswali**

(i) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)

(ii) Eleza **muundo** wa shairi hili (alama 3)

iii) Eleza jinsi mshairi alivyoutumia **uhuru** wake katika utunzi wa shairi hili. (alama 4)

iv)Taja mbinu **mbili za lugha** alizotumia mshairi na uzitolee mifano. (alama 4)

v)Andika **ubeti wa tatu** kwa lugha nathari. (alama 4)

vi)Eleza **ujumbe** wa mshairi. (alama 2)

vii)Toa mfano mmoja wa mshororo **mshata**. (alama 1)

viii)Kichwa gani kinaliafiki shairi hili? (alama 1)

**SEHEMU YA B:TAMTHILIA**

**BEMBEA YA MAISHA (TIMOTHY M. AREGE)**

**Jibu swali la 2 au 3**

2.'' Lakini ndiyo tabia yenu wanawake.Miaka inaposonga kama hivi mnatuona kama...kama…kama vile tambara bovu.''

a. i)Yaweke maneno haya katika **muktadha** wake. (Alama 4 )

ii)Tambua mbinu **mbili** za kimtindo katika dondoo. (Alama 2)

b) Fafanua **umuhimu wa msemaji** katika kujenga ploti. (Alama 4)

c) **Utamanduni** huthaminiwa sana na jamii ya tamthilia ya Bembea ya Maisha. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kutoa mifano **kumi** mwafaka tamthiliani. (alama 10)

3.Beni:Afadhali hao.Mjukuu wangu hatofautishi kondoo,mbuzi na mbwa.Wote hao kwake yeye ni mbwa!(*wanacheka wote)*

Yona: Inachekesha.

***Swali***

Mazungumzo haya kati ya Beni na Yona yanabainisha tofauti iliopo kati ya suala la *usasa na ukale*. Kwa kutoa mifano **kumi** inayoonyesha usasa na **kumi** inayoonyesha ukale,linganua masuala haya. (alama 20)

**SEHEMU YA C: RIWAYA**

**NGUU ZA JADI:*CLARA MOMANYI***

*Jibu swali la 4 au 5*

4."Naweza kuoa wakati wowote na idadi yoyote ya wanawake."

(a)Weka dondoo hili katika **muktadha** wake. (alama 4)

(b)Tambua **maudhui** katika dondoo hili. (alama 4)

(c)Kwa kutoa mifano **kumi na miwili** mwafaka kutoka riwayani,onyesha jinsi maudhui uliyotambua hapo juu(4b) yalivyoshughulikiwa na mwandishi. (alama 12)

5. **Tamaa na ubinafsi** ni baadhi ya masuala makuu yaliyoshughulikiwa kwa mapana na marefu na *Clara Momanyi* katika riwaya yake ya *Nguu za Jadi*. Kwa kutoa mifano mwafaka riwayani thibitisha ukweli wa kauli hii. (alama 20)

**SEHEMU YA D :HADITHI FUPI**

***MAPAMBAZUKO YA MACHWEONA HADITHI NYINGINE***

*Jibu swali la 6 au 7*

**WINNIE NYARURI OGENCHE:SABINA**

**6.** Maneno ya ripota huyo yalimwiingia Ombati maskioni yakasalia huko.Hayakufika akilini.Mwalimu mkuu alipenya kwenye umati uliokuwa umeanza kuwa mkubwa na kumtaka Ombati awaelekeze alikokuwa Sabina .Kabla ya Ombati kuwajibu,Sabina alifika nyumbani amevaa rinda kuukuu huku harufu ya samadi inamvuka.Watu waliokuwa wakimngoja walimzoa juujuu na kuanza kuimba tena. Ombati aliwafurusha wageni waliokuja kumwoa Sabina pamoja na mifugo wao.Baada ya kufanya hivyo,alijiunga na Sabina kuhojiwa na kupigwa picha.Alijitanua jinsi alivyotunukiwa kumlea mwana mwepesi masomoni.

a) Eleza umuhimu wa mhusika Sabina katika **kukuza hadithi husika**. (alama 6)

b) Kwa kutoa mifano mwafaka kutoka kifunguni,onyesha **aina nne za taswira** zilizojitokeza. (alama 4)

c) Fafanua **changamoto** zinazokabili jinsia ya kike kwa mujibu wa hadithi hii.

(alama 10)

**YUSSUF SHOKA HAMAD:** ***Mzimu wa Kipwerere***

7.“…Kabla mwanamke yule hajakiwasha kile kibatari,nilijitokeza mle mvunguni na maguo yangu meupe kama ya maiti nikaangua mwangwi mkali mfano wa parapanda ya siku ya kiama.”

(a)Yaweke maneno haya katika muktadha wake. (Alama 4)

(b)Fafanua umuhimu wa mandhari katika dondoo hili. (Alama 4)

(c)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili. (Alama 2)

(d)Onyesha jinsi itikadi ilivyomwezesha *mlinda mzimu na wahenga waliotukuka* kuwafanya wanakijiji kuogopa na kuamini mzimu wa Kipwerere kiasi cha kutofanya mzaha na maeneo yale ambayo mzimu uliotea.. (alama 10)

## SEHEMU YA E: FASI HI SIMULIZI

***Swali la nane***

8. a) Ulumbi ni nini? (alama 2)

ii) Ulumbi hutekeleza **majukumu** gani katika jamii?. ( alama 6)

iii) Eleza **vipengele sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. (alama 6)

b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. ( alama 6)

**MTIHANI 31**

**SEHEMU YA A :USHAIRI**

1 LAZIMA.

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Kiapo kwao majaji, wanosimamia haki
Kwa sharia ni magwiji, wahalifu hawatoki,
Wengi wao ni walaji, kwa rushwa ni mashabiki,
Kwa rushwa mashabiki.
Kiapo kwa daktari, wagonjwa hawadhiliki,
Kazi zao ni dhariri, maradhi hayakwepeki,
Na wengine ni hatari, bila pesa hutibiki,
Bila pesa hutibiki.

Kiapo cha mawaziri, kwa mbwembwe na itifaki,
Na suti zao nzuri, shingo tai haitoki,
Na wengi wana dosari, ni kwa mikataba feki,
Ni kwa mikataba feki.

Kiapo cha magavana, mikoa kuimiliki,
Hujifanya ni mabwana, wala hawasogeleki,
Nayo nchi huitafuna, na kuwa haikaliki
Na kuwa haikaliki.

Kiapo cha maraisi, kwa mizinga na fataki
Na wageni mahususi, hualikwa kushiriki,
Ikulu wakijilisi, kwa wizi hawashikiki
Kwa wizi hawashikiki.

Viapo vya utiifu, kwa sasa havistahiki
Wanoapa ni wachafu, tena hawaaminiki,
Biblia misahafu, washikapo unafiki
Washikapo unafiki

**Maswali**

a) "Dhamira ya shairi hili ni kushtumu ukiukaji wa maadili ya kikazi." Fafanua. (alama 3)

b) Eleza namna vipengele vifuatavyo vya kimtindo vilivyotumika katika shairi hili.
  (i) Usambamba (alama 2)
  (ii) Aina za taswira (alama 3)

c) Bainisha toni katika shairi hili. (alama 2)

d) Fafanua mbinu mbili alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. alama 4)

e) Ainisha bahari kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo; (alama 3)
  i. Mpangilio wa vina
  ii. Mizani
  iii. Mpangilio wa maneno

f) Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 3)

**SEHEMU YA B**

**RIWAYA : NGUU ZA JADI**

**Jibu swali la 2 au la 3**

2."*Alipotazama, zilimtafishi na kumtia kichefuchefu*"

a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (al.4)

***©kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706 au tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke***

b) Tambua mbinu mbili za uandishi katika dondoo hili.(al.4)
c) Fafanua matumizi ya mbinu yoyote uliyotambua kwa kurejelea riwaya nzima.(al.12)

**AU**

3. *".nilidhani una hekima kumbe huna hata chembe."*
   *a)* Weka dondoo hili katd«a muktadha wake. (alama 4)
   *b)* Tambua toni katd«a dondoo hili_ (alama 2)
   *c)* Tambua maudhui katika dondoo hili. (alama 2)
   *d)* Fafanua maudhui uliyotambua kwa kurejelea hadithi nzima. (alama 12)

(alama 4)

**SEHEMU YA C: TAMTHILIA**

**Jibu swali la 4 au la 5**

4. La! Kila mbegu ipandwayo haina budi kuzaa na izaapo mazao yake huvunwa. Mtu hutakasa sahani akijua itamfaa tena. Kinacholelewa hakina budi kulea
   **a)** Eleza mutadha wa dondoo (alama4)
   **b)** Chambua mtindo katika dondoo (alama4)
   **c)** Kauli iliypigiwa mstari inaonyesha majukumu ya watoto kwa wazazi. Thibitisha kwa kuonyesha wazi alivyowajibika anayerejelewa na msemaji katika mjadala. (alama4)
   **d)** Tathmini umuhimu wa msemaji katika dondoo hili katika kujenga tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama4)
   **e)** Eleza sifa tano za msemewa katika dondoo hii (alama4)
5. Fafanua mabadiliko yanayojitokeza katika tamthilia ya Bembea ya maisha (alama20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

**Jibu swali la 6 au la 7**

6. Kwa kurejelea hadithi zifuatazo, jadili maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii. (alama 20)
   a) Toba ya kalia
   b) Ahadi ni deni
   c) Nilitamani
   d) Pupa
7. Rachel wangari katika hadithi ya **Mapambazuko ya Machweo** ametumia mbinu ya jazanda kwa upana. Jadili (alama 20)

**SEHEMU E :FASIHI SIMULIZI**

8. ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Walisema waliosema
Kitali hakina macho
Huvizia wapendwa
Kikafakamia
Kwenye kinywa kisochoka
Kwa mara nyingine hasidi
Ametudhalilisha
Amewapapu kutisha wanetu
Majagina kupiga busu la sime
Jeshi letu sasa ni mateka
Wasaliti wamewapa mahasimu
Cheko la kutucheka
Nii kilio ni kilio ni kilio tangamano

a) Tambua utanzu na kipera cha kifungu hiki. (alama 2)
b) Eleza toni ya kifungu hiki. (alama 2)
c) Eleza sifa sita za kipera kinachorejelewa. (alama 6)
d) Fafanua majukumu ya kipera hiki katika uwasilishaji wa ngano. (alama 10)

**MTIHANI 32**

**SWALI LA LAZIMA ALA. 20**
**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI**

***Soma utungo ufuatao kasha ujibu maswali yanayofuata.***

Nilipokukopoa,
Cheko la mwivu wangu lilipaa sana
Ukewenza ukamshawishi kuchukua buruji kueneza habari.
"Njooni mwone jana la ajabu."
"Hajawahi kuonekana kama huyu
Tangu kuumbwa kwa ulimwengu."
Ndivyo walisema walokubeza
Kijiji kizima kilimiminika mwangu nyumbani
Kuyatuma maozi kukutazama weye
Uso na thamani walikwona,
Wakaupa unyonge moyo wangu toto,
Wakanituma kuola viungo vyako
Wakanitanabahisha upungufu ulokulemaza!
Chozi chungu likapukitika
Likalovya change kidari
Likalovya chaoko kipaji
Tabasamu ukatoa kunihakikishia
"Mimi si mjalana!
Katu sivyo wasemavyo walimwengu!"
Neno lako hili likanipa tulivu
Nikaamua alakulihali kupambana na yangu jumuiya
Ilpsema kwa moja kauli utokomezwe, chakani utupwe.
Tazameni mahasidi mloteka
Teko la dharau mlonimwaiya
Mkanitia ukiwa usomithilika!
Oleni! Tungeni macho!
Mwana mlioambaa ukoma
<lomwinga ja nyuni wala mtama, tazameni
Mekuwa malaika, anowaauni
Kiguru mlomtajia hakimzuwii kufuma mishale!
Maadui wamwonapo hutetema kama jani
Mefagia vijiji vinane kwa pigo moja la kiganja chake
Mepigana vita visohisabika
Na Wetu mahasimu waliotupoka na mifugo.

Jamii yetu sasa metawala kote
Umekuwa nahodha mwenye kubwa saburi
Akili yako nyepesi sumaku kweli kweli
Hupakata yote ya neema na shwari
Mwili wako japo lemavu,
Mesheheni nguvu za majagina mia moja!
Naposhika zana, maadui elfu huanguka!
Umeifaa jamii hii, ilotaka kuangamiza
Majagina wote, wakusujudia
Walokufurusha wamebaki hizika

***©kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706 au tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke***

Watukuka ewe shibli
Mfano wa Shaka Zulu
Alowayeyusha kama barafu.

Limwengu mzima wakujua, mwana
Alozawa kishika mkuki
Ulosema na miungu, alfajiri lipoukumbatia ulimwengu
Wla mwana jihadhari usaliti wao waja
Wasije kutosa lindini kwa nduli kukukabidhi.

**MASWALI**

a) Ainisha utungo huu kimuundo na kimaudhui. (ala. 2)
b) Eleza sifa tatu za mighani ambazo zinajitokeza katika utungo huu. (ala.6)
c) Jadili fani katika wimbo huu. (ala.5)
d) Jadili sifa za jamii iliyoizaa kazi hii. (ala. 2)
e) Ni nani anayimba wimbo huu (nafsineni)? (ala.1)
f) Eleza tofauti 4 kati ya mighani na visasili (ala.4)

**SEHEMU YA B: NGUU ZA JADI**

***Jibu swali la 2 au 3.***

**2.** "*Ajabu ni kwamba moto huo uliwaka lakini hakukuwa na dalili za moshi*"

*a)* Fafanua muktadha wa dondoo hili_ (alama 4)
*b)* Tambua mbinu katika dondoo hili_ (aalama 4)
*c)* Tambua maudhui katika dondoo hili_ (alama 2)
*d)* Kwa kurejelea riwaya nzima, Fafanua maudhui uliyotambua_ (alama 10)

**3.** "*Chukua mzigo wako wa dhambi*"

*a)* Fafanua muktadha wa dondoo hili (al.4)
*b)* Tambua mbinu ya uandishi katika dondoo hili.
*c)* Tambua maudhui katika dondoo hili. (ai.2)
*d)* Fafanua madhara ya 'inzigo wa dhambi' unaorejelewa kwa kurejelea riwayamima (al.12)

**SEHEMU CH: TAMTHILIA**

***Jibu swali la 4 au 5***

**4.** 'Nilikupata wapi? Mahututi!'

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
(b) Bainisha mbinu mbili za kimtindo zilizomo kwenye dondoo (alama2)
(c) Onyesha toni ya msemaji (alama2)
(d) Jadili changamoto alizopitia msemewa wa maneno haya (alama12)

**5.** Eleza namna wahusika mbalimbali wanakabiliana na changamoto zinazowakumba katika tamthilia ya
Bembea ya Maisha (alama20)

**SEHEMU D: HADITHI FUPI**

***Jibu swali la 6 au 7***

**6.** Ndoa ni taasisi iliyokuzwa katika hadithi fadhila za punda. Fafanua alama 20

**7.** ...wajua siku hizi huwezi kuamini yeyote apitaye na hasa akiomba msaada au umekula kututapeli?"

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
**b)** Eleza umuhimu wa msemewa wa maneno haya katika kujenga maudhui kwenye hadithi hii. (alama 10)
**c)** Eleza sifa za msemaji wa maneneo haya. (alama 5)

**SEHEMU YA E: USHAIRI**

**8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yaliyofuata.**

**a.** Jambo lolote ni nia, kuweka yako azima,
Hasa ukikusudia, kulepuka la lawama,
Mola takusaidia, kila la ovu kuzama,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**b.** Hakika si masikhara, wa kale waliyosema,
Ni maneno ya busara, tena ni wasia mwema,
Kuwa hasira hasara, ghadhabu zisizokoma,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**c.** Mja katu haitaki, hasira kuziandama,
Punguza zako hamaki, moyo uwe na huruma,
Kwani zikizidi chuki, hapo huja uhasama,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**d.** Na uhasama ujapo, uadui kukwegema,
Hapo ndipo upatapo, kukufikia zahama,
Mwisho ndipo ujutapo, ikabaki kulalama,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**e.** La usawa sinyamai, kukweleza ni lazima
Chuki nyingi hazifai, hebu tuliza mtima,
Waweza tupa uhai, au nyingi darahima,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**f.** Upunguze wako mori, mwana na mtu mzima,
Upoze moyo wa hari, hasira zipate hama,
Subira huvuta heri, ikaleta na neema,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**g.** Kifaya nilipofika, hapa ndiyo kaditama,
Sahibu wasia shika, hasira si kitu chema,
Mtegemee Rabuka, atakulinda Karima,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**MASWALI**

a) Toa anwani mwafaka kwa shairi hili. (Al. 1)
b) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia:- (Al. 4)
   i) Mishororo   ii) Vipande
c) Fafanua umbo la shairi hili. (Al. 4)
d) Dhihirisha matumizi ya idhini ya mshairi katika shairi hili. (Al. 3)
e) Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi. (Al. 3)
f) Eleza toni ya shairi hili. (Al. 2)
g) Ni nani nafsineni katika shairi hili? Eleza (Al. 1)
h) Fafanua msamiati ufuatao kama ulivyotumika shairini. (Al. 2)
   i) Mtima   ii) Darahima

**MTIHANI 33**

**1. SEHEMU YA A: USHAIRI**
**SWALI LA LAZIMA.**

1 Mbiu naipulizia, kwa wa hapa na wa ng'ambo,
Kwani ngoja 'mesikia, inaumiza matumbo,
Kwa upole sitafyoa, hata kama kwa kimombo,
Yafaa jihadharia, maisha yas,ende kambo;

2. Maisha yas'ende kombo, kututoa yetu ari,
Zingatia haya mambo, wetu walezi mukiri,
Kuwa wana kwa viambo, huwa Baraka na kheri
Watunzeni na maumbo, msijezusha hatari

3. Msijezusha hatari, na nyingi hizi zahana,
Wazazi haya si siri, mawi mnayoandama
Twaeleza kwa uzuri, matendoyo yatuuma.
Watoto tunayo mori, ni lini mtajakoma?

4. Ni nani mtajakoma, na pombe ziso halali?
Sio baba sio mama, mbona ny'hamtujali
Mwafa ja nzi twasema, mwatuacha bila hali
Hangaiko acha nyuma, kwani hamuoni hili?

5. Kwani hamuoni hili, kila mwapigana
Nyumbanizo hatulali, jehanamu tumeona
Mwatusumbua akili, twaumia tena sana
Achene na ukatili, kwani upendo hamna,

6. Kwani upendo hamna, Kama mbwa mwatuchapa
Mwatuchoma sisi wana, mioyetu yatupapa
Pa kujificha hatuna, tumebaki tukitapa
Maisha hamu hayana, timevunjwa na mifupa.

7. Tumevunjwa na mifupa, hata leo uke wetu,
Mwatubaka na kuapa, kutung'ata nyi' majitu,
Maisha hatujakopa, fahamu mkosa utu,
Hayo makeke na pupa, mtakoma utukutu,

8. Mtakoma utukutu, na kutumia mikiki,
Na tabia zenye kutu, tumechoka nayo chuki,
Hatutakubali katu, kutendewa yenya siki,
Serikali fanya kitu, kwani nasi tuna haki.

**Maswali**

a) Eleza **dhamira** ya mtunzi wa shairi hili (alama 2)
b) Fafanua tamathali nne za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 4)
c) Taja **nafsi neni** katika shairi hili. (alama 1)
d) Eleza **bahari** nne zinazowakilishwa katika shairi hili. (alama 4)
e) Andika ubeti wa nne kwa lugha **nathari**. (alama 4)

f) Eleza maudhui matatu yanayojitokeza katika shairi hili. (alama 3)

g ) Huku ukitoa mfano taja uhuru mmoja wa mshairi ambao umetumiwa katika shairi hili. (alama 2)

## SEHEMU B: TAMTHILIA

*Jibu swali la 2 au 3*

**2.** Eleza nafasi ya mbinu rejeshi katika tamthilia ya Bembea ya Maisha kukuza vipengele vifuatavyo:

a) Maudhui (alama8)
b) Ploti (alama8)
c) Wahusika (alama4)

**3.** "Ninavaa vizuri na kujivisha tabasamu ila ndani viraka na huzuni tele"

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
**b)** Tambua kipengele cha mtindo katika dondo hili (alama2)
**c)** Tambua sifa za msemewa inayojitokeza katika dondoo hili (alama2)
**d)** Eleza mambo yanayomjaza msemaji viraka na huzuni (alama12)

## SEHEMU CH:
## HADITHI FUPI: Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine

*Jibu swali la 4 au 5*

**4.** "kwa kweli, nimeungulika sana miaka yote hii kwa unyama tuliomtendea Jack.. ."

**a.** eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
**b.** jadili umuhimu wa msemaji wa dondoo hili. (alama 6)
**c.** jadili ukatili aliokuwa ametendewa mhusika jack kulingana na dondoo hili. (alama 5)
**d.** kwa kurejelea mhusika jack, jadili maudhui ya nafasi ya vijana. (alama 5)

**5.** Onyesha namna mwandishi wa hadithi ya nipe nafasi alivyodokeza maudhui ya taasubi ya kiume. (alama 20)

## SEHEMU YA D: RIWAYA:
## NGUU ZA JADI. CLARA MOMANYI

*Jibu swali la 6 au 7*

**6.** "*Alitazama jinsi kina mama wengine walijikunyata kutokana na kibaridi kile cha asubuhi*"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
b) Tambua mbinu ya lugha katika dondoo hili. (al.2)
c) Fafanua unuhimu wamandhañ ya dondoo hili- (al.14)

**7.** Eleza jinsi Mtemi Lesulia amejenga maudhui mbalimbali katika riwaya ya Nguu za Jadi. (alama 20)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8.** ***Soma hadithi hii kisha ujibu maswali***

Ilikuwa alfajiri yenye baridi. Umande ulitapakaa kote. Ukungu ulitanda hivi kwamba hungeweza kumuona mtu alikuwa hatua chache mbele yako.Ndovu alipoamka, alikuta fisi mlangoni pake. Fisi alikuwa amemlimia ndovu shamba lake, lakini alikuwa hajalipwa ujira wake.

Kila alipomwendea ndovu kwa ajili ya malipo yake, fisi alitiliwa huku na kutolewa kule."Leo ni leo",fisi alimwambia ndovu."Nimevumilia vya kutosha. Kila siku ninapokuja kuchukua pesa zangu, hukosi hadithi mpya ya kunisimulia. Leo sitoki hapa bila pesa zangu!"

Fisi alipomaliza kumwaga joto lake, ndovu alimwambia: "Sikiliza fisi. Mimi nimeheshimika kote kijijini. Naona haja yako ni kunivunjia heshima –mbele ya familia yangu na wanakijiji kwa jumla. Sikulipi pesa zako, mpaka ujifunze kuwaheshimu wazee. Nakuamuru uondoke hapa mara moja, kabla sijakasirika! Nataka uende popote, unapofikiria kwamba unaweza kupata msaada. Ukienda kwa chifu, usisahau kwamba tunakunywa na yeye. Ukienda polisi, mkuu wa kituo amejaa tele

mfukoni mwangu. Ukienda mahakamani, hakimu tulisoma darasa moja. Popote uendapo, hakuna yeyote atakayekusikiliza”
“Zaidi ya hayo, hakuna yeyote atakayekuamini.Mimi naitwa Bwana pesa.Kwangu umeota mpesapesa na kustawi. Nani ataamini kwamba naweza kushindwa kulipa vijisenti vichache ninavyodaiwa na fisi?”
Fisi alisikiliza kwa makini majitapo ya ndovu. Aliamua kumpasulia ndovu mbarika: “Bwana ndovu najua kuwa wewe una nguvu na uwezo mkubwa wa kifedha.Lakini hayo yote mimi hayanihusu ni yako na familia yako. Sitakuruhusu unidhulumu kilicho haki yangu. Usiutumie uwezo uliopewa na Muumba kuwaonea na kuwanyanyasa maskini wasio mbele wala nyuma” alimaliza usemi wake na kuondoka huku machozi yakimdondoka.

Fisi alipofika nyumbani, aliwasimulia fisi wanyonge wenzake yaliyomsibu.Fisi walikusanyika na kulizingira boma la ndovu huku wakisema: “Tunataka haki itekelezwe! Dhuluma lazima ikome! Unyanyasaji lazima ukome!” Ndovu aliposikia kelele langoni mwake, alipiga simu kwenye kituo cha polisi.

Mara, kikosi cha polisi wa kupambana na ghasi kiliwasili. Fisi walipigwa mijeledi na kuezekwa marungu. Waliojifanya mabingwa walipigwa risasi. Fisi waliosalia walikimbilia makwao, huku wakichechemea kwa maumivu. Mpaka wa leo fisi wangali wanatembea kwa kuchechemea.

**maswali**

a) Usimulizi huu ni wa aina gani? Toa sababu. (alama 4)
b) Eleza mtindo wa lugha uliotumika katika hadithi hii. (alama 4)
c) Eleza sifa za ndovu katika hadith hii. (alama 5)
d) Fafanua jinsi kisa hiki kinavyo dhihirisha methali: ‘Mwenye nguvu mpishe’ (alama 4)
e) Je, hadithi zina umuhimu gani katika jamii? (alama 3)

**MTIHANI 34**
**KARATASI YA 3 - FASIHI**
**1. LAZIMA**
***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Sahibu mwenda nyumbani, msalimu mke wangu
Mwambie ni kifungoni, huku kwa wazungu
Walonifunga katani, kutwaa uhuru wangu
Ila asihofu sana, nitarudi siku moja

Mwambie nawatamani, ninawahamu wanangu
Hata niwapo njozini, huwaona tu wanangu
Mavuno ya upeponi, ni sauti tu wanangu
Ila asihofu sana, nitarudi siku moja

Nina maradhi moyoni, niuhisio uchungu
Ni mateso mtimani, wala si vyao virungu
Nikiwaza kiamboni, huko makaoni kwangu
Ila asihofu sana, nitarudi siku moja

Mwambie anithamini, alitunze shamba langu
Lisitolewe rubuni, kwa yeyote mlimwengu
Kheri libaki porini, vimelea viwe chungu
Ila asihofu sana, nitarudi siku moja

Ukimuona hanani, hana chake wala changu
Sahibu mpe auni, kirudi takupa fungu
Wala usidai deni, kulitaka shamba langu
Ila asihofu sana, nitarudi siku moja

Sijui nikuamini, nikujuze siri yangu
Au nawe u mhuni, japo huna tena pingu
Nakwambia walakini, kam'manyishe mwenzangu
Ila asihofu sana, nitarudi siku moja

Kamwambe aole chini, chini ya ule mvungu
Kuna shimo kibulani, na ndani mna kijungu
Ya mumo humo mapeni, hiyo ndo akiba yangu
Ila asihofu sana, nitarudi siku moja

Asihofie katani, akumbuke yupo Mungu
Nitatoka gerezani, nipumue kula ndengu
Nitarudi na imani, japo yatande mawingu
Ila asihofu sana, nitarudi siku moja

Maswali
a) "ila asihofu sana…"
Fafanua kinyume kinachobainika katika dondoo hili kwa kumzingatia mtunzi wa shairi.(al. 6)
b) Kwa kutoa mfano, eleza namna toni ya utunzi huu inakuza maudhui. (al. 2)
c) Taja na ufafanue sifa zozote nne za mtunzi huyu. (al.4)
d) Onyesha namna usambamba unajitokeza katika utunzi huu. (al. 2)

e) Andika ubeti wa saba katika lugha nathari. (al. 2)

f) Huku ukitoa mifano, eleza namna idhini ya kishairi ilivyotumika kukidhia mahitaji ya kiarudhi. (al. 2)

g) Tambua nafsi neni na nafsi nenewa katika shairi. (al. 2)

## SEHEMU B: HADITHI FUPI

## Mapambazuko Ya Machweo Na Hadithi Nyingine

*Jibu swali la 2 au 3*

**2. "...iwapo penzi hili litatia doa, basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya kulitupa penzi langu kama jongoo na mti wake...**

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. (alama 4)
c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)
d) Eleza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti. (alam 6)

**3.** Kwa kurejelea hadithi ya **Ahadi ni Deni**, fafanua namna uwajibikaji umejitokeza. (alama 20)

## SEHEMU C: RIWAYA

## Clara Momanyi: nguu za jadi

## Jibu swali la 4 au 5

**4.** "*Polisi hawa wako hapa kuwalinda pamoja na mali yenu*"

*a)* Fafanua muktadha wa dondoo hili. (aL4)
*b)* Tambua mbinu ya uandishi katika dondoo hili. (aL2)
*c)* Kwa kurejelea riwaya fafanua jinsi mbinu uliyotambua imetumlka. (aL14)

**5. *"Tunafukuzwa ili turudi makwetu tujiandikishe ili tupige kura huku"***

*a)* Eleza muktadha wa dondoo hili. (aL4)
*b)* Tambua maudhui katika dondoo hili. (aL2)
*c)* Kwa kurejelea riwaya nnmaj j adili maudhui uliyotambua. (aL14)

## SEHEMU D: TAMTHILIA

## BEMBEA YA MAISHA

**6.** Eleza umuhimu wa wahusika wafuatao katika kujenga tamthia ya Bembea ya Maisha (alama20)

a) Yona
b) Dina

**7.** ***Mgaala muuwe na haki umpe***

a) Eleza muktadha wa dondoo (alama4)
b) Tambua kipengele cha kimtindo katika dondoo hili (alamal)
c) Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo uliyotaja (alama2)
d) Dhibitisha ukweli wa msemaji kwa mujibu wa dondoo hili (alama3)
e) Onyesha namna mbinu hiyo ya kimtindo ilivyotumika katika tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama10)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8.** ***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

Hapo zamani, katika enzi za mababu zetu, wanyama wote waliishi jinsi sisi binadamu tunavyoishi. Waliweza kulima, kufunga, kuchota maji na hata kupika. Wanyama wote waliishi katika jamii tofauti tofauti kwenye vijiji. Vijiji kadha, kwa pamoja viliunda milki iliyotawaliwa na mnyama mmoja aliyechaguliwa na wanyama wengine kuwa mfalme wao. Kwa kawaida, mnyama aliyechanguliwa kuwa mfalme alikuwa na sifa za kipekee. Kama vile sungura alikuwa

na werevu mwingi, Faru, Nyati na Ndovu walikuwa na nguvu za kupindukia . Simba , Chui au Duma walikuwa wakali sana.

Kulikuwa na milki mbili kubwa zaidi zilizopakana; Almasi iliyoongozwa na Simba na Dhahabu iliyoongozwa na Nyati. Milki hizi mbili zilitoshana kwa kila kitu – si ustawi wa kielimu, si wa kiuchumi, si wa miundomsingi. Wanyama wote katika milki hizi waliishi kwa mtagusano uliowawezesha kuishi kwa amani na umoja. Hili lilitiwa mbolea zaidi na kwamba viongozi wao walikuwa marafiki wa kufa kuzikana.

Hata hivyo, baada ya muda, Simba alianza kujiona kuwa alistahili eneo kubwa kuliko Nyati. Alianza kuota akiwa mfalme wa milki zote mbili. Katika ndoto zake alimwona Nyati akinyenyekea mbele yake. Alifikiri kuwa wadhifa wake ungekuwa wa juu zaidi kama angemiliki rasilmali za miliki zote mbili. Mawazo haya yalimfanya Simba kujaa chuki nyingi kila walipokutana na Nyati.

Kama wasemavyo wahenga, “Kikulacho ki nguoni mwako.” Simba alianza kumtembelea Nyati kuuliza ushauri wa jinsi wangeweza kuunda muungano wa milki zao. Nyati aliliona wazo la Simba kuwa nzuri lakini akampendekezea rafikiye kuwa wachukue muda kutafakari zaidi juu ya muungano huo. Wazo hili halikumfurahisha Simba kwani alimwona Nyati kama kizingiti kwenye ngazi yake ya madaraka. Hapo ndipo Simba alipoanza kupanga mikakati ya kumng’oa Nyati mamlakani.

Baada ta kuhakikisha kuwa mipango yake imekamilika, Simba aliamua kumvizia Nyati kumwangamiza. Hata hivyo, Nyati aliweza kuonywa na marafiki zake waliokuwa kwenye utawala wa Simba kabla ya Simba kumvamia. Alipofahamu mipango hasi ya Simba, Nyati pia aliamua kujihami ili kujikinga dhidi ya Simba. Pupa za Simba za kuongoza zilimfanya amvamie Nyati katika milki yake. Simba alikuwa amesahau kuwa mwenye pupa hadiriki kula tamu. Vita vikali kati ya milki hizi mbili vilizuka. Umoja uliokuwepo ukageuka utengano, uhusiano wao ulikuwa umeingia nyufa.

Nyati alikataa Abadan kumwachia Simba mamlaka kwa nguvu. Alihimiza kikosi chake kupigana kwa vyovyote vile ili kuhifadhi uhuru wao, jambo ambalo walilifanya kwa uwezo wao wote. Kama isemavyo, “Fahali wawili wapiganapo nyasi ndizo huumia.” Wengi waliumia wasiojua kiini cha vita hivi.

Vita vilidumu kwa muda mrefu. Kwa kawaida Nyati aliwapenda wanyama aliowaongoza kwa moyo wake wote. Kila usiku alifikiri jinsi ya kuvimaliza vita hivi ili kuepusha maafa zaidi katika milki yake. Hata hivyo, alipata na namna mbili tu za kulishughulikia jambo hili – aidha aendelee kupigana na kuwaangamiza wanyama wake wote au akubali wito wa Simba kung’atuka mamlakani. Aliamua kuwaita washauri wake kwenye makao makuu ya milki ili wajadili jinsi ya kunusuru milki yao. Washauri wake walionekana kugawanyika mara mbili. Kundi moja lilisistiza kuwa amani haiji ila kwa ncha ya upanga ilhali lingine liliona heri nusu shari kuliko shari kamili. Nyati aliwaza na kuwazua asijue la kufanya.

Hadithi yangu inaishia hapo.

***Maswali***

a) (i) Kwa kutoa mfano katika hadithi hii, eleza kwa nini ngano hii ni ya mtanziko. (al. 2)

(ii)Fafanua mitindo yoyote mitano aliyotumia msimulizi kufanikisha usimulizi wake. (al. 5)

(iii) Huku ukitoa sababu tano fafanua umuhimu wa kushirikisha hadhira katika usimulizi wa ngano kama hii. (al. 5)

(b) Onesha kwa mifano mine jinsi jamii huhifadhi kipera cha ngano sasa. (al. 4)

(c) Ni changamoto zipi zinazoweza kumkumba mtafiti akifanya utafiti wa ngano nyanjani. (al.4)

***©NAKALA HII IMEANDALIWA NA BWANA CHEPKWONY. PIGA SIMU kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706***

***©NAKALA HII IMEANDALIWA NA BWANA CHEPKWONY. PIGA SIMU kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706***

**MTIHANI 35**

**SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI**
**(*SWALI LA LAZIMA ALA. 20)***

**1. *Soma utungo ufuataao kasha ujibu maswali yanayofuata.***

Nilipokukopoa,
Cheko la mwivu wangu lilipaa sana
Ukewenza ukamshawishi kuchukua buruji kueneza habari.
"Njooni mwone jana la ajabu."
"Hajawahi kuonekana kama huyu
Tangu kuumbwa kwa ulimwengu."
Ndivyo walisema walokubeza
Kijiji kizima kilimiminika mwangu nyumbani
Kuyatuma maozi kukutazama weye
Uso na thamani walikwona,
Wakaupa unyonge moyo wangu toto,
Wakanituma kuola viungo vyako
Wakanitanabahisha upungufu ulokulemaza!
Chozi chungu likapukitika
Likalovya change kidari
Likalovya chaoko kipaji
Tabasamu ukatoa kunihakikishia
"Mimi si mjalana!
Katu sivyo wasemavyo walimwengu!"
Neno lako hili likanipa tulivu
Nikaamua alakulihali kupambana na yangu jumuiya
Ilpsema kwa moja kauli utokomezwe, chakani utupwe.
Tazameni mahasidi mloteka
Teko la dharau mlonimwaiya
Mkanitia ukiwa usomithilika!
Oleni! Tungeni macho!
Mwana mlioambaa ukoma
<lomwinga ja nyuni wala mtama, tazameni
Mekuwa malaika, anowaauni
Kiguru mlomtajia hakimzuwii kufuma mishale!
Maadui wamwonapo hutetema kama jani
Mefagia vijiji vinane kwa pigo moja la kiganja chake
Mepigana vita visohisabika
Na Wetu mahasimu waliotupoka na mifugo.

Jamii yetu sasa metawala kote
Umekuwa nahodha mwenye kubwa saburi
Akili yako nyepesi sumaku kweli kweli
Hupakata yote ya neema na shwari
Mwili wako japo lemavu,
Mesheheni nguvu za majagina mia moja!
Naposhika zana, maadui elfu huanguka!
Umeifaa jamii hii, ilotaka kuangamiza
Majagina wote, wakusujudia
Walokufurusha wamebaki hizika

Watukuka ewe shibli
Mfano wa Shaka Zulu
Alowayeyusha kama barafu.

Limwengu mzima wakujua, mwana
Alozawa kishika mkuki
Ulosema na miungu, alfajiri lipoukumbatia ulimwengu
Wla mwana jihadhari usaliti wao waja
Wasije kutosa lindini kwa nduli kukukabidhi.

**MASWALI**

g) Ainisha utungo huu kimuundo na kimaudhui. (ala. 2)
h) Eleza sifa tatu za mighani ambazo zinajitokeza katika utungo huu. (ala.6)
i) Jadili fani katika wimbo huu. (ala.5)
j) Jadili sifa za jamii iliyoizaa kazi hii. (ala. 2)
k) Ni nani anayimba wimbo huu (nafsineni)? (ala.1)
l) Eleza tofauti 4 kati ya mighani na visasili (ala.4)

**SEHEMU YA B: NGUU ZA JADI**

***Jibu swali la 2 au 3.***

**2.** *Hamtafua dafu kama ni huko mnaenda. Afisi ile imesaki wazembe ambao kazi yao ni kupokea rushwa na kufurahisha mafumbo"*

*a)* Fafanua muktadha wa dondoo hili. (aL4)
*b)* Tambua tamathali ya usemi katika dondoo hili_ (aL2)
*c)* Tambua maudhui katika dondoo hili. (aL2)
*d)* Eleza maudhui uliyotambua kwa kurejelea riwaya nzima. (aL12)

**3.** "*Pesa hubadili mtu. Pesa hubadili tabia hata yule anayedhaniwa Msalihina.* "

*a)* Fafanua mujktadha wa dondoo hili_ (aL4)
*b)* Tambua maudhui katika dondoo hili_ (aL2)
*c)* Jadili maudhui uliyotambua lava kurejelea riwaya nzima. (aL14)

**SEHEMU CH: BEMBEA YA MAISHA**

**4.** "Lakini nilivyosema, Mungu hamwachi mja wake.."

a) Eleza mutadha wa dondoo hili (alama4)
b) Tambua sifa tatu za msemewa (alama3)
c) Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya katika kukuza vipengele vifuatavyo:
   i. Ploti (alama2)
   ii. Maudhui (alama4)
d) Kwa kurejelea tamthilia nzima eleza ukweli wa kauli "Mungu hamwaachi mja wake." (alama7)

**5.** Kwa kurejelea mifano mbalimbali thibitisha namna ndoa katika tamthilia ya Bembea ya maisha zimemulika uhalisia wa jamii za kiafrika. (alama20)

**SEHEMU D: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

**6.** Fafanua jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika hadithi ya **Nipe Nafasi** (alama 20)

**7.** ***"Thank you. U mteja wa pekee, unajua kuthamini huduma nzuri unapopewa."***

**a)** Fafanua muktadha wa dondoo hili. (al.4)
**b)** Taja na ueleze mbinu mbili za kimtindo katika dondoo hili. (al.4)
**c)** Kwa kurejelea hadithi ya "kila mchezea wembe," fafanua changamoto zinazowakumba watumiaji wa vileo kupita kiasi. (al. 12)

**SEHEMU YA E: USHAIRI**

**8. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yaliyofuata.**

**a.**

Jambo lolote ni nia, kuweka yako azima,
Hasa ukikusudia, kulepuka la lawama,
Mola takusaidia, kila la ovu kuzama,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**b.**

Hakika si masikhara, wa kale waliyosema,
Ni maneno ya busara, tena ni wasia mwema,
Kuwa hasira hasara, ghadhabu zisizokoma,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**c.**

Mja katu haitaki, hasira kuziandama,
Punguza zako hamaki, moyo uwe na huruma,
Kwani zikizidi chuki, hapo huja uhasama,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**d.**

Na uhasama ujapo, uadui kukwegema,
Hapo ndipo upatapo, kukufikia zahama,
Mwisho ndipo ujutapo, ikabaki kulalama,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**e.**

La usawa sinyamai, kukweleza ni lazima
Chuki nyingi hazifai, hebu tuliza mtima,
Waweza tupa uhai, au nyingi darahima,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**f.**

Upunguze wako mori, mwana na mtu mzima,
Upoze moyo wa hari, hasira zipate hama,
Subira huvuta heri, ikaleta na neema,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**g.**

Kifaya nilipofika, hapa ndiyo kaditama,
Sahibu wasia shika, hasira si kitu chema,
Mtegemee Rabuka, atakulinda Karima,
Ukiitaka salama, jua hasira hasara.

**<u>MASWALI</u>**

i) Toa anwani mwafaka kwa shairi hili. (Al. 1)
j) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia:- (Al. 4)
 iii) Mishororo
 iv) Vipande
k) Fafanua umbo la shairi hili. (Al. 4)
l) Dhihirisha matumizi ya idhini ya mshairi katika shairi hili. (Al. 3)
m) Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi. (Al. 3)
n) Eleza toni ya shairi hili. (Al. 2)
o) Ni nani nafsineni katika shairi hili? Eleza (Al. 1)
p) Fafanua msamiati ufuatao kama ulivyotumika shairini. (Al. 2)
 iii) Mtima
 iv) Darahima

**MTIHANI 36**

**<u>SEHEMU YA A</u>**

**USHAIRI**

**1.** ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:***

**<u>UMOJA WA MENDE</u>** Wadogo tena wadudu, ila wajua kuvuna, wasikokupanda,
Wakija utawabudu, kwa sura tunafanana, wanavyojipenda,
Nyoyo zidunde dududu! Watabaki kujibana, waje kukuponda,
Mende wanao umoja, waonapo pana lishe.

Huja usiku usiku, waja wanapojilaza, wasionekane,
Huwacha yao shauku, ila wanapeleleza, wasijulikane,
Wametafuna mabuku, akili wamezijaza, nd'o tusiwaone, Mende wanao umoja, waonapo pana lishe.

Wao ni kama mapanya, huuma kipulizia, kukutulizisha,
Wanapenda kudanganya, huku mejinyamazia, kukupofuzisha,
Usiwaone waminya, kwa kutukandamizia, kwani wanachosha, Mende wanao umoja, waonapo pana lishe.

Wao huja taratibu, kwa vipindi vya misimu, vijulikanavyo,
Hurudi bila aibu, *vitano vikishatimu*, tuwapendezavyo,
Wakatutia ububu, kutulisha na vya sumu, watuongozavyo, Mende wanao umoja, waonapo pana lishe.

Tumbo lake la kiriba, tayari limeshashiba, linamusokota,
Lataka tena kushiba, wenye nyumba tuna tiba, tutamuokota,
Wakishatupa kibaba, kina mama kwa wababa, si tunajitata,
Mende wanao umoja, waonapo pana lishe.

Mwishowe tunafungua, apite akaingie, ndani kabatini,
Humo mlimo murua, twataka atuchungie, vyetu vya thamani,
Mwishowe anararua, ndani amejifungie, wamtakiani?
Mende wanao umoja, waonapo pana lishe.

Hubeba na familia, wana na bibi za kwake, wale kwa pamoja,
Nasi tukivumilia, kufikike kule kwake? Ng'o! sekunde moja,
Hadi ije kufikia, kuosha kabati lake, hapa tu pamoja, Mende wanao umoja, waonapo pana lishe.

Kachukuwe yake dawa, mende tukawakatae, tukawafukuze,
Tuseme tunazo mbawa, nd'o mende tuwakomee, siye tujikuze,
*Tuwang'atue machawa*, tuseme tuondokee, tukawachukize, Mende na wao umoja, tuje wapa redikadi.

**(Kutoka: Meja S. Bukachi – Diwani ya Kupe) MASWALI**

a) Tambua mende wanaorejelwa na mshairi. (Alama 1)
b) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (Alama 1)
c) Nani nafsi nenewa katika shairi hili? (Alama 1)
d) Taja tamathali za lugha zilizotumika katika shairi hili. (Alama 2)
e) Fafanua uhuru wa ushairi alioutumia malenga. (Alama 2)

f) Weka shairi hili katika bahari mbalimbali. (Alama 3)

g) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (Alama 4)

h) Tambua mambo manne anayolalamika nafsi neni kuhusu mende. (alama 4)

i) Vifungu vifuatavyo vina maana gani katika shairi? (alama 2) i. vitano vikishatimu ii. Tuwang'atue machawa

**SEHEMU YA BRIWAYA: NGUU ZA JADI**

(Clara Momanyi) Jibu swali la ***Pili*** au la ***Tatu***

**2.** Eleza jinsi Sagilu amejenga maudhui ya tamaa katikati riwaya ya Nguu za Jadi. (aL20

**3.** "*Tangu lini mke akamuuliza mumewe kule atokako au aendako?*" (aL8)

*a)* Weka dondoo hili katika muktadha wake. (aL4)

*b)* Tambua tamathali ya usemi katika dondoo hili. (aL2)

*c)* Tambua maudhui katika dondoo hili. (aL2)

*d)* Kwa kurejelea hadithi nzima, Fafanua maudhui uliyoitambua

**SEHEMU CH: BEMBEA YA MAISHA**

**2.** Naam, bembea! Hata ikiwa ya kamba au chuma hatimaye hulika. Wanasema papo kwa papo kamba hukata jiwe. Bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo. Huungwa na mchezo kuanza tena.

a) Jadili dhana 'bembea inapolika na kukatika haiwi mwisho wa mchezo. (alama10)

b) Jadili namna wahusika tofauti wanavyounga bembea (alama10)

**3.** Wewe unajua vote valivosemwa. hadharani na faraghani. Si makanisani, si magweni. leo nikiviona vitoto hivi vilivyochekwa na kusimangwa jana, vikijiendeshea mambo yao ninaridhika"

(a) Bainisha matokeo ya maneno yaliyopigiwa mstari (alama6)

(b) Eleza sifa za mwanawe msemewa(alama4)

(c) Kwa hoja kumi, jadili namna suala la malezi lilivyoangaziwa katika tamthilia. (alama10)

**SEHEMU D: MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

**4.** Fafanua dhana ya ajira katika hadithi Mapambazuko ya Machweo (alama 20)

**5.** **"mwanangu, nizike duniani unifunike…"**

**a)** Fafanua muktadha wa maneno haya. (al.4)

**b)** Taja na utolee mfano mbinu moja ya kimtindo inayojitokeza katika dondoo hili (al.2)

**c)** Ukirejelea hadithi ya" **Mzimu wa Kipwerere**," fafanua jinsi imani katika mambo ya kichawi yamejikita katika jamii. (al. 14)

**SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI**

***8. Soma utungo ufatao kisha ujibu maswali***

"Hapo zamani za kale, kale sana kabla ya ujio wa manabii Issa, Musa ama hata Yesu, walimwengu wote waliishi pamoja kama ndugu na dada. Hakukuwepo haya makabila tunayoyasikia yakitajwa kila siku. Hakukuwepo na utabaka. Hapakuwepo na maskini. Watu wote waliishi pamoja kama wafanyavyo wanyama wa familia moja. Hakukuwepo na tofauti na tamaa ya uongozi na kujitakia kwa wananchi. Ubinafsi.

Mwanadamu alipogundua umoja aliopewa na Mungu wake, alianza kusoma mengi mno na kutaka kujua mengi kuhusu Mola. Alidhani kwamba Mungu aliishi mbinguni. Hivyo basi, wanadamu wote waliitana pamoja katika kamkunji; mkutano wa siri, waratibu jinsi wangeweza kumfikia mwenyezi Mungu. Mwisho wa kikao, walikubaliana kuwa waanze kujenga ukuta mkubwa ambao ungewawezesha kufika juu mbinguni na kuzungumza moja kwa moja na Mola Mkuu.

Siku iliyofuatia waliingia katika kazi. Huyu alileta jiwe hili na huyu msumari huu. Kazi ilifanywa kwa kujitolea na jitihada kuu kila mmoja akiamini kuwa atakaye kilicho mvunguni ni sharti ainame. Aidha, mgaagaa na upwa hali wali mkavu. Ukuta wao ulipanda kwa kasi. Wazee wenye busara walijaribu kuwaonya wajenzi dhidi ya hatua hii yao ila wakashikilia msimamo wao wa kutaka kuonana na Muumba wa mbingu na ardhi ana kwa ana.

Mungu alipoona kuwa mwanadamu amejawa na kiburi, aliwachanganya wajenzi kwa kuzichanganya lugha zao. Hili liliwanya kutoelewana kiasi kwamba fundi mmoja alipoomba aletewa bisibisi alileletewa nyundo. Hatimaye ukuta mzima ulianguka na kuwaangamiza wajenzi na waliosalia wakabaki kutoelewana lugha zao. Hii ndiyo sababu wanadamu wana lugha tofauti."

***Kutoka: Meja S. Bukachi- Mola Mkuu (Riwaya)***

**Maswali**

(a)Tambua kipera hiki cha hadithi. (Alama 2)

(b) Wewe ni mtafiti uliye nyanjani kwa uchunguzi zaidi kuhusu kipera hiki:

(i) Taja mbinu tatu utakazotumia katika utafiti wako. (Alama 3)

(ii) Upi umuhimu wa kukusanya na kuhifadi tungo kama hizi? (Alama 5).

(iii) Taja njia tano zinazotumiwa na jamii ya kisasa kuendeleza fasihi simulizi. (alama 5)

**MTIHANI 37**
**SEHEMU A : HADITHI FUPI**
**MAPAMBAZUKO YA MACHWEO NA HADITHI NYINGINE**

1. Wafanyikazi katika nchi nyingi zinazoendelea wanakumbwa na changamoto nyingi sana. Thibitisha hali hii kwa kurejelea hadithi ya " harubu ya Maisha(alama 20)

**SEHEMU B : RIWAYA, NGUU ZA JADI**
**Jibu swali la 2 au la 3.**

2. Fafanua jinsi Sagilu amejenga maudhui riwavani. (Al 20)
3. "*Ukiwa na tabasamu utapata chochote na kwenda popote duniani."*
   *a)* Fafanua muktadha wa dondoo hili_ (aL4)
   *b)* Eleza sifa za msemaji wa maneno haya. (aL4)
   *c)* Fafanua jinsi msemaji alichangia kuporomosha jamii yake. (aL12)
      (i) Vitisho
      (ii) Ufuska/ Uzinzi
      (iii) Ukiritimba
      (iv) Uchochezi

**SEHEMU CH: BEMBEA YA MAISHA**

4. (a)Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama10)
   (b)Mwanamke ni nguzo imara katika ujenzi wa jamii. Eleza kauli hii ukirejelea tamthilia ya Bembea ya Maisha (alama10)
5. Basi tu! Wenzenu ndio walioniingiza kwenye mkondo huu. Kama unakumbuka nilikuwa miongoni mwa vijana kwanza kuingia kwenye dini. Hata tulikuwa tunahubiri.
   a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama4)
   b) Tambua kwa kutolea mfano wa toni inayojitokeza katika muktadha huu. (alama2)
   c) Kwa kurejelea mifano mbalimbali eleza madhara au matokeo ya maneno ya yaliyopigiwa mstari katika tamthilia hii kwa jamii husika (alama14)

**SEHEMU D: USHAIRI**
Jibu swali la 6 au la 7.

**6.** ***Soma shairi lifuatalo kasha ujibu masuali***

1. Mkata ni mkatika, harithi hatorithiwa
Sina ninalolishika, wala ninalochukuwa
Mlimwengu kanipoka, hata tone la muruwa!
Mrithi nini wanangu?

2. Sina ngo'ombe sina mbuzi,sina kondesi na buwa
Sina hata makaazi, mupasayo kuyajuwa
Sinamazurimakuzi, jinsi nilivyoachiwa
Mrithi nini wanangu?

3. Sina kazi sina bazi, ila wingi wa shakawa
Sina chembe ya majazi, mno ni kukamuliwa
Nakwa'cheni upagazi, mgumu kwenu ku'tuwa
Mrithi nini wanangu?

4. Sina sikuacha jina, mkatahatasifiwa
Hata nifanye la mana, mno ni kulaumiwa
Poleni wanangu sana, sina kwenu cha kutowa
Mrithi nini wanangu?

5. Sina leo sina jana, sina kesho kutwa liwa
Sina zizi sina shina, wala tawi kuchipuwa
Sina wanangu mi sana, la kwacha nakuraduwa
Mrithi nini wanangu?

6. Sina utu sina haki, mila yangu meuliwa
Nyuma yangu ilidhiki, na mbele imekaliwa
N'na wana na mikiki, hadi n'tapofukiwa
Mrithi nini wanangu?

7. Sinai la kesho kwenu,wenyewe kuiongowa
Muwane kwanyingi,mbinu Mwende pasi kupuwa
Leo siyo, keshoyenu,kama mutaji kamuwa
Mrithi nini wanangu?

(Kina cha maisha A.S.Mohammed)

**MASWALI**

a) Eleza hali ya mzungumzaji katika shairi hili ( alama 4)
b) Eleza dhamira kuu ya mshairi kulitunga shairi hili (alama 2)
c) Ni nani anayezungumziwa na nafsi neni katika shairi hili? (alama 2)
d) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)
e) Fafanua mbinu tatu za lugha zilizo tumiwa katika shairi hili (alama 3)
f) Tambua bahari ya shairi hili ukizingatia. (alama 4)
   a. Mizani
   b. Vina
g) Andika ubeti wa mwisho kwa lugha ya tutumbi (alama 3)

**7. Soma shairi lifuatalo kasha ujibu masuali**

Jama, Jama, Jamani
Mbona twabebeshwa mateso hivi
Mizigo mikubwa ya dhiki kama
Kwamba hatuna haki ya kusema
Kukataa ndoa za lazima
Kukataa kuozwa wazee
Kukataa kukatishwa masomo
Kukataa tohara ya lazima

Jama, Jama Jamani
Iweje tuteswe mateso haya
Na watu wasio kuwa hata na haya kama
Kwamba hatuna haki ya kulalamika
Kulalamikia kutumikishwa kama mayaya

Kulalamikia kudhalilishwa kiunyama
Kulalamikia kutolindwa na sheria

Jama, Jama, Jamani
Sasa hii ni awamu nyingine
Na macho tumeyafungua kabisa
Tumekataa kudhalilishwa kabisa
Tumekataa kuteswa kama watumwa
Tumekataa tohara ya lazima
Tumekataa kuozwa....... Tumekataa! Tumekataa
Hii awamu ya 'Haki ya mtoto wa kike'

**Maswali**

a) Hili ni shairi la aina gani? (alama 1)
b) Taja na ueleze mambo matatu muhimu yaliyozungumzwa na mshairi (Alama 3)
c) Eleza muundo wa shairi hili (Alama 4)
d) Taja mbinu mbili za lugha alizotumia mshairi kufanikisha shairi lake (Alama 4)
e) Kwa nini mshairi huyu anasema hii ni 'awamu' nyingine? (Alama 3)
f) Eleza matumizi ya mishata katika shairi hili (alama 2)
g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa na mshairi (alama 3)

(i) awamu
(ii) kudhalilishwa
iii) Dhiki

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8**. a) Wewe ni mwigizaji wa michezo ya jukwaani. Eleza mambo sita ambayo utazingatia ili kufanikisha uigizaji wako. (alama 6)

b) Mbinu ya uigaji sauti ina umuhimu gani katika fasihi simulizi: (alama 4)

c) Soma utungo ufuatayo kisha ujibu maswali. (alama 10)

Mwananguuu , ni wewe kweli !
ndimi niliyekupa uhai mwana unoringia,
Anokufanya upite ukinitemea mate,
Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,
Miungu na waone uchungu wangu,
Radhi zao wasiwahi kukupa
Laana wakumiminie,
Uje kuzaliwa mara mia na wanao,
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,
Wakazamwanao wasikuuguze katika utu uzimawake
(kutoka – Fani ya Fasihi Simulizi)

**Maswali**

i)Tambua kipera hiki cha Fasihi simulizi (alama 1)
ii)Eleza sifa zozote nne za kipera hiki cha Fasihi Simulizi (alama 4)
iii) Eleza kwa kutoa ithibati jinsia ya nafsineni? (alama 1)
iv)Fafanua umuhimu wa kipera ulichokitaja hapo juu katika jamii. (alama 4)

**MTIHANI 38**

**SEHEMU A(SWALI LA LAZIMA)**

**A: USHAIRI**

.**Soma ushairi ufuatao kisha ujibu maswali**

1.

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyatubu
Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha wenye raha na tabu,ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina,Saidi Ali Rajabu
Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, Ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni  kiwanja wenye dini, wamtiio wahabu
Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu
Mapadiri kanisani, huvihubiri vitabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa na moyo kisebusebu
Tunakaribia kuja, kwa kushindwa kujimudu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
Na wengine sitotaja, msinambe ninagubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha  wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

**Maswali**

*©kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706 au  tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke*

(a)Lipe shairi hili anwani ifaayo. (alama 1)
(b) kwa kutoa mfano, eleza mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika shairi.(alama 2)
©Eleza jinsi uhuru wa mshairi ulivyotumika katika shairi. (alama 2)
(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (alama 4)
(e)Taja na ueleze bahari zozote mbili zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)
(f)Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
(g)Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)
(h)Fafanua dhamira ya mshairi. (alama 2)
(i)Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi. (alama 2)
(i) Malofa:
(ii) Udubu:

**SEHEMU YA B: NGUU ZA JADI– CLARA MOMANYI**

**Jibu swali la 2 au la 3**

**2.** ***"Siku hizi kila mtu anazisaka chapaa, haijalishi kwa njia gani ilimradi maisha yamnvokee"***
   *a)* Eleza muktadha wa dondoo hili_ (aL4)
   *b)* Kwa kurejelea riwaya nzima, thibitisha kuwa wahusika hawakunyookewa na Maisha(aL16)

**3.** ***"Unampa pesa kidogo na kumwonyesha mahaba ya pesa nane naye anadhani unataka kumwoa."***
   *a)* Fafanua muktadha wa dondoo hili. (aL4)
   *b)* Tambua maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili. (al. 10)
   *c)* Jadili nafasi ya msemaji wa maneno haya katika kujenga maudhui riwayani. (aL6)

**SEHEMU CH: HADITHI FUPI-MAPAMBAZUKO YA MACHWEO**

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** **..iwapo penzi hili litatia doa, basi nirudishie mfuko huu kama ishara ya kulitupa penzi langu kama jongoo na mti wake..."**
   a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
   b) Fafanua mbinu mbili ambazo zimetumika katika dondoo hili. (alama 4)
   c) Eleza sifa sita za msemaji wa maneno haya. (alama 6)
   d) Eleza umuhimu wa msemewa wa hadithi hii katika kujenga ploti. (alama 6)

**5.** Wanaume katika mataifa mengi barani afrika wametawaliwa na ubabedume. Jadili kauli hii ukirejelea hadithi ya **"Fadhila za Punda**" (al.20)

**SEHEMU D: BEMBEA YA MAISHA**

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6.** "Kumbuka mrina haogopi nyuki. Marehemu mamangu alozoea kutuambia kuwa nguvu hazimwishi mwanadamu wala hazipotei bure; humalizwa tu na mabuu... usifanye hofu. Nikujuavyo mimi, hukuingia katika bahari si yako. Wala hakuna refu lisilokuwa na ncha. Yote yanakikomo eti. Ipo siku haya yote yatapita. Mkulima hodari ni libasi yake huwa imechakaa na kuchoka lakini moyoni anabaki safi kama theluji kwa kutosheka na tija ya sulubu zake. Huwezi kumlinganisha na mkulima wa nguo safi zilizopigwa pasi zikanyooka"
   (a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama4)
   (b) Tambua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo. (alama4)
   (c) Eleza sifa za msemaji (alama6)
   (d) Tambua maudhui mawili yanayojitokeza katika kifungu hiki. (alama2)
   (e) Fafanua maudhui katika swali la (e) kwa kurejelea tamthilia nzima. (alama4)

**7.** Timothy Arege amewajenga wanaume kwa njia hasi na chanya. Jadili kauli hii kwa kutolea mifano kutoka kwenye tamthilia (alama20)

## SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

**8. . Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Ndimi Nguli, dume la ukoo mtukufu
Ulojipambanua kwa mabingwa
Wachezaji hodari wa ngoma
Ndimi dume liloingia nyanjani
Makoo yakatetemeka
Yakang'ang'ania gozi kusakata nami.

**Maswali**

(a) Tambulisha kipera kinachojitokeza katika kifungu hiki. (alama 2)
(b) Eleza sifa tano bainifu za kipera hiki katika fasihi simulizi. (alama 10)
(c) Fafanua umuhimu wa kipera hiki. (alama 8)

*©kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706 au tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke*

**MTIHANI 39**

**LAZIMA**

**SEHEMU A: USHAIRI**

**1.** ***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Kiapo kwao majaji, wanosimamia haki
Kwa sharia ni magwiji, wahalifu hawatoki,
Wengi wao ni walaji, kwa rushwa ni mashabiki,
Kwa rushwa mashabiki.

Kiapo kwa daktari, wagonjwa hawadhiliki,
Kazi zao ni dhariri, maradhi hayakwepeki,
Na wengine ni hatari, bila pesa hutibiki,
Bila pesa hutibiki.

Kiapo cha mawaziri, kwa mbwembwe na itifaki,
Na suti zao nzuri, shingo tai haitoki,
Na wengi wana dosari, ni kwa mikataba feki,
Ni kwa mikataba feki.

Kiapo cha magavana, mikoa kuimiliki,
Hujifanya ni mabwana, wala hawasogeleki,
Nayo nchi huitafuna, na kuwa haikaliki
Na kuwa haikaliki

Kiapo cha maraisi, kwa mizinga na fataki,
Na wageni mahususi, hualikwa kushiriki,
Ikulu wakijilisi, kwa wizi hawashikiki
Kwa wizi hawashikiki.

Viapo vya utiifu, kwa sasa havistahiki
Wanoapa ni wachafu, tena hawaaminiki,
Biblia misahafu, washikapo unafiki
Washikapo unafiki

***Maswali***

a) ''Dhamira ya shairi hili ni kushtumu ukiukaji wa maadili ya kikazi.'' Jadili. (alama 3)

b) Eleza namna vipengele vifuatavyo vya kimtindo vilivyotumika katika shairi hili.
   (i) Usambamba ( alama 2)
   (ii) Aina za taswira ( alama 3)

c) Bainisha toni katika shairi hili. (alama 2)

d) Fafanua mbinu **mbili** alizotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya kiarudhi katika shairi hili. (alama 4)

e) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo; ( alama 3)
   i. Mpangilio wa vina
   ii. Mizani
   iii. Mpangilio wa maneno

f) Fafanua muundo wa shairi hili. (alama 3)

**SEHEMU YA B:**

**Bembea ya Maisha-Timothy Arege**

*Jibu swali ya pili au tatu*

**2.** Eleza nafasi ya mbinu rejeshi katika kuikuza tamthilia ya Bembea ya maisha (alama20)

**3.** "Maisha ya sasa hayana fundi. Yanamwendesha kila mtu kama tawi lilsilosukumwa hadi likang' oka kutoka tagaani na kupeperushwa na upepo"

- ***a)*** Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
- ***b)*** Tambua vipengele vya kimtindo katika dondoo hili (alama2)
- ***c)*** Eleza sifa nne za msemewa (alama4)
- ***d)*** Thibibitisha kauli ya msemaji ukirejelea tamthilia nzima (alama10)

**SEHEMU YA CH**

**Mapambazuko ya Machweo na Hadithi Nyingine**

*Jibu swali ya nne au tano*

**4.** Urumo umekita mzizi katika jumuiya ya **Mapambazuko ya Machweo**. Jadili alama 20

**5.** ***Miti katika misitu ilizidi kuangamizwa kwa makali ya shoka lakini miti ilizidi kulifurahia shoka...miti ikafikiri shoka ni mmoja wao*!"**

a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
b) Bainisha mbinu zozote mbili katika mkutadha huu. (alama 4)
c) Eleza sifa mbili za shoka. (alama 2)
d) Kwa kurejelea hadithi ya msiba wa kujitakia, jadili mbinu zinazotumiwa na viongozi kuingia mamlakani. (alama 10)

**SEHEMU YA D**

**Riwaya NGUU ZA JADI- CLARA MOMANYI**

***Jibu swali moja kutoka sehemu hii.***

**6.** "*Kila neno lililoandikwa lilikuwa kama dhoruba kali juu ya kisu moyoni mwake.*"

- *a)* Weka dondoo hili katika muktadha wake. (aL4)
- *b)* Tambua mbinu katika dondoo hili. (aL2)
- *c)* Fafanua matumizi ya mbinu uliyotambua kwa kurejelea riwaya nzima. (aL14)

**7.** a.Fafanua nafasi ya Mbungulu katika kujenga maudhui riwayani. (alama 10)
b. Dhihirisha kuwa Bi Mbungulu ni mwaminifu kwa kurejelea riwaya nzima (al.10)

**SEHEMU YA E**

**Fasihi simulizi**

**8.** ***i)Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

"Mwanangu, dunia haitaki papara. Ikiwa unataka kufanikiwa katika mustakabali wako kuwa mtoto mtiifu na mwongofu. Kumbuka kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu…"

a) Tambua na ueleze kipera hiki cha fasihi (alama 2)
b) Eleza sifa tatu za kipera hiki. (alama 3)
c) Fafanua dhima tano za kipera hiki katika jamii. (alama5)

ii) Fanani anawezaje kuihusisha hadhira katika usimulizi wake?(alama 4)

iii) Eleza utaratibu unaofuatwa wakati wa kutega na kutegua vitendawili. (alama 6)

***©kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706***

**MTIHANI 40**
**SEHEMU A: USHAIRI**
**SWALI LA LAZIMA**
1.**Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Ulimwengu ulimwengu, ulimwengu naratibu
Yaliyo kichwani mwangu, nataka kuyatubu
Wayasome ndu zangu, wa mbali na wa karibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ulimwengu ni kiwanja, cha wenye raha na tabu
Wengine wanajikonja, kwa wengine ni adhabu
Kucha na kutwa twahanja, kutafuta matulubu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa balaa, aliniusia babu
Mna mambo yamejaa, ya faraja na kusibu
Na machache ya kufaa, ila mengi ya udubu
Cha wenye raha na tabu,ulimwengu ni kiwanja.

Ni kiwanja cha Amina,Saidi Ali Rajabu
Wengine kitu hatuna, tunaishia kababu
Wale wamejaza sana, wanashindwa kuhesabu
Cha wenye raha na tabu, Ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa urongo, na kweli pia ajabu
Kichwa hudanganya shingo, tumbo kiuno chasibu
Usitumai ubongo, wa nduguyo na swahibu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa walevi, pombe kwao ni dhahabu
Mara vile mara hivi, wakilewa majudhubu
Maneno ya kiujuvi, hujipaka hata shabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni  kiwanja wenye dini, wamtiio wahabu
Mashekhe msikitini, humo humfanya muhibu
Mapadiri kanisani, huvihubiri vitabu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa malofa, lofa mtu mwenye tabu
Kusema sana kashifa na moyo kisebusebu
Tunakaribia kuja, kwa kushindwa kujimudu
Cha wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

Ni uwanja wa faraja, alowajali habibu
Na wengine sitotaja, msinambe ninagubu
Ni uwanja wa viroja, vigumu kuvikutubu
Cha  wenye raha na tabu, ulimwengu ni kiwanja.

***©kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706 au  tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke***

**Maswali**

a) Lipe shairi hili anwani ifaayo. (alama 1)

b) kwa kutoa mfano, eleza mbinu zozote mbili za lugha zilizotumika katika shairi.(alama 2)
c) Eleza jinsi uhuru wa mshairi ulivyotumika katika shairi. (alama 2)
d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha tutumbi. (alama 4)
e) Taja na ueleze bahari zozote mbili zilizotumika katika shairi hili.(alama 2)
f) Eleza umbo la shairi hili. (alama 4)
g) Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)
h) Fafanua dhamira ya mshairi. (alama 2)
i) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika shairi.(alama2)
    i. Malofa:
    ii. Udubu:

**SEHEMU B: RIWAYA-NGUU ZA JADI**

***Jibu swali la pili au la tatu***

**2.** "*Lakini afadhali tuukabili ukweli ingawa mchungu ili tusambaratishe mbegu ya chuki."*
*a)* Fafanua muktadha wa dondoo hili_ (al-4)
*b)* Tambua maudhui katika dondoo hili. (aL2)
*c)* Fafanua jinsi maudhui uliyotambua yamejitokeza katika riwaya nzima (aL14)

**3.** "*Shetani ni wewe mwenyewe. Shetani wa mtu ni mtu."*
*a)* Weka dondoo hili katika muktadha wake (aL4)
*b)* Thibitisha ukweli kuwa shetani wa mtu ni mtu kwa kurejelea riwaya nzima. (aL16)

**SEHEMU CH: BEMBEA YA MAISHA**

***Jibu swali la nne au la tano***

**4.** Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. Siku hazigandi wala jana haitarudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baaada ya kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuilewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. Kwaheri pombe. Buriani.
***a)*** Changanua mtindo (alama6)
***b)*** Tambua maudhui yoyote matatu yanayojitokeza kwenye kifungu (alama6)
***c)*** (Tambua toni mbili inayojitokeza kwenye dondoo hili (alama4)
***d)*** Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya

**5.** "Imani na itikadi huthaminiwa sana na jamii ya watu". Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea tamthilia ya bembea ya Maisha (alama 20)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

**Mapambazuko ya Machweo Na Hadithi Nyingine**

**6.** Fafanua changamato wanazokumbana nazo waajiriwa katika hadithi **Harubu ya Maisha** (alama 20)

*AU*

**7.** Jadili matumizi ya pombe haramu na athari zake katika hadithi kila mchezea wembe (alama 20)

***©NAKALA HII IMEANDALIWA NA BWANA CHEPKWONY. PIGA SIMU kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706***

***©kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706 au tovuti www.goldlitekcserevision.co.ke***

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI.**

**8. Soma makala yafwatayo kisha ujibu maswali yafwatayo**

Hapo zamani za kale, paloindokea mtu mmoja kwa jina mzee Kata. Mzee Kata alikuwa na wake wawili. Mke wa kwanza aliitwa Neema na wa pili aliitwa Nduli. Kila mmoja wa wake hawa alikuwa na mtoto mmoja. Neema alikuwa na mtoto wa kike kwa jina Majaliwa. Majaliwa alikuwa ameumbwa akaumbika.Uso wake ulihimili macho meupe mfano wa theluji. Meno yake ya juu yalipangika kwa njia ambayo iliyafanya kuacha mwanya ambao ulifanya tabasamu yake kuwa ya mvuto wa sumaki. Urembo wa Majaliwa, kama walivyosema wengi, ungemtoa nyoka yeyote pangoni.

Kwa upande mwingine Kutu, bintiye Nduli, alikuwa mwenye sura mbaya ya kutisha.Uso wake usiopendeza ulimfanya kuonekana kama ajuza wa miaka mia moja! Tabia yake ya ukorofi ilikoleza mvuto wake hasi. Vijana wa kijijini walimfanyia inadi kila mara kwa kumkumbusha kuwa hakufaa kuringa. "Sura kama kiboko", wangemtania

Tofauti za kiumbo kati ya Majaliwa na Kutu zilizua uhasama mkubwa kati ya ndugu hawa, sikwambii mama zao. Hali hii ilizidishwa Zaidi na nongwa za kila siku zilizotokana na ukewenza. Familia yam zee Kata ikawa medaniya vita vya wenyewe kwa wenyewe.

Hali ya mtafaruku iliendelea kuikosesha nyumba yam zee kata amani. Asubuhi moja, Mzee Kata aliamka kama kawaida yake, alijikohoza kama isharaya kutangaza kufika kwake. Daima hakupenda kuzungumza na wakeze asubuhi na mapema. Aliamini kuwa wangemletea nuksi. Kinyume na siku nyingine, mzee Kata hakuitikiwa. Ilibidi kujikaribisha nyumbani mwake. Mara tu alipovuka kizingiti cha kijumba hicho, alitupa macho yake juu yakitanda cha mayoweambapo mke wake alijinyosha twaa kakauka kama ukuni; hanapumzi. Weupe wa macho yake na mapovu yaliyomtoka kinywani yalimhakikishia Mzee Kata kuwa Neema kampungia mkono. Harufu kali ya sumu ilihanikiza hewa kumwarifu kuwa Mzee kata kuwa mkewe kafa kwa kutendwa na mkemwenza

Maisha ya Majaliwa yalichukua mkondo mpya baada ya tanzia hii. Mama wa kambo sasa alipata mwanya wa kumhini majaliwa. Kazi zote za nyumbani aliachiwa yeye.Huku Kutu akiachwa huru kucheza. Majaliwa alipewa chakula hapa; wengine wakila biriani yeye alipewa wali wa kawaida. Mavazi yake yaligeuka matambara.Siku zilivyozidi kusonga ndivyo mateso yalivyoongezeka. Mama wa kambo alizidisha wivu wake kwa majaliwa. Hata Majaliwa alipovunja ungo na wachumba kuja kumposa, mama wa kambo aliwafukuzia mbali. Wenine walihimizwa kumposa Kutu. Wachumba waliochachawa kutaka kumuoa majaliwa wakidai kuwa hawamtaki Kutu kwa sababu ya kiburi chake, walinyeshewa matusi, wakahizinika na kujiendea zao.

Siku moja alitokea kijana mmoja makini .alikuja amavalia gwanda jeusi lililojiinamia kwa uchovu. Viatu alivyovaa vilikuwa vimejichokea kwa kupiga lami. Kofia iliokuwa kichwani pake ilitosha kumhakikishia mama wa kambo kuwa huyu alikuwa fakiri. Mama mtu alikubali mara moja posa ya kijana huyu kwa Majaliwa akijua kuwa angeadhibika. Aliamini amemtokomeza Majaliwa ndani ya lindi la ulitima. Mzee Kata naye hakusita kumwoza Majaliwa kwa kiajana huyu maana aliiona hii kama fursa ya pekee ya kumwepusha vitimbi vya mama wa kambo

Majaliwa aliandamana na mume wake hadi Kijiji cha peponi ambako kijana huyu allishi. Wallingia katika nyumba ya msonge ambamo Majaliwa alitarajia kuanza Maisha ya ndoa. Walitayarisha chajio, wakala na kulala.

Asubuhi, Majaliwa aliamshwa na nyimbo za ndege. Alipofunguamacho, alijikuta kalala ndani mya chumba chenye sakafu ya vigae. Ukuta wa chumba hicho ulikuwa wa rangi wa zari. Mapambo ya dhahabu yalitundkwa ukutani. Kumbe kijana aliyemuoa hakuwa maskini kama ilivyodhaniwa! Alikuwa mwana wa mfalme! Na hili lilikuwa kasri hasa! Majaliwa hakueza kuamini! Alikuwa ameamkia Maisha ambayo hakuwahi yawazia.

Alipoingia sebuleni alimpata mama yake mpenzi, akiwa na tabasamu ya milele usoni. Walikumbatiana kwa shauku kuu. Kumbe kijana huyo alikuwa ametumwa na mamake Majaliwa!

Mumewe majaliwa alishuhudia kwa umbali. Machozi ya mama mtu na mwanawe yakilovya vifua vyao na kuyeyusha simanzi na kuyeyusha simanzi iliyokuwa imeyaandama Maisha yao. Tangu siku hiyi, watu hawa wallishi kwa raha mstarehe. Hadithi yangu inaishia hapo.

**MASWALI**

a) Taja na utolee mifano mbinu sita za kimtindo zilizotumiwa katika utungo huu (al.3)
b) Utungo huu unaweza kuainishwa kama ngamo, toa sababu (al.1)
c) Fafanua umuhimu nne wa formula ya kumalizia katika utungo huu (al. 4)
d) Taja shughuli moja ya kijamii katika jamii ya utungo huu (al. 1)
e) Jadili tatizo moja la ukewenza katika utungo huu (al.1)
f) Taja na ufafanue dhima tano ya utungo huu katika jamii yake (al.5)
g) Taja mambo mawili ambayo fanani anaweza kutekeleza ili kuufanya utungo huu uwe wa kuvutia Zaidi (al. 1)
h) Miviga ni nini? (al.1)
i) Taja hasara tatu za miviga (al.3)

***©NAKALA HII IMEANDALIWA NA BWANA CHEPKWONY. PIGA SIMU kwa majibu piga simu kwa nambari 0724351706***